Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi – Tarehe 22 Juni, 2009**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika ( Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI, SERA, UTATIBU NA BUNGE:**

Hotuba ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadilio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI, WIZARA YA ELIMU NA MAFUZO YA UFUNDI (MHE GAUDENSIA M. KABAKA):**

Taarifa ya Mwaka, Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Mzumbe; kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2008 (*The Mzumbe University Annual Report and Accounts for the year ended 30th, June, 2008*).

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Ahsanteni sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ahsante sana.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa anayeuliza swali la kwanza, nawakaribisha tena Ukumbini, baada ya mapumziko ya *week end*, natumaini mmerudi na nguvu mpya, kukabiliana na changamoto za kawaida zilizomo ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

Kwa njia ya pekee, napenda nimkaribishe sana nyumbani na pia hapa Bungeni Ukumbini, Mheshimiwa Naibu Spika, aliyekuwa anatuwakilisha kule Cairo, kwenye Mkutano wa Maspika wote wa Bonde la Mto Nile.

Mkutano ulikuwa, tuseme mkali sana na niwadokezee tu kwamba baadhi ya watu kule Wabunge, wamechukizwa sana na sisi Tanzania kuchukua maji ya Ziwa Victoria kufikisha Shinyanga na Kahama. Kwa hiyo, ni mambo ya namna hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, Naibu Spika anaandaa taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ataiona na Serikali ijiandae, kwa sababu Waziri wa Maji wa Misri anakuja hivi punde kwa mambo hayo hayo.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana. Sasa swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Na. 75

### Haki za Viongozi wa Serikali za Vijiji na Vitongoji

**MHE. JACOB D. SHIBILITI (MISUNGWI)** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka huu 2009 tutakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa; na kwa kuwa Viongozi hawa sehemu kubwa wamekuwa wakijitolea tu hawapati chochote.

Je, haki yao hasa ni shilingi ngapi na mlipaji ni nani hasa; au wao ni Viongozi wa kujitolea tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

MheshimiwaSpika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji ni Viongozi wa kijamii (*Civic Leaders),* ambao huchaguliwa kupitia tiketi za vyama vyao vya siasa.

Viongozi hao huchaguliwa kwa kuzingatia sifa kama zilizoelekezwa kwenye Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa. Kimsingi, uzoefu umeonyesha duniani kote kwamba Viongozi wa kijamii, hufanya kazi kwa kujitolea. Aidha, kwa mujibu wa Sheria za Tanzania, moja ya sifa ya watu wanaogombea uongozi wa kisiasa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kuwa na kipato halali kinachomwezesha kuendesha maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Viongozi wa ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa, hufanya kazi yao ya kuwakilisha wananchi kama Viongozi wa Kijamii kwa kujitolea na kwa kuzingatia uzalendo walionao kwa jamii.

Hata hivyo, Serikali kwa kutambua mchango wao katika jamii ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha na kuwaongoza wananchi kushiriki katika shughuli za kijamii za maendeleo ilielekeza kuwa mapato yanayokusanywa na Halmashauri ndani ya kijiji, asilimia 20 ya mapato hayo inabaki/ibakie katika Kijiji na yanapaswa kutumika kama ifutavyo:-

(i) Asilimia 3 posho ya Mwenyekiti;

(ii) Asilimia 3 posho ya Mwenyekiti wa Kitongoj;i na

(iii) Asilimia 14 kugharamia uendeshaji wa Ofisi za Kijiji na kuchangia katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufutwa kwa vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyokuwa vinakusanywa kutoka kwenye kila Kijiji. Halmashauri zinalazimika kuendelea kutoa kiasi cha asilimia 20 ya mapato yanayotokana na vyanzo vyao na

sehemu ya ruzuku; inayotelewa kama fidia ya vyanzo vilivyofutwa na kurejesha kwenye Vijiji na Mitaa ili kugharamia shuguli za uendeshaji zikiwemo posho za viongozi wa kijamii kama nilivyoelezwa hapo juu. Aidha, kwa kuzingatia dhana ya Upelekaji wa Madaraka kwa Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kuamua ni kiwango gani cha posho kinafaa kuwalipa Viongozi wake wa kijamii. Uamuzo huo usiathiri huduma zinazopaswa kutolewa kwa jamii.

**MHE. JACOB SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, yeye mwenyewe amekiri kwamba shughuli zinazofanywa na viongozi hawa ni kubwa na ni nyingi sana. Lakini yapo matatizo ambayo, pamoja na kwamba Serikali inaendelea kutoa ruzuku ile ya asilimia 20, lakini zipo Halmashauri ambazo, bado hazipeleki pesa hizo kwenye vijiji husika.

(a) Je, anaagiza nini yeye kama Waziri, kwenye Halmashauri hizo zinazofanya makosa hayo?

(b) Kwa kuwa asilimia 20 ni ndogo sana ukilinganisha na shughuli zao, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa kuna kila sababu ya kuongeza asilimia hiyo, ili angalau waweze kuendelea kujitolea kama wanavyojitolea? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwanza kabisa nikubaliane na Mheshimiwa Shibiliti kwamba, kazi wanayofanya Wenyeviti wetu wa vijiji na Wenyeviti wetu wa Vitongoji ni kazi nzuri na ambayo tunaipongeza sana hapa nchini. Viongozi hao, wamekuwa wanafanya kazi hiyo katika mazingira magumu, natambua kwamba kama anavyosema kweli kuna Halmashauri zingine ambazo inafika mahali unakuta kwamba hazitoi hata hiyo asilimia 20 inayozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba, kwa upande wa Misungwi, ninayo barua. Tena wao wamefanya vizuri zaidi, faili ninalo hapa. Hii barua imeletwa kwetu na Mkurugenzi Mtendaji, kwamba Wenyeviti wa Vijiji, walipwe asilima 50 ya fedha zinazopelekwa kutoka kijijini na Wenyeviti wa Vitongoji asilimia 30. Mimi hapa nimesema asilimia 3, lakini nimesema kwamba Halmashauri, zinapewa uhuru wa kuamua wafanyeje. Wanayo asilimia 30 ambayo inatokana na ushuru unaotokana na samaki nayo wanai–*retain* pale. Pamoja na asilimia 20. Nataka niseme kwamba, hawa wanafanya vizuri na wanaonesha mfano mzuri.

Mheshimiwa Spika, Sasa swali lilizoulizwa hapa, wale ambao hawafanyi hivyo, wanakwenda kinyume cha Sheria. Wanakwenda kinyume cha Sheria na kwa niaba ya Meshimiwa Waziri Mkuu, nawaomba Wabunge kama mnawafahamu, ambao ushuru umeshachukuliwa, asilimia 20 ambayo ilitakiwa ibakie pale, hawakupewa. Na ile asilimia

20 ambayo inatokana na ile fidia wanayopewa, hawakupewa tungeomba, tupate majina yao, tupate majina ya hao wanahusika, kwa maana ya Halmashauri ili tuweze kuchukua hatua zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ambalo linazungumzia kuhusu asilimia 20 kwamba bado ni kidogo, na mimi nakubaliana na yeye Mheshimiwa Spika. Pale kwako Urambo, asilimia 20 itategemeana na kwamba mlikusanya kiasi gani. Sasa hili ni jambo linalohusu masuala ya Bajeti, nafikiri ni jambo ambalo tunaweza tukalitazama sisi wote kwa pamoja; tukaona kiwango hiki. Kwa sasa huu ndio msimamo wa Serikali ambao naufahamu, lakini naamini kwamba Serikali imesikia, na tutazingatia ushauri huu, anaoutoa mwenzetu Mheshimiwa Shibiliti. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri Naibu Waziri anafahamu, mwanzoni ku-*calculate* asilimia 20 ya mapato, yanayotokana na vijiji ilikuwa rahisi. Lakini ruzuku inayoletwa na Serikali, inakuwa tayari imeshapangiwa vitu vya kufanya. Maana yake iko *budgeted*. Sasa nilikuwa nafikiri, je, Naibu Waziri, ili kuifanya Halimashauri iweze kutimiza wajibu wake wa kutimiza asilimia 20. Kwa nini wanapotoa ruzuku, wasifanye hesabu ya asilimia 20 tayari kwenye ile ruzuku kusudi iandikwe rasmi; kwamba hii ni asilimia 20 inayotakiwa kwenda kwenye vijiji?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tuelewana hapa kwamba hii asilimia 20, labda nitaje jina lake, ni ile inayoitwa *General Purpose Grant*; ndio tunazungumzia hapa. Na najua kwamba Mheshimiwa Estherina Kilasi, ni mtaalamu katika masuala ya hesabu ndio maana ana *pose* hili swali analo li-*pose* hapa. Anachosema, ni kwamba wakati unapoileta ile, na wakati unapozileta zile hela pale, weka katika *calculations* zako kabla na iingie pale.

Mimi nadhani haya ni mawazo mazuri, tutayafanyia kazi, ili sasa ikienda, iende sehemu kubwa; kwa sababu, kweli utakuta sehemu kubwa, kwanza inabaki pale kwenye Halmashauri, na kwa hiyo kunakuwa na haya mapunjo. Na nadhani ni jambo ambalo tunaweza tukalitizima, ili kuimarisha ule mfuko uweze kuendeleza shughuli katika maendeleo katika vijiji vyetu.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji anapata asilimia 2 peke yake. Lakini kwa kuwa Wenyeviti wa Vitongoji hugawana zile asilimia 3 wote kwa pamoja, haoni kwamba kuna kuwapunja hao Wenyeviti wa Vitongoji kwa sababu kuna vitongoji vingine vingi viko kwenye vijiji na Mwenyekiti wa Kijiji anapata nyingi zaidi kuliko Wenyeviti wake wa Vitongoji ambao ndio wanafanya kazi zaidi kuliko Mwenyekiti wa Kijiji.

Je, haoni kwamba arekebishe hili Wenyeviti wa Vitongoji na wenyewe wapate pesa nyingi zaidi kama ambavyo kazi yao ilivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, asilima nilizozitaja hapa kwanza nakubaliana na yeye. Hiki anachozungumza, naiona hoja yenyewe. Mwenyekiti wa Kijiji ni mmoja katika kijiji. Lakini Wenyeviti wa Vitongoji ni wengi, na asilimia tuliyoisema hapa kama Serikali, ni asilimia 3 kwa Mwenyekiti wa Kijiji, na asilimia 3 kwa ajili ya Wenyeviti wa Vitongoji. Mheshimiwa Selelii anaposema kwamba kweli ukiwapa wale asilimia 3 ile na Mwenyekiti ukampa ile nyingine yote amebakia nayo, wale kwa sababu ni wengi, kiasi kile kinakuwa ni kidogo. Mimi nakubaliana naye, lakini maana kubwa zaidi ya hapo, tunalolizungumza hapa, kwanza kile kiasi ambacho wao wenyewe wanatoza, kwa sababu bado kuna ushuru ambao unatozwatozwa pale katika *level* ya kijiji.

Jinsi unavyotaja kiwango kikubwa, ndivyo unavyo *retain* kiwango kikubwa kwa maana asilimia 20 na jinsi tunavyopeleka kwa maana hii Mheshimiwa Mheshimiwa Estherina Kilasi, alichokuwa anazungumza hapa, unavyopeleka kiasi kile kwa kuangalia hiyo *formula* aliyozungumza, maana yake kiasi kitakuwa ni kikubwa.

Lakini nadhani nakubaliana na yeye, kwamba kama unampelekea mtu mmoja, mwenyekiti wa kijiji pale na wale wengine unawapelekea asilimia ile ile, ni kweli kwamba kuna haja ya kulitizama tena upya. Sasa haya ni mawazo, ni ushauri mzuri, tutaufanyia kazi ili tuweze kuona. Lakini nadhani kubwa zaidi ni kuzalisha, ili tuweze kutoza ushauri mkubwa zaidi na tuweze kuwaona hawa wote ambao ni muhimu.

Na 76

**Mindombinu ya Hifadhi ya Selous Kuboreshwa**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa Hifadhi ya Wanyamapori ya *Selous* ni Hazina ya Dunia (*World Heritage*).

(a) Je, Serikali ina Mpango Mkakati gani wa kuboresha miundombinu ndani ya Hifadhi hiyo ili kuwa Bora?
(b) Je, Serikali inapata mapato kiasi gani na inapoteza mapato kiasi gani kwa mwaka?

(c) Je, kuna mpango kamilifu wa kunyanyua vipato na hali ya maisha ya wanavijiji vya Ngorongo, Nyaminywili, Mtanza/Msona, Mwaseni na Mloka?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Idrisa Mtulia, Mbunge wa Rufiji, swali lake lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Mpango Mkakati wa kuboresha miundombinu ndani ya Hifadhi ya *Selous*, ni kukarabati miundombinu iliyopo pamoja na kuongeza mingine kulingana na uwezo wa Bajeti. Kila mwaka ukarabati unafanyika katika Pori la Akiba la *Selous*, ili kuboresha miundombinu mbalimbali zikiwemo barabara, viwanja vya ndege na majengo.

Pori linao mtandao wa barabara unaofikia kilomita 20,000 ikilinganishwa na mtandao wa kilomita 25,000 za barabara unaohitajika katika pori zima.

Mtandao huo unafanikisha shughuli za utawala, doria, utalii wa picha,uwindaji wa kitalii na usafirishaji. Pia ukarabati unafanyika kwa viwanja vya ndege ishirini na mbili (22) vinavyotumika kutoa huduma kwa watalii wa picha, wawindaji wa kitalii na shughuli za utawala.

Wizara imekuwa ikiongeza Bajeti ya kutengeneza barabara kila mwaka. Katika kipindi cha miaka sita (6) kati ya mwaka 2002 hadi 2007 zilitengwa fedha Tsh. 60,000,000/= hadi 365,000,000/= sawa na asilimia 6.35 hadi 18.73 ya Bajeti ya *Selous* kwaajili ya ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege.

Aidha, ili kuboresha na kukidhi mahitaji ya nyumba za watumishi katika Pori la Akiba la *Selous*, jumla ya nyumba 96 zimejengwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, (*African Development Bank(ADB)*. Wizara itaendelea kuboresha miundombinu na jinsi au kadri Bajeti itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, pori la Akiba la *Selous*, linachangia katika pato la Serikali kutokana na shughuli za uwindaji wa kitalii na utalii wa picha. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2002 hadi 2007, jumla ya watalii 55,204 walipokelewa katika Pori la *Selous*. Kati yao, Watalii wawindaji walikuwa 3,675 na Watalii wa picha walikuwa 51,529; ambao waliliingizia Taifa pato la jumla ya Tsh. 8,471,817,294 na pia *USD. 14,973,964.*

(c) Mheshimiwa Spika, katika kunyanyua vipato na hali ya maisha ya wanavijiji wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi, wananchi wa vijiji vya Ngorongo, Nywaminywili, Mtanza/Msona, Mwaseni na Mloka, walishaunda Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori iitwayo, *JUHIWANGO* ambayo ilisajiliwa kwa nambari SO. 14218, tarehe 24 Machi, 2006. Kinachotakiwa kufanyika ni kuandaa mpango wa matumizi bora ya malihai katika eneo hilo ili wananchi waishio katika vijiji hivyo waweze kuanza kunufaika na mpango huo wa ushirikishwaji na hatimaye kuinua vipato na hali ya maisha ya wananchi hao. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana na vilevile nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini nimepata mshangao mkubwa sana, kwa pori linalotoa bilioni 8, *investiment* ya kutengeneza pori hilo ni milini 300 yaani hata bilioni 1 haikufika.

(a)Je, kwa mwendo huu, lini pori hili litakuwa na barabara madhubuti, hizo barabara ulizotaja, hatujui ni za aina gani, Changarawe, tope au lami? (*Makofi*)

(b)Mheshimiwa Spika, ni wazi kabisa kwamba tangu mapato mengi yanapopatikana haya ya kutoka *Sealou*, wananchi wale wa vijiji vilivyotajwa, hawajapata faida yeyote mpaka Juhiyango ijikamilishe. Je, ikimaliza kujikamilisha italipwa fidia tangu mwaka ilipoanza kukusanya fedha mpaka wakati itakapo jikamilisha? Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, barabara madhubuti, kwa hivi sasa napenda niseme kwamba barabara zilizopo, zinapitika wakati wote, isipokuwa labda sehemu ambazo zisizo na barabara, na barabara hizi zote ni za changarawe ambayo imechanganyika na udongo wa kawaida.

Lakini mimi wiki iliyopita nilikuwa huko kuzikagua zina hali nzuri na sasa hivi zinapitika hata viwanja vya ndege sasa hivi vina hali nzuri na vinatumika, ila tu napenda tu kusema kwamba, tutazidi kuongeza udhubutu wa hizi barabara na kuongeza zingine zilizobakia jinsi ambavyo kadri ya pesa zitakavyoongezeka na hali ya uchumi itakavyozidi kuimarika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda kusema kwamba, kwa sasa hivi Wilaya ya Rufiji, ikiwemo na Vijiji vyote alivyovitaja, wananufaika na asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii na kwa upande wa Rufiji, napenda kusema kwamba, katika mwaka 2005/2006 jumla ya Tsh. milioni 21,200, 290 walipatiwa Halmashauri ya Rufiji, kwa ajili ya vijiji husika.

Lakini mwaka 2006/2007 pia walipatiwa Tsh. Milioni 26, 800,058 na pia mwaka 2007/2008 walipatiwa Tshs. milioni 9, 400,078 jumla ya zote hizi kwa upande wa Rufiji wameshapata Jumla ya Tsh. Milioni 57,537,292. Hata hivyo kwa mwaka 2008/2009 tuliishapeleka mapendekezo kwa Wizara ya fedha, ili Rufiji waweze kupewa jumla ya Tsh. Milioni 50 na taarifa niliyoipata ni kwamba, bado hazijagawiwa.

Na. 77

**Utekelezaji wa Mkukuta Nchini**

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, MKUKUTA ni Mkakati wa Kupunguza na Kukuza Uchumi Tanzania:-

(a) Je, ni Watanzania wangapi ambao ni maskini na wangapi ni matajiri?

(b) Je, tangu tuanze kutekeleza MKUKUTA, ni maskini wangapi wamekuwa matajiri?

(c) Je, Serikali inatumia vigezo gani kupima kuwa mtu fulani ni tajiri na mwingine ni masikini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali namba 37 la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, tarehe 15 Juni, 2009, nililielezea Bunge lako Tukufu kuwa, mwaka 2007 wakati idadi ya Watanzania ilikuwa 38.3 milioni, waliokuwa maskini ni asilimia 16.5. Hata hivyo, kwa upande wa idadi ya matajiri, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania pamoja na nchi nyingi duniani haina idadi ya matajiri na hii inatokana na kwamba, hatupimi utajiri bali tunapima umaskini. Kwa maana hiyo, idadi ya Watanzania ambao ni matajiri takwimu hiyo haipo isipokuwa asilimia 50.1 ya Watanzania walionekana wanajiweza kwa mahitaji yao muhimu. (*Makofi*)

(b)Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wanne (4) tokea tumeanza kutekeleza MKUKUTA, kama nilivyojibu katika sehemu (a), hatuna takwimu za matajiri, takwimu zilizopo ni idadi ya Watanzania walio katika hali ya kujiweza. Kwa maana hiyo, tokea kuanza kwa MKUKUTA, asilimia 2.3 ya Watanzania walionekana hali zao zimetoka katika umaskini na kuwa katika hali ya kujiweza.

(c)Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika katika kufahamu mtu gani ni maskini ni kushindwa kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula na mahitaji mengine kama vile makazi, elimu, tiba, mavazi, maji safi na salama.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba, nchi yetu haipimi matajiri na kwa kuwa, kile mabacho unanuia ndicho ambacho unakipata.

(a) Je, kwa nini sasa hivi Serikali haioni haja ya kupima matajiri na kuwatambua, ili tuwe na matajiri wengi nchini?

(b) Kwa kuwa Watanzania wengi sana tunauchukia umasikini napenda kumwuliza Naibu Waziri. Nini kifanyike, tufanye nini kama nchi ili tuweze kuutokomeza kabisa umasikini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Devota Likokola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu yoyote ile ambayo nchi inataka kuwa nayo lazima muwe na uwezo wa kuweza kui-*compare* na nchi nyingine, kama takwimu hiyo itakuwa haina maana katika *comparative analysis.* Kwa hivyo takwimu hiyo kuikusanya itakuwa haina faida yoyote. Kwa maana hiyo, hata ukiwapima Watanzania matajiri utalinganisha na matajiri wa nchi gani, wa Marekani?

Kwa hivyo itakuwa haina maana takwimu hiyo ndiyo kwa maana nchi nyingi hazikusanyi takwimu za matajiri, tunakusanya takwimu za umasikini ili tuweze kujua ni Watanzania wangapi ambao hawajitoshelezi na chakula.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Devota alitaka kujua kama nchi, tufanye nini? Ya kufanya yako mengi, lakini nataka nieleze machache tu.

Kwanza, tubadili mtazamo wetu, kwenye suala la kilimo. Tutoe nafasi ya Kilimo ili kiwe ni sekta moja katika kusaidia kukuza uchumi. Watanzania tukibadili *mind-set* yetu, badala ya kukichukulia kilimo ni cha chakula tu, tukichukulie kilimo ni kwa ajili ya biashara na kukuza uchumi hilo litaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, la pili ni mtazamo wetu kwenye elimu. Tuwekeze zaidi katika elimu, ambayo itakayoweza kuwasaidia Watanzania kujitegemea badala ya kusubiri kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala la uwekezaji katika viwanda. Tukiamua kwa makusudi tukakaribisha wageni kuwekeza katika viwanda na sisi wenyewe Watanzania tukaamua kuwekeza nguvu zetu katika viwanda, ni dhahiri kwamba, nchi yetu itaweza kuandokana na umasikini. Nataka niseme tunaweza na *Yes,* tunaweza. *(Makofi).*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, utekelezaji wa *MKUKUTA* awamu ya kwanza umekuwa ukisuasua kutokana na gharama kubwa ya utekelezaji wake ambao inakadiriwa kuwa ni zaidi ya bilioni 900 kwa mwaka, kilimo peke yake ni zaidi ya bilioni 300. Na kwa kuwa, awamu ya pili ya *MKUKUTA* inaanza Julai mwaka 2010 bila kutathmini yaliyojiri katika awamu ya kwanza.

Je, serikali haioni kuwa katika hali hii ya mtikisiko wa Dunia, tunachotegemea sasa kukiona ni *failure* ya awamu ya pili ya *MKUKUTA.*

**SPIKA:** Wewe ndio  mnaoitwa *Persimist.* Enhee, Mheshimiwa Naibu Waziri. Unayaona magumu tu mbele? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimwambie tu Mheshimiwa Salima, kwamba Serikali haiendi katika awamu ya pili ya *MKUKUTA* pasi na kufanya tathmini. Na tathmini tayari sasa hivi inaendelea na tunawashirikisha wadau wote. Kwa maana hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Salim, kwamba awamu ya pili ya *MKUKUTA* haitafeli kama awamu ya kwanza ya *MKUKUTA. (Makofi).*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, iliyosomwa wiki iliyopita hapa Bungeni, pamoja na mambo mengine alisema kwamba mkakati wa kupunguza umasikini, yaani *MKUKUTA* hapa nchini kasi yake hairidhishi hata kidogo.

Je, Mheshimiwa Waziri, ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba kasi ya umasikini hapa nchini inapungua kwa kasi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa kasi ya umasikini nchini, nataka niseme tu mambo mawili; kwanza Watanzania wote *we have to change our mind set.* Tuwe na mtazamo tofauti kidogo. Kama nilivyoeleza katika jibu la kwanza kwamba tukipe mtazamo mkubwa sana kilimo.

Lakini la pili, nataka niseme tu kwamba katika *MKUKUTA* wa pili tutashirikisha sekta zote mpaka sekta binafsi. Kwa maana hiyo tunamategemeo makubwa sana kasi ya kupungua kwa umasikini itaongezeka.

Na. 78

**Ubadhirifu Uliofanyika Kwenye Kampuni Mbalimbali**

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika hotuba ya Waziri Mkuu Kivuli kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI,* niliyotoa Bungeni Juni, 2007 pamoja na mambo mengine nilieleza juu ya ubadhirifu mkubwa uliofanywa kupitia kampuni ya *MEREMETA*, *Tangold*, Mwananchi na *Deep Green Finance Co.* Wenye jumla ya zaidi ya shilingi 215 bilioni:-

(a) Je, ni lini kampuni hizo zitafanyiwa ukaguzi wa kina, *Special Audit*, kama ilivyofanyika kwa akaunti ya *EPA* ili kubaini ubadhirifu huo uliohusisha uhamisho wa fedha kutoka Benki Kuu na vyombo vya umma kupitia *NBC Corporate Branch DSM* na *NedBank* ya Afrika ya Kusini?

(b) Je, ni sababu gani za msingi zilizofanya kuchukua muda mrefu kuanza ukaguzi wa kina hata pale tuhuma hizo zilizopigiwa kelele na jamii na hata kamati mbalimbali zilizoundwa kuchukua tuhuma hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kukumbusha Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 27 Juni, 2008 Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa maelezo kuhusu makampuni ya Meremeta, *Deep Green Finance* na *Tangold*, kama inavyonukuliwa na *Hansard.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelezo ambayo yalifafanua kuwa masuala ya makampuni haya yamejikita ndani ya Jeshi la Wananchi. Na kwa hiyo, yanahusu ulinzi na usalama wa nchi ninaomba Mheshimiwa Mbunge aridhike na maelezo hayo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Mwananchi Gold Company*, hii kampuni ilianzishwa kama kiwanda cha kusafisha dhahabu ghafi ambapo Benki Kuu ilichukua hisa zenye thamani ya 36% wakati 15% ya hisa katika kampuni hiyo zinamilikiwa na *National Development Co-Operation (NDC),* 20% ya hisa ziko mikononi mwa wawekezaji wa nje, *Chimera Company Ltd*, na 29% ya hisa zinamilikiwa na Mfuko wa Wadhamini, *Mwananchi Trust.* Kulingana na taarifa zilizoko kwa Msajili wa Makampuni, Taasisi zenye hisa katika Mfuko wa Wadhamini wa Kampuni ya Mwananchi ni pamoja na *Umoja Entertainment Ltd, Y.M. Investiments Ltd, VMB Holdings* na *CCM Trust.*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania iliwasilisha pendekezo la kujitoa kwenye umiliki wa kampuni hii katika kikao ya bodi ya kampuni ya *Mwananchi Gold* kilichofanyika tarehe 29 May, 2008 kwa sasa kampuni ya *Mwananchi Gold* imesimamisha shughuli zake.

Kufuatia hali halisi ya kampuni, Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni ya *Mwananchi Gold* ilikutana Disemba, 2008 na kuamua kuiomba Benki Kuu ianzishe taratibu za kuifilisi kampuni ya *Mwananchi Gold.* Mchakato wa ufilisi huo unaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kampuni ya *Mwananchi Gold* imewekwa kwenye ufislisi, Serikali inaona si vyema kufanya ukaguzi wa kina wa kampuni hii wakati ufilisi ukiendelea. Hata hivyo kwa kuwa ufilisi ni mchakato wa kisheria, tunatarajia serikali itapata taarifa kwa undani zaidi kutoka kwa Mfilisi.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nieleze masikitiko yangu kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, ambayo hayakujibu kabisa maswali yangu. Kwa yeyote aliyesoma ataona swali langu linaongelea makampuni mengi; Waziri anazungumzia mawili tu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza; Kwa kuwa, hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu Meremeta ilikuwa ya tarehe 27 June; na kwa kuwa, tunazungumzia tuhuma ya ubadhirifu wa bilioni 155 katika meremeta. Na kwa kuwa, Kamati ya Mheshimiwa…..

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa. Tulikaa katika Kamati, tukakubaliana mambo yote yanayohusu Jeshi letu la Wananchi kwamba hayawezi kuwa ni ya hadharani. Na Mheshimiwa Waziri Mkuu, akaitoa taarifa ndani ya Kamati ya Uongozi, tukiwa wote na ninadhani na wewe ulikuwepo. Kwa hiyo, siwezi kuruhusu swali lolote linalohusu Meremeta, uliza swali linalohusu Mwananchi. *(Makofi).*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakubali ila tu niseme kwamba mimi sikuwa nauliza kuhusu Jeshi, nauliza kuhusu wizi. Lakini niulize swali la pili linalohusu *Tangold, Deep Green, Mwananchi.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, haya makampuni nayo yana ubadhirifu wa jumla ya fedha zinazokaribia bilioni 120. Na kwa kuwa, makampuni yote katika nchi hii, hasa ya Serikali ambayo ni mali yetu sisi sote, yanatakiwa kwa mujibu wa sheria kukaguliwa hata kama yanakuwa kwenye ufilisi. Je, Serikali inasema nini inapoenda kinyume na Kamati ya Bomani, ambayo nayo iliagiza mwezi Oktoba, 2008, kwamba makampuni haya yakaguliwe?

Je, serikali inaenda kinyume na kuikana sasa Kamati ya Bomani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri

wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba Mheshimiwa alipotoa ufafanuzi ule alisema kwamba Meremeta na hizo kampuni nyingine zilizoambatana na Meremeta. Kwa hiyo *Tangold* na hizi nyingine unazotaja, ziko humo humo. Na ndio sababu tukatenganisha kati ya kampuni hizo na mwananchi. Sasa kuhusu Mwananchi, nimesema kwamba iko katika ufilisi. Nimesema kwamba Ufilisi ni mchakato wa kisheria na yule Mfilisi pamoja na kufuata sheria lakini moja ya mambo anayofanya ni kuingia kwa undani kutafuta mali iko wapi, madeni yako wapi na kutoa taarifa kwa wale ambao watakuwa wamemtuma. Kwa hiyo sio busara kwa serikali kuweka *a parallel audit system* ama *procedure* wakati mfilisi anapofanya kazi. Na mimi ninafikiri ni vyema tukasubiri, haraka ni ya nini? Halafu na wewe tafuta hoja nyingine? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante, ahsante, utulivu. Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu. Kwa kuzingati muda tunaendelea na Wizara ya afya na ustawi wa Jamii. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini. *(Kicheko).*

Naomba Utulivu waheshimiwa. *Order please.*

Na. 79

**Vituo Vinavyotoa Huduma Kwa Jamii Kusajiliwa**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mama Advella wa Kishuro, Kata ya Ngenge, amekuwa akilea watoto yatima na wazee kwa miaka mingi; na kwa kuwa, vituo vinavyotoa huduma kama hiyo husajiliwa, hutembelewa na kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo za ujenzi na usafiri na kwa kuwa suala hili limeshafikishwa Serikalini.

Je, kwanini mama Advella asitambulike na kusajiliwa kama kituo kinachotoa huduma hii muhimu kwa jamii?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni kusajili na kutoa leseni za kuendesha makao ya malezi ya watoto. Kazi hii hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Makao Na. 4 ya mwaka 1968. Kabla ya Makao kusajiliwa ni lazima mmiliki airidhishe Wizara kwamba anao uwezo wa kifedha na kirasilimali wa kumudu kutoa huduma kwa watoto watakaotunzwa na kulelewa kwa muda wote bila kutegemea msaada. Sharti lingine linalozingatiwa katika kusajili makao hayo ni kuhakikisha kuwa

wamiliki wa Makao hayo wanatoa huduma kwa kuzingatia viwango vya ubora kulingana na masharti yaliyowekwa na Sheria niliyoitaja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wa Wakala za Hiari kama vile, Mashirika ya Dini, Mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi katika kutoa huduma za malezi, matunzo na ulinzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi.

Kwa kutambua mchango huo, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutoa ruzuku kwa Wakala hizo ili ziweze kuboresha huduma wanazozitoa katika Makao wanayomiliki. Ruzuku inayotolewa huzingatia hali halisi ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mama Advella wa Kishuro, Kata ya Ngenge hayumo katika orodha ya Wizara ya watu wanaolea watoto yatima ingawa muuliza swali anatuarifu kuwa amekuwa akifanya hivyo kwa miaka mingi. Ili kuhalalisha shughuli anayofanya nashauri awasilishe maombi yake kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, ambaye atawasiliana na Wizara yangu kwa madhumuni ya kumpatia leseni iwapo atakuwa ametimiza masharti ya usajili wa Makao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wote wanaoendesha makao bila leseni, wawasiliane na Ofisi za Halmashauri katika maeneo yao ili wapate maelekezo sahihi ya usajili wa Makao hayo kutoka kwa Maafisa ustawi wa Jamii katika Halmashauri husika.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na kwamba Mama Advella wa Kishuro, anatambulika hajasajiliwa na Serikali, lakini amekuwa anafanya kazi hii kwa muda mrefu. Serikali itakuwa tayari kumpongeza na kumshukuru kwa kazi hii kubwa anayoifanya?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi hii ni muhimu na kazi anayoifanya Mama Advella ni ya kuisadia Serikali. Tayari mama huyu anaendelea kulea watoto na kutunza wazee. Serikali itakuwa tayari kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, aende akamtembelee ili aweze kumshauri na kuona kama anastahili kuajiriwa badala ya kumtaka tena yeye aende Muleba kwa kutoa gharama zake nyingine za kulea watoto katika safari za kutaka kuhangaika. Je, Serikali itasaidia suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Serikali inathamini sana wale wote ambao wanafanya huduma hizi za kuwalea watoto ambao wanaishi katika mazingira hatarishi. Lakini hata hivyo, sasa naomba

niseme akiwemo Mama Advella. Kwa hiyo nampongeza sana Mama Advella wa Kishuro kwa kazi nzuri sana anayoifanya na kweli hii inaonesha kwamba yeye amejitolea. Kwa hiyo pongezi hizi tunaomba kwa niaba ya Wizara ya afya na kwa niaba ya Serikali tunampongeza sana. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kumsaidia Mama Advella ili kuweza kupata usajili. Kama jibu langu la msingi lilivyosema, nimesema kwamba wanatakiwa Halmashauri waweze kuomba maombi ili Halmashauri iweze kuwasiliana na Wizara ya Afya. Lakini vile vile sasa ili kumsaidia Mama Advella na wale wengine wote ambao wanaendesha Makao ambao hawana leseni, basi napenda niagize halmashauri zote zilizoko katika nchi hii kwamba wahakikishe kwamba katika Halmashauri zao wanatembelea Makao yote ambayo watu wanatoa malezi kwa watoto na wazee ili wawapitie na kuweza kuhakikisha kwamba kama yana kidhi mahitaji waweze kuwapatia leseni.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nikumbushe kwamba jukumu la kulea watoto yatima na wazee sio jukumu la Mama Advella wala sio jukumu la Serikali. Ni sisi kama jamii tuhakikishe kwamba wazee na watoto wetu tunawatunza na pale tu inapobidi ndio wakae katika makambi.

Na. 80

**Vyandarua Vya Bure kwa Akina Mama Wanaojifungua**

**MHE. MARIA IBESHI HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hapa nchini watoto wengi wenye umri wa mwaka mmoja hadi mitano hufa kwa ugonjwa wa malaria:-

Je, serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kutoa chandarua cha bure chenye dawa ya kinga ya mbu kwa kila mama anayejifungua hospitali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba watoto wengi wenye umri wa chini ya miaka mitano hufa kwa malaria. Takwimu tulizo nazo zinaonyesha kuwa wastani wa watoto 60,000 hufa kwa malaria kila mwaka. Matumizi ya vyandarua vilivyotiwa viuatilifu ni afya ambayo imethibitika kupunguza vifo vinavyotokana na malaria kwa watoto na akina mama wajawazito kabla na baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi zaidi ya mitano Serikali yetu imekuwa inatekeleza Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo kwa madhumuni ya kuwasaidia wajawazito na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja kununua vyandarua kwa bei nafuu. Kupitia mpango huu mama mjamzito anatakiwa kulipia shilingi 500 ili kupata chandarua imara na ambacho kina dawa ya kudumu, *Long Lasting Insecticide Trated Net.* Thamani halisi ya chandarua aina hiyo ni kati ya shilingi 7,000 na shilingi 9,000 kutegemeana na ukubwa, hivyo Serikali imekuwa ikichangia kati ya shilingi 6,500 na shilingi 8,500. Aidha kwa sasa Wizara imeamua kutoa bila malipo vyandarua milioni 7.2 kwa watoto wote nchi nzima wenye umri chini ya miaka mitano, *Underfive Catch-Up Campaign.*

Zoezi hili tayari limetekelezwa katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Tanga, pamoja na Wilaya ya Mpanda ambapo hadi sasa jumla ya vyandarua 962,312 vimetolewa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Zoezi hili linaendelea Kanda ya Ziwa, ambapo shughuli ya uandikishaji inaendelea na vyandarua vitaanza kutolewa tarehe 10 Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara imepata ruzuku ya Dola milioni 113 za Kimarekani kupitia duru ya 8 ya Mfuko wa Dunia, *Global Fund Round 8.* Fedha hizo zitatumika kununua na kugawa bila malipo wastani wa vyandarua 2 kwa kila Kaya Tanzania Bara. Matayarisho yamekamilika na ugawaji huu unatarajia kuanza mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. MARIA IBESHI HEWA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba nimwulize swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kwamba tatizo lipo na kweli watoto wengi sana wanakufa. Na katika majibu ya Naibu Waziri, anasema vyandarua vipo na vinagawiwa; mamilioni ya fedha yapo na yananunua vyandarua vinagawiwa. Vyandarua hivyo vyote vitakwisha na akina mama wataendelea kujifungua.

Je, hilo taifa linalozaliwa hivyo wakati vyandarua vimekwisha, Serikali ina mpango gani endelevu ili nalo taifa hilo liweze kupata hiyo huduma kama ile wanayoipata hivi sasa wale wanao orodheshwa? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ninamwelewa swali lake yeye anaamini kwamba vyandarua hivi vitaisha na watoto bado wanaendelea kuzaliwa. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi; nimesema kwa sasa hivi kuna huu mpango wa *Under Fiver Catch-up Campaign* ambao kuna vyandarua milioni 7.2 vinaendelea kugawiwa. Lakini vilevile Wizara imepata ruzuku ya milioni 113 za Kimarekani kutoka *Global Fund,* ambayo 2009/2010 zitaanza kugawiwa. Lakini huu ni mpango endelevu Mheshimiwa siweze nikasema kwamba wale ambao watakuja kuzaliwa hawatakuja kupata vyandarua.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa, kwamba huu mpango ni endelevu. Tulianza na akina mama wajawazito, sasa tumekuja wa watoto wa *under five,* lakini sasa tunataka kila Kaya waweze kupata vyandarua ili waweze kuvitumia. Labda tu niseme naomba niombe kwamba hivi vyandarua vitakapokuwa vinapatikana tuhakikishe kwamba watoto na akina mama wajawazito wanavitumia badala ya akina baba kupewa vyandarua hivi au kutumika kwa matumizi mengine ili kuweza kuhakikisha kwamba malaria nchi hii inakuwa ni historia. *(Makofi).*

Na. 81

**Udhamini wa Serikali Katika Mikopo ya Ujenzi wa Vyuo**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imefanya kazi nzuri ya kudhamini mikopo ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Hombolo kutoka Mifuko ya Pensheni ili kujenga na kupanua vyuo hivyo:-

Je, ni lini sasa serikali itadhamini mikopo kwa vyuo vingine kama *MIST, DIT, CBE,* Dodoma na vinginevyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la wananfunzi wanaohitimu na kufaulu masomo ya Sekondari, Serikali iliamua kuongeza nafasi za wanaodahiliwa katika Vyuo Vikuu Vya Umma.

Pia ilianza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kutumia mikopo ya Mifuko ya Jamii ya *PSPF*, *NSSF* na *PPF.* Ambacho kitakuwa na uwezo wa kudahili wananfunzi zaidi ya 40,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kupanua Vyuo vya Elimu ya Juu ili viweze kudahili wanafunzi wengi zaidi.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwenye elimu kwa kuboresha na kujenga Vyuo vya Elimu ya Juu nchini kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwenye Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kuwa Serikali hukopa kulingana na uwezo wa Bajeti kulipa deni husika na pia uwezo wa nchi kuhimili ukuaji wa deni na madhara yake kwenye uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti na madhara ya kuwa na deni la ndani lisilohimilika, nashauri Wizara mama za Vyuo vya *CBE, DIT, CBE* zibainishe mahitaji yake ya fedha mapema na kuingiza kwenye mpango wa muda wa kati wa matumizi *(MTEF),* ya Wizara hizo ili vyuo viweze kujengwa kwa awamu kupitia Bajeti zao.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kama kuna kitu ambacho Serikali ya Awamu ya Nne imefanya na kitaweka alama kwenye historia ya nchi hii, ni Chuo Kikuu cha Dodoma. Na kwa kuwa, kudhamini mikopo hiyo kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, hakukutokana na mipango ya Wizara bali utashi wa Kisiasa wa Uongozi wa Juu. Na kwa kuwa, ajali ambazo tumeziona miaka ya karibuni za majengo yanayojengwa yakaanguka yameonesha dhahiri kwamba kuna upungufu wa kada ya kati katika fani hiyo.

(a) Je, Serikali itadhamini lini mkopo kwa ajili ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya ili kiweze kupanua miundombinu yake na kufundisha kada hiyo? *(Makofi).*

(b) Kwa kuwa, Chuo Kikuu cha Mzumbe, kina tawi mjini Mbeya ambalo mpaka sasa limekidhi matakwa yote ya kuwa Chuo Kikuu Kishiriki kamili katika miundombinu na katika utawala.

Je, tawi hilo la Chuo Kikuu cha Mzumbe cha Mbeya. Je, tawi hilo la Chuo Kikuu cha Mbeya, ni lini Serikali italifanya kuwa Chuo Kikuu Kishiriki kamili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba arejee tena jibu langu la msingi kwamba masuala ya mikopo na udhamini wa Serikali, unaiingizia Serikali deni kubwa sana ambalo halivumuliki. Kwahiyo tunashauri badala ya kuendelea kudhaminiwa na Serikali ili kukopa katika mashirika haya ya fedha. Kwa kweli Wizara mama ya hiki chuo cha *MIST* ambacho ni *Mbeya Institute of Science and Technology,* waendelee kutumia mipango yao ya kawaida ambayo inatokana na Bajeti za Serikali kupanua chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa chuo Kikuu cha Mzumbe, tawi lililoko Mbeya ni tawi ambalo chuo kile sio kishiriki, ni *campus*. Kwa hiyo suala la kukifanya kiwe Chuo Kikuu Kishiriki itategemea na hali halisi ya hali ya upanuzi wa chuo na mipango ambayo imewekwa. Kwa hiyo nafikiri tusubiri Bajeti yetu itakapokuwa inasomwa hapo tutakuwa tunaelezea mambo zaidi kuhusiana na upanuzi wa vyuo vyetu ikiwemo Chuo Kikuu Cha Mzumbe.

Na. 82

**Mpango Wa Kuanzisha Vyuo Vya VETA Kila Wilaya**

**MHE. IDDI M. AZZAN (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kuanzisha Vyuo vya *VETA* angalau chuo kimoja kila Wilaya kwa lengo la kuongeza nafasi za masomo ya ufundi stadi:-

(a) Je, ni vyuo vingapi vimejengwa mpaka sasa kuanzia mwaka 2005 hadi 2008?

(b) Je, ni Wilaya zipi zilizojengwa Vyuo vya *VETA* kwa kipindi hicho?

(c) Je, wilaya ya Temeke imo katika mpango huo wa kujengwa Chuo cha *VETA?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005 hadi 2008, hakuna Chuo ambacho kimeshajengwa.

Hata hivyo maandalizi yamefanywa ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa stadi katika wilaya 28, kuandaa michoro ya vyuo, kubainisha maeneo ya ujenzi na kuandaa andiko la mradi na kuwasilisha kwa wafadhili kwa ajili ya kuomba fedha. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, hatua za awali za ujenzi zimeanza katika Wilaya ya Makete kwa kuwa wilaya hiyo ina idadi kubwa ya vijana yatima ambao wakipatiwa Mafunzo ya Ufundi Stadi wataweza kujitegemea.

(c) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Temeke haipo katika mpango huu kwa vile katika Wilaya hiyo tayari kuna Chuo cha *VETA* eneo la Chang'ombe.

Aidha, Wilaya hii ipo katika mpango wa kujengewa chuo cha Teknolojia eneo la Kipawa ambapo Mkandarasi ameshakabidhiwa eneo na wakati wowote shughuli za ujenzi zitaanza.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa vyuo vya *VETA* Wilaya ni kwa ajili ya Wilaya 28 tu ambazo hazina chuo chochote cha ufundi cha Serikali au cha binafsi. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa chuo cha *VETA* mkoa wa Lindi imekuwa ni Hadithi za Alfu Ulela Ulela. Je, leo Serikali itatamka kwamba kabla ya kuendelea kujenga kwenye wilaya waangalie kwanza ujenzi wa chuo cha mkoa wa Lindi, Manyara, Kibaha na Pwani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, sio mara ya kwanza swali hilo linaulizwa hapa Bungeni naomba tu nirudie majibu kwamba vyuo hivi vya mikoa mitatu vitajengwa *funding* yake au pesa yake ni tofauti na pesa vyuo hivi vya wilaya. Na maandalizi yameshafanywa, mkandarasi ameshaandaliwa na mhusika Serikali ya Korea iko tayari kuanza ujenzi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge katika mikoa hii wavute subira, vyuo hivi kwa kweli si udanganyifu vitajengwa Mheshimiwa Mudhihir.

**SPIKA:** Ahsante kwa kuwa vitajengwa basi nadhani tuendelee, tunaendelea kidogo kwa sababu mtagundua tulikuwa na matangazo mengi ya kuwasilisha hati mezani yalichukua kama dakika kumi hivi, basi hiyo itatupa fursa ya kumalizia maswali mawili la Katiba na Sheria linaulizwa na Mheshimiwa Fred Mpendazoe wa Kishapu.

Na. 83

**Hakimu wa Wilaya kupelekwa Kishapu**

**MHE. FRED TUNGU MPENDAZOE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kishapu haina Mahakama ya Wilaya na hivyo kesi za Wilaya kupelekwa Shinyanga kusababisha usumbufu kwa wananchi:-

Je, Serikali kwa nini isiweke utaratibu wa kupeleka Hakimu wa Wilaya angalau mara mbili kwa wiki kwa kutumia jengo la mahakama ya mwanzo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa madhumuni ya kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi, huduma ya utoaji haki katika ngazi ya wilaya kuna haja ya kuweka utaratibu wa mahakama ya wilaya Shinyanga kuendesha vikao vyake wilayani Kishapu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato mzima wa Wilaya ya Kishapu kuwa na Mahakama yake ya wilaya unaendelea na haujakamilika kwa sasa Serikali kupitia mahakama inaangalia uwezekano huo aliopendekeza Mheshimiwa Mbunge ili utumike na pindi utaratibu utakapokamilika wananchi wa wilaya ya Kishapu watafahamishwa ipasavyo.

**MHE. FRED TUNGU MPENDAZOE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, kwanza naomba niishukuru Serikali kwa dhati kabisa nakutoka kwenye sakafu ya moyo wangu kwa kuweza kusikia kilio cha wananchi wa Kishapu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakipata shida ya kwenda mahakama ya mkoani Shinyanga.

Swali ndogo ni kwamba je, Waziri atakubaliana na ushauri wangu kwamba wakati Serikali inaendelea na mchakato ambao utawezesha vikao vya mahakama ngazi ya Wilaya kufanyika wilaya Kishapu, kwamba kwa sasa Serikali itenge fedha zitakazowezesha jengo ya la mahakama ya Mwanzo ambapo vikao vya mahakama ya wilaya vitafanyika iweze kufanyiwa ukarabati mzuri ili majengo hayo yawe katika hali nzuri kuliko ilivyo sasa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba Mahakama sasa iangalie uwezekano wa kutenga pesa za kwenda kukarabati mahakama ya mwanzo ya Kishapu ili iweze kutoa huduma kama Mahakama ya Wilaya, hadi hapo mahakama ya Wilaya itakapojengwa. Nakubaliana naye na tutaangalia uwezekano huo tunaomba mahakama itenge pesa kwa ajili hiyo.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Lakini niipongeze Serikali kwa kuanzisha mahakama wilayani Bukombe. Kwa kuwa Wilayani Bukombe, tumeanzisha mahakama ya Wilaya, na Mheshimiwa Hakimu mahali anapoishi kwa kweli hapana heshima ya Mheshimiwa Hakimu kuishi pale, lakini pia Mheshimiwa Hakimu hana gari.

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na makazi ya Mheshimiwa Hakimu ambaye anayetenda haki katika wilaya pamoja na gari asiwe anatembea kwa miguu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nilitembelea mahakama ya Bukombe, nilikutana na huyo hakimu anayemsema, nakubaliana naye ni kweli kwamba sehemu anayoishi labda hairidhishi sana. Lakini nafikiri Mheshimiwa Mbunge wakishirikiana na uongozi wa Wilaya pale wanaweza wakajaribu kutafuta nyumba itakayomfaa hakimu huyo.

Kuhusu suala usafiri ni wiki kama tatu hivi nilikabidhi mahakama magari 30 kutoka kwenye mradi wa *legal sector reform program* na ni matumaini yangu kwamba

katika gari hizo 30 basi wanaweza wilaya ya Bukombe nao wakatengewa moja katika magari hayo. (*Makofi*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa swali la msingi linazungumzia kuhusu uhaba wa Mahakama na kwa kuwa wilaya ya Ruhangwa, haina mahakama ya wilaya na wananchi wake wanalazimika kwenda kwenye mahakama ya mkoa wa Lindi ambako ni mbali sana kuliko mahali waliko.

Na kwa kuwa Nachingwea kuna mahakama ya wilaya, kwanini isiwe hawa watu wanaohitaji kutumia mahakama ya wilaya wasiende katika wilaya ya Nachingwea badala ya kwenda mkoa wa Lindi ambako ni mbali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wilaya ya Ruhangwa bado haina mahakama ya wilaya, lakini ni kweli pia watuhumiwa wanaokamatwa wilaya ya Ruhangwa wanaweka katika jela ya wilaya ya Nachingwea na ziko kesi ambazo zinasikilizwa za watuhumiwa wa wilaya ya Ruhangwa zinasikilizwa Nachingwea. Ingawaje ni kweli pia zipo zingine zinazokwenda Lindi.

Lakini nafikiri ufumbuzi wa jambo hili ni kujenga mahakama wilaya ya Ruhangwa ambayo iko katika utaratibu wa chini ya Wizara yangu kujenga mahakama hiyo katika wilaya ya Ruhangwa hivi karibuni.

Na 84

**Uharamia wa Kuteka Nyara Meli**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwenye pembe ya Afrika kumeibuka uharamia wa kuteka nyara meli zinazofanya safari za kimataifa; na kwa kuwa, nchi yetu haiko mbali ki-jiografia na eneo hilo:-

Je, Serikali imejipanga vipi kupambana na maharamia hao pindi wakipenya kwenye fukwe zetu kwa malengo ya utekaji nyara wa meli?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia Jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ) hususani kamandi ya *Navy*, Kamandi ya Anga na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, limeweza kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo la bahari kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kufanya doria katika eneo la bahari lililo chini ya miliki ya nchi yaani *Territorial Water.*

(ii) Kusindikiza meli zinazohitaji huduma hiyo katika eneo la bahari lililo chini ya miliki ya Tanzania.

(iii) Kushirikiana na majeshi mengine, katika kuimarisha mapambano dhidi ya uharamia katika eneo hilo.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, lakini nina swali dogo la nyongeza, ikiwa vikosi vya wana maji wa mataifa makubwa duniani, vinatolewa jasho kweli kweli na maharamia hawa ambao wanafanya mashambulizi yao kwa kushtukiza.

Je, sisi ambao inaonekana hata hatujajipanga vizuri kulinda uvuvi haramu katika bahari yetu kuu, ni kweli tumejiweka sawasawa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, chanzo au ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharamia kama tunavyoelewa ni kuhakikisha kwamba nchi ya Somalia inapata Serikali na sheria zinatumika katika nchi hii. Hivi sasa kuna masuala kadhaa yanayofanyika ili kuweza hatimaye kuhakikisha kwamba Serikali madhubuti ya Somalia inapatikana na hivyo kuleta utaratibu wa kisheria unaofaa ili kuzuia matatizo ya uharamia kutoka nchini Somalia.

Lakini hata hivyo kama nilivyosema kwamba ni kweli kwamba kuna mataifa mengi sasa hivi ambayo yana manuari zao katika eneo hili husika na kama nilivyosema wanashirikiana na sisi katika sehemu ya tatu nilisema kwamba wanashirikiana na sisi kuhakikisha kwamba wanatusaidia na sisi tunasaidiana nao kutoa ulinzi madhubuti pale ambapo maharamia wale wataelekea upande wa Tanzania. Hivi sasa napenda kusema kwamba hawajafanya hivyo bado, bado tatizo liko katika *Gulf of Eden* kuliko huku Tanzania, bado hali ni shwari. Uwezo wetu sisi ni kulinda maji yetu hilo ndilo tunalifanya endapo itatokea kwamba tutahitaji kwenda nje ya hapo, basi nchi wanachama wa Ulaya pamoja na Marekani wamekuwa tayari kutoa msaada huo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha maswali yamekwisha, sasa ni wakati wa matangazo. Tunao wageni wengi kidogo lakini wengine nitawatamka kwa makundi tu.

Kwanza ni Mheshimiwa Mama yetu Tunu Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante sana Mama, tunafarijika mara kwa mara unapokuja kufuatilia shughuli hapa.

Anayefuata ni Katibu Mkuu Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bwana Peniel Lyimo, Katibu Mkuu ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI Bi. Maimuna Tarish, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Bwana Fanuel Mbonde, Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa, Mheshimiwa John Tendwa, Mkurugenzi Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndugu Rajab Kiravu, na Afisa Usalama wa Serikali Bwana Majid Kikula. (*Makofi*)

Leo Waheshimiwa Wabunge tunafurahi Wakuu wetu wote wa Mikoa ya Tanzania Bara wako hapa na kwa heshima nitaomba niwatambulishe mmoja mmoja, Major General Mstaafu Said Kalembo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Col. Enosi Elisa Mfuru, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Lt. Col. Issa Salehe Machibya, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Sasa hawa ni wenzetu sijui wamekaa wapi lakini tutawaona Dr. Christina Ishengoma, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Mheshimiwa William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Hayupo, inawezekana amekwenda Mbagala. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Monica Mbega, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Hajat Amina Mrisho Said, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Mohamed Abdul Aziz, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Abdallah Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Abbas Hussen Kandoro, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Isidori Shirima, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Abeid Mwinyimsa, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Jonn Livingstone Mwakipesile, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mheshimiwa Sadik M. Sadik, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Col. Anatory Albin Tarimo, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Daniel Ole-Njolai, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Parseko Vincent Kone, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mheshimiwa Col. Joseph Simbakalia, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mheshimiwa Brig. Gen. Yohana Daudi Balele, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, tunawakushukuru sana mnapokuwa hapa na kuweza kusikiliza mjadala kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu, kwa sababu ninyi ndiyo wasimamizi wakuu wa shughuli za Serikali katika Mikoa yetu yote, karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa wakuu wa taasisi zilizoko chini ya ofisi ya Waziri Mkuu Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI, Dr. Fatuma Mrisho, Mkurugenzi Mkuu wa *CDA* Bwana Kitila, Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Uwekezaji Bwana Emmanuel Ole-Naiko, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, *LPF* Bwana Sanga na Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Biashara, Bwana Mrutu, Katibu wa Bodi ya Mfuko wa Serikali za Mitaa Bwana Kabisama, Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Col. Mstaafu Swai, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania Bwana Tido Mhando. (*Makofi*)

Naomba sasa Wakuu wa Idara na Vitengo Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI wasimame tu ili Wabunge waweze kuwaona. Inafurahisha kuona kwamba ile jinsia inayokandamizwa kidogo inachomoza hapa katika Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Sasa ni Wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, ambao ni Bwana Ramadhan Sudi, kada wa CCM Magomeni. (*Makofi*)

Samahani Waheshimiwa kuna orodha ya Makatibu Tawala, naomba kwa ujumla wao wote 21 waweze kusimama. Makatibu Tawala wote wa mikoa tafadhali. Ahsante sana karibuni sana watendaji wakuu ndani ya Mikoa, tunashukuru sana ujio wenu hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa wageni wa Mheshimiwa Abdul Karim Shaha, ni Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Mheshimiwa Hadija Salum, naomba asimame pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Lucy Kalinjuma, Afisa Mipango na wageni wote wa kutoka Mafia tunaomba tafadhli wasimame. *(Makofi)*

Kwa kweli mambo yanabadilika, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ni Mwanamke. Hongera sana mama Hadija Salum. (*Makofi*)

Washiriki sita wa programu ya Maisha Plus, ambao ni Upendo Peneza, Maulid Wadi, Steven Sandu, Modesta Peter, Moshi Maona, na Efrasia Manji, yule mshindi ni yupi sijui, Abdul hayupo, siku nyingine mtuletee Abdul bwana tuweze kumwona. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo yanayohusu wageni, matangazo ya kazi zetu, Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Maliasili na Mazingira mkutane leo saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya *LAAC* mkutane leo saa saba mchana katika ukumbi namba 231 gorofa ya pili jengo la utawala. Huu ndiyo mwisho wa mtangazo na sasa namwita Katibu, kwa shughuli zinazofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda tuelewane kuhusu Kanuni, kanuni ya 99 kifungu kidogo cha (6) inasema ifuatavyo, isipokuwa kwa hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu muda wa Waziri anayewasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yake utakuwa ni dakika zisizozidi 60. Tafsiri yake hii ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza akaongea kwa dakika 60, 120, 180, mchana kutwa. Kwa hiyo, naacha kwa busara yake tu yeye hakupangiwa muda. *(Kicheko/Makofi)*

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2009/2010 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2008/2009 na mwelekeo wa kazi kwa mwaka 2009/2010. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya Matumizi ya fedha O fisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, Marehemu Richard Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Busanda, na Mbunge wa Zamani wa jimbo la Biharamulo na Marehemu Pharis Kabuye. Vilevile katika kipindi hiki kumetokea matukio mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali za wananchi wengi. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote walipatwa na misiba hii na maafa mbalimbali, tunamwomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka majeruhi wote na aziweke roho za marehemu mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wamepata fursa ya kujadili taarifa kuhusu hali ya uchumi wa taifa katika mwaka 2008/2009 na mpango wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010. Nitumie nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mustafa Mkulo Mbunge, Waziri wetu wa Fedha na Uchumi kwa hotuba nzuri na ufafanuzi fasaha wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri waliyoitoa wakati wa mjadala wa hotuba hizo na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali. Serikali itazingatia ushauri uliotolewa katika utekelezaji wa mpango wa Bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge Tukufu kwa Michango na ushauri waliotoa wakati wa kupitia makadirio ya matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa mchango wao mkubwa wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya fedha ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kuboresha Makadirio ya Bajeti ya ofisi hizi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepitisha Bajeti ya Serikali ambayo ndiyo itatuongoza kuelekea mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama cha mapinduzi ya mwaka 2005. Katika ilani hiyo chama kiliahidi mambo mbalimbali ambayo imezingatiwa katika bajeti hii. Vilevile Bajeti hii imezingatia yaliyomo katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini, yaani MKUKUTA. Dira ya taifa ya maendeleo 2025 na malengo ya milenia. (*Makofi*)

Serikali katika ngazi zote itaendelea kutekeleza kwa makini ahadi zilizoahidiwa kwa kuimarisha usimamizi na matumizi mazuri ya Bajeti ya Serikali iliyopitishwa.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayotekeleza demokrasia ya vyama vingi ili kudumisha demokrasia kumekuwepo na maboresho mbalimbali yanayofanyika kila mara kabla baada ya uchaguzi mkuu. Kwa mfano kabla ya uchaguzi mkuu wa vyama vingi uliyofanyika mwaka 2005 kulianzishwa daftari la kudumu la wapiga kura na kutumika wakati wa uchaguzi huo. Maboresho hayo pia yalihusu marekebisho ya sheria ya uchaguzi namba 1 ya mwaka 1985 na namba 4 ya mwaka 1979. *(Makofi)*

Masuala mengine yanayodumisha demokrasia ya nchi yetu ni kukubalika kwa maadili ya uchaguzi kuimarika na mahusiano baina ya Tume ya uchaguzi na wadau, vyama vyote vya siasa kupewa fursa sawa ya kunadi na kushindanisha sera za kwa wananchi, kuboresha kwa mchakato wa kupiga na kuhesabu kura pamoja na kutangaza matokeo.

Mheshimiwa Spika, ofisi ya msajili wa vyama vya siasa imeendelea na majukumu yake ya kusajili vyama kuratibu shughuli za vyama vya siasa na kukuza demokrasia ya vyama vingi hapa nchini. Hadi sasa idadi ya vyama vya usajili wa kudumu hapa nchini ni kumi na saba. Katika mwaka 2008/2009 vyama vitatu vya *Peoples Democratic Movement (PDM), Democratic National Congress* (*DNC*) na *Alliance for Tanzania Formers Party (ATFP*) vimepatiwa usajiri wa muda. Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa imeendelea kutoa elimu kwa umma ili kudumisha na kuendeleza mfumo wa demokrasia ya vyama vingi nchini na kufungua ofisi ya Kanda Dodoma. Ofisi hiyo itahudumia mikoa ya Dodoma, Iringa, Singida na Tabora. Aidha, Bunge lilipitisha marekebisho ya sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya mwaka 1992 ili kutoa fursa sawa ya kukuza na kuendeleza Demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 ofisi ya msajili wa vyama vya siasa itaandaa kanuni za sheria zitakazoelekeza jinsi marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa yatakavyotekelezwa. Vilevile, itafungua ofisi ya kanda ya Mwanza itakayohudumia mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kulifanyika chaguzi ndogo tatu za Wabunge katika majimbo ya Tarime, Mbeya Vijijini na Busanda, vilevile zilifanyika chaguzi ndogo za madiwani katika kata 45. Nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi waote na vyama vya siasa viliyvoshiriki katika chaguzi hizo ambazo zilifanyika kwa amani na utulivu. Aidha, nawapongeza wale wote walioshinda katika chaguzi hizo kipekee napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge, kwa kuchaguliwa Mbunge wa Jimbo la Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Busanda. Wote nawatakia mafanikioa katika kuwatumikia wananchi wa majimbo yao na vyama vyao katika muda uliobaki kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Viongozi wa ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa utafanyika mwezi Oktoba, 2009. Maandalizi muhimu ya kufanikisha uchaguzi huo yanaendelea ikiwemo kuandaa Orodha ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa kwa ajili ya Uchaguzi huo.

Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Kisiasa kuendelea kuwahamasisha Wananchi watambue umuhimu wa Uchaguzi kama nguzo muhimu ya kuimarisha Utawala Bora na Demokrasia Nchini, na wawe tayari kushiriki kikamilifu katika kuwachagua Viongozi wanaowataka kwa hiari yao wenyewe. Aidha, Vyama vya

Siasa na Wanachama wao wanahimizwa kufanya shughuli zao za Siasa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu ili kudumisha Amani na Utulivu uliopo Nchini.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010. Serikali kupitia Tume ya Uchaguzi imekamilisha Awamu ya Kwanza ya Uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hatua hii ni sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, inakusudia kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya Mwaka 1985 na Sheria Na. 4 ya mwaka 1979. Mapendekezo hayo ni pamoja na Tume kupewa Mamlaka ya kuandikisha Wapiga Kura wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa na Kipindi Maalum cha kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura walau mara mbili kati ya chaguzi na kubadilisha kipindi cha kufanya uteuzi wa mgombea endapo Mgombea Urais au Makamu atafariki.

Mapendekezo mengine ni kuondoa Vifungu vya Sheria vinavyoruhusu takrima, muda wa kufungua Kesi za Kupinga Matokeo kuongezwa, kuwekwa kikomo cha mgombea kujitoa katika Uchaguzi na Tume kupewa Mamlaka ya kufanya Chaguzi Ndogo za Madiwani walau mara mbili kwa mwaka badala ya kila wakati wa ukomo wa muda wa kusikiliza Kesi za Madiwani katika Mahakama. Pia, Tume ya Uchaguzi itaandaa vigezo na utaratibu utakaotumika kugawa Majimbo ya Uchaguzi. Nawasihi Wananchi kushirikiana na Tume ya Uchaguzi katika zoezi la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili wasikose haki yao ya msingi ya kuwachagua Viongozi wao ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Muungano. Muungano wetu unaendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, bado zipo kero chache ambazo pande zote mbili zinaendelea kuzifanyia kazi. Ili kuhakikisha kwamba kasi ya kushughulikia kero hizo inaongezeka, Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayojadili na kutoa ufumbuzi wa kero mbalimbali za Muungano imeandaa ratiba maalum kwa lengo la kuharakisha mchakato wa kutatua kero hizo.

Mheshimiwa Spika, tangu mwezi Februari, 2008 Mheshimiwa Makamu wa Rais alipoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Vikao vya Pamoja vya kushughulikia Kero za Muungano hadi kufikia mwezi Mei 2009, jumla ya Vikao Saba vimeshafanyika katika ngazi za Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Pamoja yenye Wajumbe kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mazungumzo katika Vikao vya kutatua maeneo yenye Kero za Muungano yanakwenda vizuri ambapo baadhi ya maeneo hayo yamemalizika baada ya maamuzi yenye muafaka wa pamoja kutolewa. Maeneo hayo yanahusu utekelezaji wa:-

(i) Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar;

(ii) Sheria ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu;

(iii) Sheria ya Biashara ya Meli katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais, kwa kuongoza kwa makini Vikao vya pamoja vya kushughulikia Kero za Muungano hadi kupata mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, Serikali imechukua hatua za makusudi kuelimisha umma kuhusu masuala ya Muungano kupitia vipindi vya Redio, Luninga na Vipeperushi. Aidha, Miradi ya pamoja ya kijamii na kiuchumi kama vile *TASAF*, *PADEP* na *SELF* inaendelea kutekelezwa katika pande zote mbili. Katika mwaka 2009/2010, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu Vikao vya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kudumisha Muungano wetu. Aidha, itaendelea na jukumu la kuimarisha ushirikiano kati ya pande mbili za Muungano kwa masuala yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Bunge. Katika mwaka 2008/2009, Bunge lilitekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Ibara 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge lilifanya Mikutano minne kama ilivyopangwa ambapo jumla ya Maswali 1,028 yaliulizwa na kujibiwa na Serikali. Aidha, Waziri Mkuu aliulizwa jumla ya maswali ya msingi 95 katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo.

Bunge pia, lilipitisha Miswada 24 na kuridhia Maazimio 10. Vilevile, Bunge lilizindua rasmi Mpango Mkakati wa Bunge wa miaka mitano kuanzia mwaka 2009 hadi 2013. Malengo Makuu ya Mpango Mkakati huo ni kuimarisha utendaji na uwajibikaji, kuboresha huduma itolewayo kwa Waheshimiwa Wabunge na matumizi ya TEKNOHAMA. Aidha, unalenga kutoa mafunzo kwa Watumishi na Wabunge ili kuwaongezea uwezo wa kuhudumia Wananchi vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Bunge letu lilishiriki Mikutano mbalimbali ya Kibunge katika Kanda na ile ya Kimataifa. Miongoni mwa Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola uliofanyika Malaysia tarehe 1 - 10 Agosti, 2008. Katika Mkutano huo, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samwel Sitta (Mb.), alichaguliwa kuwa Rais wa Taasisi ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

Aidha, mwezi Mei 2009, Bunge letu lilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Chama cha Wabunge wa Kamati za Hesabu za Serikali kwa Nchi za Mashariki mwa Afrika *(Eastern Africa Association of Public Accounts Committes).* Mkutano huo ulijadili na kubadilishana uzoefu kuhusu uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge katika kufuatilia Hesabu za Serikali. Nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioshiriki na kutuwakilisha vizuri katika Mikutano hiyo. Nampongeza Mheshimiwa Spika kwa nafasi hiyo aliyopewa ambayo imetuletea heshima katika Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Bunge litaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi na kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Bunge. Aidha, Bunge letu litakuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola utakaofanyika mwezi Septemba, 2009 Jijini Arusha.

Nawasihi tutumie fursa hiyo kujifunza na kubadilishana uzoefu na wenzetu kuhusu Kauli Mbiu ya Mkutano huo ambayo ni “Kukabiliana na Changamoto Zinazoikabili Dunia”. Aidha, hii ni fursa nzuri ya kuitangaza Nchi yetu hasa katika Sekta ya Utalii na Biashara.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa uchumi. Serikali imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 katika eneo la kusimamia Uchumi Jumla. Takwimu zinaonyesha kwamba Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2007. Hata hivyo, Uchumi umeendelea kukabiliwa na Mfumuko wa Bei uliotokana hasa na athari za kupanda kwa bei za bidhaa katika Soko la Dunia na upungufu wa chakula. Hali hii ilisababisha Mfumuko wa Bei kufikia asilimia 13.5 mwezi Desemba 2008. Kufuatia kushuka kwa bei ya bidhaa, kama vile vyakula na mafuta, Mfumuko wa Bei umeshuka na kufika asilimia 12.0 mwezi Aprili 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla ili kuleta hali ya utulivu na ukuaji mzuri wa Uchumi Nchini. Wito wangu ni kwamba, sote tufanye kazi kwa bidii kujenga Uchumi imara, wa kisasa na endelevu ili tuweze kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo ni kuwa Nchi ya Pato la Kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, ili kuutoa Uchumi wetu kutoka kwenye Uchumi uliyo nyuma na tegemezi na kuuingiza kwenye Uchumi imara, wa kisasa na endelevu tunahitaji kufanya Mapinduzi katika Sekta ya Kilimo na Viwanda. Mapinduzi haya yataongeza uzalishaji na tija na hivyo kuongeza ukuaji wa Uchumi. Uzalishaji wa mazao ya Kilimo ukiongezeka, mavuno yataongezeka na hivyo ongezeko hilo litawawezesha Wakulima kunufaika kupata kipato kutokana na kuuza mazao mengi zaidi nje.

Mheshimiwa Spika, hii pia, inavutia Wawekezaji kujenga Viwanda vya Usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za Viwandani kutokana na mazao ya kilimo. Tukifanya mapinduzi hayo, tutakuwa tumetekeleza ahadi yetu ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania. Hivyo, Viongozi na Watendaji wa Serikali wanao wajibu mkubwa wa kusimamia mapinduzi haya ili kukuza Uchumi kwa kiwango kikubwa na Kuutokomeza Umasikini.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoelezea Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake ya tarehe 10 Juni, 2009 mjini Dodoma, Dunia inakabiliwa na Msukosuko wa Masoko ya

Fedha ulioanzia huko Marekani na Nchi za Ulaya, Asia na kuenea sehemu nyingine Duniani. Msukosuko huu umesababisha Uchumi wa Dunia kuporomoka. Athari kubwa ya Msukosuko huo kwa Nchi Zinazoendelea inatarajiwa kujitokeza zaidi katika mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, athari za Msukosuko huo kwa Tanzania zinaweza kutazamwa katika Sekta ya Fedha na Uchumi wa Nchi. Kwa upande wa Sekta ya Fedha, Soko letu la fedha halitegemewi kuathirika sana kwa sababu ya kuwa na kiwango kidogo cha muunganiko na Masoko ya Fedha Duniani. Athari za kiuchumi ni pamoja na ukuaji mdogo wa Uchumi, kushuka kwa bei za mazao na bidhaa tunazozalisha Viwandani, kushuka kwa mapato kutokana na utalii na kupungua kwa uwekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali imeandaa Mpango wa Kunusuru Uchumi wa Tanzania na Athari za Msukosuko wa Fedha na Uchumi Duniani. Napenda kusisitiza kuwa, ni vyema tuhakikishe kuwa kuna nidhamu katika matumizi ya Serikali kutokana na hofu ya kupungua misaada kutoka nje. Vilevile, tuongeze juhudi katika kukusanya mapato ya ndani na kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuendeleza uwekezaji kwenye maeneo yatakayosaidia ukuaji wa Uchumi.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa sekta binafsi na uwekezaji. Uwekezaji na Maendeleo ya Sekta Binafsi, Serikali inatambua nafasi ya kimkakati ya Sekta Binafsi katika kukuza Uchumi na kuleta maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha Sekta Binafsi. Ili kutekeleza azma hiyo, katika mwaka 2008/2009, Serikali ilihamishia Ofisi ya Waziri Mkuu jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia masuala yote yanayohusu Maendeleo ya Sekta Binafsi na Uwekezaji ili iweze kupata msukumo unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hii, Ofisi yangu imesambaza Taarifa ya Hali ya Kufanya Biashara Nchini *(Report on Doing Business 2009)* kwa Watendaji Wakuu wote katika Wizara, Mikoa na Halmashauri. Taarifa hiyo ambayo imeainisha maeneo kumi yanayokwamisha Wawekezaji na Wafanyabiashara hapa Nchini, ilisambazwa kwa Watendaji Wakuu ili wachukue hatua zinazostahili kuondoa vikwazo hivyo. Nawaagiza Watendaji Wakuu wote kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji kuhusu hatua zinazochukuliwa kuondoa vikwazo hivyo Ofisi ya Waziri Mkuu kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA). Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania - MKUMBITA *(Business Environment Strengthening Programme - BEST).* Lengo la Mpango huu ni kupunguza gharama za kuanzisha na kuendesha Biashara kwa kuondoa vikwazo vya Sera, Sheria pamoja na udhibiti katika Sekta mbalimbali. Ili kuondoa vikwazo hivyo, MKUMBITA umejikita katika maeneo manne ambayo ni Usajili wa Miliki ya Ardhi, Maboresho ya

Sheria na Soko la Ajira, Ufumbuzi wa Migogoro ya Kibiashara na Usajili, Udhibiti na Ufilisi wa Biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, MKUMBITA umewezesha maandalizi ya utoaji Hati Miliki za Kimila kwa Vijiji na kuendeleza Makazi yaliyojengwa kiholela katika Jiji la Mwanza na Dar es Salaam. Mchakato wa kutoa Hati Miliki katika Wilaya za Babati na Bariadi umeanza mwezi Mei, 2009.

Aidha, Mpango umewezesha kuanzishwa kwa Mahakama ya Biashara, Mkoani Mwanza ambayo imezinduliwa na kuanza kazi na sasa inaendelea kusikiliza kesi zinazohusu migogoro ya biashara. Vilevile, Mpango wa Utekelezaji wa Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Mahakama umeandaliwa na umeanza kutekelezwa na Ripoti ya awali ya marekebisho ya Sheria zinazohusu Mfumo wa Haki na Madai imekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kukuza Sekta Binafsi na kuvutia Uwekezaji Nchini. Aidha, itaendelea na maboresho yenye lengo la kupunguza gharama za kufanya biashara na uwekezaji Nchini kama zilivyoainishwa katika Taarifa ya Hali ya Kufanya Biashara Nchini ya mwaka 2009. Serikali pia, itakamilisha Sera ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma *(Public Private Partnership Policy)* Nchini. Uzoefu wa Mataifa mbalimbali yakiwemo ya Marekani, India, Afrika Kusini, Misri, Ufaransa na Uingereza unaonyesha kuwa Sekta Binafsi ikishirikishwa ipasavyo katika kuendeleza miundombinu na kutoa huduma muhimu, mzigo katika Bajeti ya Serikali utapungua na kuiwezesha Serikali kugharamia majukumu mengine ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania imeendelea na juhudi za kuhamasisha Uwekezaji wa Ndani na Nje ya Nchi kwa lengo la kuongeza ubia, kujenga uwezo wa ushindani, kukuza Sekta Binafsi na hatimaye kukuza Uchumi wa Taifa. Kutokana na juhudi hizo, idadi ya Makampuni ya Kitanzania yameongezeka kujiandikisha ili kunufaika na vivutio vya Uwekezaji vinavyotolewa na Kituo hiki. Katika mwaka 2008/2009, Kituo cha Uwekezaji Nchini kilisajili jumla ya Miradi 797 yenye thamani ya Dola za Kimarekani Bilioni 3.6 ambayo inakadiriwa kutoa nafasi za Ajira 109,328.

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi hiyo, Miradi 454 au asilimia 57 inamilikiwa na Watanzania, Miradi 128 au asilimia 16 ni ya Wageni na Miradi 215 au asilimia 27 ni ya ubia. Sekta ya Utalii ndiyo iliyopata miradi mingi zaidi, kwa Kusajili Miradi 241. Sekta nyingine zilizovutia Wawekezaji wengi ni pamoja na Sekta ya Viwanda Miradi 215 na Sekta ya Nyumba za Biashara Miradi 124. Takwimu za Kimkoa zinaonyesha kuwa, Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro na Pwani iliongoza kwa kusajili miradi mingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania imeendelea kubuni na kutekeleza Mipango mbalimbali ya kuongeza ushiriki wa Wananchi katika kuwekeza Nchini. Kituo kimebuni mpango wa kuwahamasisha Watanzania kujiunga katika Vikundi vya Kiuchumi na kuunda Makampuni endelevu ambayo yanaweza kusajiliwa na kujiendesha kibiashara. Aidha, Kituo kwa kushirikiana na Uongozi wa Mikoa mbalimbali kimeanzisha mpango wa kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali Mikoani ili waweze kutayarisha Taarifa za Miradi inayokopesheka. Tayari kazi hii imeanza katika Mikoa ya Mara na Ruvuma. Kituo pia, kimeanzisha Mpango Maalum wa kuhakikisha kuwa Mikoa ambayo ipo nyuma katika uwekezaji inapanga maeneo ya Uwekezaji na kuyanadi kwa pamoja kupitia Kituo hiki. Mpango huu unajulikana kama Regional Partnership Program na umeanza katika Mikoa Mitano ambayo ni Rukwa, Kagera, Tabora, Tanga na Singida.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Biashara. Baraza la Taifa la Biashara limeendelea kukuza mashauriano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa madhumuni ya kuboresha mazingira ya Biashara na Uwekezaji. Katika mwaka 2008/2009, Baraza lilifanya Mikutano ya Wawekezaji wa Nje na Ndani.

Mheshimiwa Spika, katika Mikutano hiyo, majadiliano yalilenga kutathmini uelewa wa dhana nzima ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kuanzisha majadiliano katika ngazi ya Wilaya kwa kushirikisha Wadau mbalimbali na kuboresha mazingira ya biashara na fursa za uwekezaji Nchini kwa kuzingatia hali ya Uchumi Duniani. Aidha, Mheshimiwa Rais alizindua Mabaraza ya Biashara ya Wilaya zote Tanzania Bara ambayo yatashirikisha Wananchi kwenye mijadala ya maendeleo ngazi ya chini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 hadi 3 Juni 2009, Baraza la Taifa la Biashara liliandaa Mkutano Maalum na wa Kihistoria kuhusu Kilimo uliohudhuriwa na Wadau kutoka Sekta ya Umma na Binafsi kwa lengo la kujadili mikakati thabiti itakayoleta Mapinduzi ya Kijani ambayo yatafanya Kilimo chetu kiwe cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara. Mkutano huo ambao ulifunguliwa na kuongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ulihudhuriwa pia na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, Watendaji Wakuu Serikalini, Wakulima na Wawekezaji. Aidha, nilipata fursa ya kushiriki katika Mkutano huo ambao Kauli Mbiu yake ni “KILIMO KWANZA” ikiwa na maana kuwa mambo mengine yote yanaweza kusubiri isipokuwa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huo ulikuwa na mafanikio makubwa, kwa sababu tuliweza kufikia muafaka kuhusu hatua za kuleta Mapinduzi ya Kilimo Nchini, ikiwa ni pamoja na:-

(i) Viongozi na Watendaji wote kuwa na utashi wa kuendeleza Kilimo;

(ii) Kuwekeza zaidi katika Kilimo;

(iii) Kuanzisha Benki ya Kilimo; na

(iv) Kila Sekta kutayarisha Mpango Kazi wa kutekeleza “KILIMO KWANZA”.

Mheshimiwa Spika, wadau wote walikubaliana kuwa wakati umefika kukipa Kilimo kipaumbele kwani ndiyo nguzo kuu ya Uchumi wetu na pia Kilimo ndicho kitawezesha Wakulima wengi na Wananchi waishio Vijijini kutoka katika maisha duni na kufikia maisha bora tunayoyataka. Serikali inakamilisha Mpango Kazi wa kutekeleza mapendekezo ya Mkutano huo na utakapokamilika utasambazwa kwa Wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ili uwe Mwongozo wa kuhamasisha Wananchi katika jitihada za kuleta Mapinduzi ya Kilimo Nchini.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini. Katika mwaka 2008/2009, Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini imewezesha Asasi 276 za Kifedha kuwa na mifumo Bora ya Usimamizi na Uongozi. Wakufunzi kumi wa Asasi za kutoa Huduma za Mafunzo walihitimu na kupata Vyeti vya Utambuzi kama Wakufunzi wa Masuala ya Kifedha *(Accredited Trainers in Microfinance Best Practices).* Aidha, Asasi ndogo za Kifedha 140 zimeunganishwa na Mabenki na Asasi kubwa za Kifedha. Asilimia 40 ya Wanachama wa Asasi hizo ndogo ni Wanawake. Programu pia, ilikabidhi shughuli zake pamoja na nyenzo za kufanyia kazi kwa Halmashauri za Wilaya 12 ambazo ni Same, Mwanga, Rombo, Moshi (V), Dodoma (V), Mpwapwa, Kondoa, Njombe, Mufindi, Mbeya (V), Mbarali na Rungwe, kati ya Wilaya 22 ambazo ilikuwa inafanya kazi. Programu inaendelea kutekeleza shughuli zake katika Wilaya 10 zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Programu itaendelea kuboresha usimamizi na uendeshaji wa Asasi ndogo za fedha, kuimarisha mifumo ya fedha Vijijini na kuwajengea uwezo Wananchi Vijijini ili waweze kujiunga na kushiriki katika shughuli za SACCOS. Aidha, Programu itaendelea kuimarisha Benki za Wananchi, mitandao ya Asasi za Kifedha na kuendelea kusaidia mchakato wa uanzishwaji wa Benki za Wananchi. Natoa wito kwa Wananchi wajiunge kwa wingi katika Vyama vya Kuweka na Kukopa ili waweze kutumia fursa mbalimbali za Mikopo zinazojitokeza ambazo zitawasaidia kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo. Katika mwaka 2008/2009, Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo iliendelea kutekeleza shughuli zake kwenye maeneo mbalimbali katika Mikoa Nane ya Tanzania Bara. Mojawapo ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kutungwa kwa Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo. Sera hii imetoa mwelekeo na Mwongozo katika kuimarisha na kuendeleza mifumo ya Masoko ya mazao na bidhaa za

Kilimo kwa kuondoa vikwazo vinavyokabili ushiriki, uendeshaji na unufaikaji wa Mfumo wa haki na usawa kwa Wadau wote wanaoshiriki katika Soko huru la Mazao na Bidhaa za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na uwezeshaji wa Wazalishaji Wadogo katika ushiriki wa Masoko ya Bidhaa wanazozalisha, na ongezeko la idadi ya Washiriki katika Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Vilevile, Programu imejenga na kukarabati miundombinu ya Masoko kwenye Wilaya Nane za Awamu ya Mwisho ambazo ni Korogwe, Mwanga, Moshi Vijijini, Simanjiro, Kyela, Nkasi, Njombe na Makete.

Pia, shughuli kama hizi ziliendelezwa katika Wilaya nyingine chache za Awamu ya Pili ambazo ni Mbozi, Same na Mbulu. Kwa ujumla shughuli hizi zimeleta mafanikio makubwa kulingana na makusudio ya Programu ambayo ni kuongeza kipato kwa Wananchi na kuwa na uhakika wa Chakula.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Programu itasimamia na kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba shughuli zake zinakuwa endelevu hata baada ya Programu kumaliza muda wake kwa kuziwezesha Halmashauri husika kuingiza shughuli za Programu katika Mipango yao ya Maendeleo. Aidha, Programu kwa ushirikiano na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko itakamilisha Mchakato wa uandaaji wa Mkakati wa utekelezaji na Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo. Programu pia, itakamilisha ukarabati wa Barabara za Vijijini na ujenzi wa Masoko katika Wilaya za Awamu ya Mwisho.

Mheshimiwa Spika, Kilimo. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, inatamka bayana umuhimu wa Maendeleo ya Kilimo chenye Tija kama njia ya kuharakisha Maendeleo Vijijini kwa kuongeza mapato na pia kujitosheleza kwa chakula. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inatambua umuhimu wa Kilimo cha Kisasa kama sharti muhimu katika kujenga msingi wa Uchumi wa kisasa. Ili kuboresha Kilimo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za Kisera na Kibajeti ikiwemo kushirikiana na Wananchi kuandaa Miradi ya Pamoja ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2008, Serikali iliitisha Mkutano wa Wadau wa Kilimo kutoka Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Kigoma, Rukwa na Ruvuma ambayo inazalisha chakula kwa wingi ili kujiwekea mikakati ya kuendesha Kilimo cha Kisasa zaidi kwenye Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuhimiza Mikoa hiyo yenye ardhi nzuri na mvua za kutosha kati ya Milimita 800 hadi 1,500 kuwa kichocheo cha kuongoza Mapinduzi ya Kilimo katika kuzalisha na kujitosheleza kwa chakula. Katika Mkutano huo, tuliwekeana maazimio na tukakubaliana namna ya kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi na Mei 2009, nilitembelea Mikoa hiyo kujionea mwenyewe utekelezaji wa yale tuliyokubaliana. Baada ya ziara yangu katika Mikoa hiyo Sita, nimeona kazi inayofanyika na kujifunza mambo mengi. Kwa ujumla tumeanza vizuri utekelezaji wa Maazimio na Malengo tuliyojiwekea. Katika maeneo mengi niliyotembelea nimefarijika sana kuona mabadiliko ya tija yanaanza kujitokeza, hasa maeneo yale ambayo yanatumia Skimu za Umwagiliaji. Kwa mfano, uzalishaji wa Mpunga umeongezeka kutoka wastani wa Magunia 15 hadi 50 kwa Hekta katika Skimu za Umwagiliaji za Igomelo (Mbarali) na Iganjo (Uyole). Uzalishaji wa mahindi nao umeongezeka na kufikia Magunia 50 kutoka wastani wa Magunia 30 kwa Hekta, maharage nayo yameongezeka kutoka wastani wa Magunia 10 hadi kufikia 20 kwa Hekta. Vilevile, kwenye Skimu hizi Wakulima wanaweza kuvuna mazao mara mbili. Hii inaonyesha kwamba kuna umuhimu wa kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji ili kuongeza tija na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kilimo tunachokitaka ni lazima kiwe chenye tija, cha kisasa na kibiashara. Hata hivyo, ili kuongeza tija na uzalishaji, ni lazima kutumia mbegu bora, mbolea na utaalam. Serikali imekuwa ikitoa mbolea ya ruzuku kwa miaka kadhaa sasa ili imsaidie Mkulima kupunguza ukali wa bei za mbolea. Kwa mara ya kwanza, katika mwaka 2008/2009, Serikali ilianza kutoa mbolea ya ruzuku kwa kutumia Mfumo wa Vocha. Hadi kufikia mwezi Aprili 2009, Mbolea ya Ruzuku kiasi cha Tani 141,050 sawa na Vocha 1,496,000 zilisambazwa Nchini.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya awali ya Mfumo wa Vocha imeonyesha kwamba ni mfumo mzuri kwani tofauti na Mfumo tuliokuwa tunatumia awali, unamnufaisha Mkulima moja kwa moja na siyo Mtu wa Kati. Kwa kuwa ni Mfumo mpya, zimejitokeza changamoto mbalimbali katika utekelezaji. Serikali inazifanyia kazi changamoto hizo ili Mfumo huo uzidi kuwa bora zaidi na kuwafikia walengwa wengi zaidi. Ni vyema sote tufahamu kwamba, mbolea inayotolewa inalenga kukuza uzalishaji katika Kilimo, hivyo Wakulima watumie nafuu hiyo ya bei ya mbolea kuzalisha zaidi na si kuiuza tena kwa Mawakala. Kufanya hivyo ni kosa na wale watakaofanya hivyo watakuwa wanahujumu maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali pia ilitoa ruzuku ya Mbegu Bora zenye jumla ya Tani 7,180, sawa na Vocha 624,500. Vilevile, Mfuko wa Pembejeo umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.8 kwa ajili ya kununua Matrekta Makubwa 66 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.3, Matrekta Madogo 29 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.0 na Pembejeo nyingine zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.5. Wakati huo huo, tathmini ya matumizi sahihi ya Matrekta 200 yaliyokopeshwa kwa Wakulima kupitia Mfuko wa Pembejeo imefanyika katika Kanda Saba za Kilimo ili kuweza kutoa ushauri wa kiufundi kuhusu Kilimo cha kibiashara na faida za kutumia zana bora za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imeelekeza Serikali kuwaandaa Maafisa Ugani wa fani mbalimbali za Kilimo na kuwapeleka katika

maeneo wanakohitajika. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya Wataalam wa Ugani 544 waliajiriwa na kupangiwa kazi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pamoja na Serikali kuajiri Wataalam wa Ugani kila mwaka, bado mahitaji yao ni makubwa na hivyo kuhitaji ubunifu zaidi ili kufanya Mapinduzi ya Kilimo kwa kasi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mkoa wa Kigoma umewakusanya Vijana kutoka Vijiji mbalimbali na kuwapa mafunzo ya muda mfupi ya vitendo kuhusu Kanuni Bora za Kilimo ambazo watazitumia Vijijini kwao mara wanapomaliza mafunzo hayo na kusaidia Wanavijiji wengine. Vijana hawa wanaitwa Waganikazi. Hii ni hatua ya kupongezwa na kuungwa mkono na kila mpenda Kilimo. Naupongeza sana Uongozi wa Mkoa wa Kigoma kwa Ubunifu huu na Vijana walioitikia wito huo. Natoa wito kwa Mikoa mingine kuiga mbinu za Mafunzo ya Waganikazi hao na kuzitekeleza katika Mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, Utafiti umeendelea kupewa umuhimu mkubwa katika kuendeleza Kilimo katika nyakati hizi ambazo Dunia inashuhudia mabadiliko makubwa ya Tabianchi. Vituo vyetu vya utafiti vya mazao ya Kilimo viliendesha tafiti mbalimbali na kugundua aina mpya za mbegu bora zikiwemo nyanya, maharage, pamba na mahindi. Vilevile, Miradi 55 ya Utafiti iliendelea kutekelezwa chini ya Mfuko wa Utafiti ambao unatekelezwa Kikanda. Tafiti hizo zinawahusisha Wakulima, Wagani, Wasambazaji Pembejeo, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Watafiti wenyewe kwa lengo la kutoa na kusambaza teknolojia zenye ubora. Natoa wito kwa Watafiti na Vituo vya Utafiti kujizatiti kutafiti mbegu bora na kusambaza matokeo ya tafiti zao kwa Wakulima, Wafugaji na Maafisa Ugani. Aidha, Viongozi wawe na mashamba ya mfano ili kuongeza kasi ya usambazaji wa teknolojia zinazogunduliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaongeza usambazaji wa aina mbalimbali za Pembejeo za Kilimo ili Wakulima waweze kuongeza tija zaidi. Aidha, itahimiza matumizi ya Zana Bora za Kilimo ambapo Halmashauri za Wilaya Nchini zitanunua jumla ya Matrekta ya Mkono 1,628 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 10.6 na Matrekta Makubwa 55 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 2.2. Fedha hizi zimetengwa kwenye Bajeti za Halmashauri zetu.

Vilevile, Mikoa ya Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Rukwa na Ruvuma imepangiwa kupewa ruzuku ya Shilingi Bilioni 29.2 za Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya *(DADP's)* kama chachu ya kuongeza uzalishaji wa chakula katika Mikoa hiyo. Kama tulivyokubaliana katika Mkutano wa "KILIMO KWANZA", kazi ya kusukuma Kilimo siyo ya Wizara ya Kilimo peke yake. Hili ni jukumu la Viongozi na Watendaji wote katika ngazi zote wakishirikiana na Wananchi wote. Kwa hiyo, sote tushikamane kuleta Mapinduzi ya Kilimo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Umwagiliaji. Moja ya maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 ni kuweka kipaumbele zaidi katika Kilimo cha Umwagiliaji Maji, msisitizo ukiwa kwenye Miradi Midogo na ya Kati. Ili kutekeleza maelekezo hayo,

katika mwaka 2008/2009, Serikali iliongeza kiasi cha Hekta 27,500 za Umwagiliaji na kuwezesha eneo lote lililoendelezwa kwa umwagiliaji hapa Nchini kufikia hekta 318,745. Aidha, kupitia *DADP's*, Miradi ya Umwagiliaji 167 imejengwa, 94 imekarabatiwa, Visima vifupi 18 vimejengwa na jumla ya Pampu 84 zimenunuliwa na kugawanywa kwa Wakulima kwa ajili ya Umwagiliaji wa Mazao ya Bustani. Vilevile, jumla ya Miradi 141 ya Umwagiliaji imefanyiwa tafiti za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, hali hii imefanya maeneo mengi ya Kilimo cha Umwagiliaji yaliyoboreshwa kuongeza uzalishaji na hivyo kuwa kichocheo cha kupiga vita umasikini na kuwaongezea Wananchi kipato. Katika maeneo ambayo Miundombinu ya Umwagiliaji imeboreshwa kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji na kuweza kuvuna mara 2 hadi 3 ikilinganishwa na uzalishaji wa Kilimo cha kutegemea Mvua. Natoa wito kwa Maafisa Kilimo wa Halmashauri zote kuwasaidia Wakulima kuibua Miradi Midogo ya Umwagiliaji katika Wilaya zao kwani wanahitaji msaada katika kuibua Miradi mizuri na yenye matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, Mifugo. Serikali inaendelea kufanya jitihada za kutenga ardhi kwa ajili ya Mifugo ili kupunguza na hatimaye kumaliza migogoro inayotokea mara kwa mara kati ya Wakulima na Wafugaji. Hata hivyo, kumeendelea kuwepo kwa migogoro ya matumizi ya rasilimali mbalimbali hasa Ardhi, Maji na Malisho katika baadhi ya Wilaya. Serikali haipendi kuona migogoro hii ikiendelea kwani inapotokea huambatana na madhara makubwa ambayo wakati mwingine husababisha kupotea kwa mali za Wananchi, kupoteza maisha na kusababisha Majeraha kwa Watu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo, kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2008/2009, jumla ya Hekta 1,391,109.4 za Ardhi zimetengwa katika Vijiji 240 vya Wilaya 31 katika Mikoa 13 kwa ajili ya Mifugo. Natoa wito kwa Viongozi wote wa Mikoa na Wilaya kuongeza kasi ya kutenga maeneo kwa ajili ya Malisho ya Mifugo na kuhakikisha kwamba utengaji huo hauna madhara kwa mazingira. Aidha, Wakulima na Wafugaji wote Nchini waheshimu Haki na Mipaka ya kila mmoja ili waendelee kuishi kwa amani na kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kwa uhakika. Serikali inathamini mchango wa Wakulima na Wafugaji na inaheshimu Haki zao za kufanya kazi za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi. Sekta ya Uvuvi imeendelea kuchangia ukuaji wa Uchumi wetu na kupunguza umasikini. Hata hivyo, Sekta hiyo inakabiliwa na tatizo kubwa la nyenzo duni na Uvuvi Haramu. Katika mwaka 2008/2009, Serikali imechukua hatua za kudhibiti na kupambana na Uvuvi Haramu kwa kufanya doria na kutoa elimu kuhusu athari za Uvuvi Haramu. Aidha, Zana Haramu nyingi zilikamatwa zikiwemo Nyavu zisizoruhusiwa, Makokoro, Mitumbwi na Boti. Vilevile, Meli kubwa ya Uvuvi (Tawariq 1) iliyokuwa ikivua kinyume cha Sheria katika Bahari Kuu ya Tanzania ilikamatwa na kukutwa na jumla ya Tani 294 za Samaki.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuona kwamba Rasilimali za Tanzania tulizopewa na Mwenyezi Mungu zinawanufaisha Wananchi wote na siyo wajanja wachache wanaotumia Uvuvi Haramu kuhujumu rasilimali tulizonazo. Napenda tena nichukue fursa hii kuwaonya wale wote wanaoendesha Uvuvi Haramu kwa njia yoyote ile, wawe wa Ndani au wa Nje waache. Doria zitaendelea kuimarishwa katika maeneo yote ya Nchi na wale watakaokamatwa watachukuliwa hatua kali za Kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kuboresha Miundombinu muhimu ya Mifugo kama Maabara ya Mifugo, Majosho, Malambo na Minada. Aidha, itapima maeneo ya Wafugaji, kufanya Sensa ya Mifugo na kuimarisha Vituo vya Utafiti vya Mifugo. Vilevile, itaimarisha Miundombinu ya kupokelea, kuhifadhi, kusafirisha Samaki na Mazao ya Uvuvi, kudhibiti Uvuvi Haramu na kuhifadhi mazingira na kuimarisha shughuli za utoaji wa huduma za Ufugaji wa Samaki na ukuzaji wa Viumbe wengine kwenye Maji.

Mheshimiwa Spika, Viwanda na Biashara. Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini, inaendelea kuimarika kutokana na juhudi za Serikali kuwajengea uwezo Wajasiriamali Wadogo kuanzisha Viwanda Vidogo na vya Kati na kuhimiza wenye Viwanda vikubwa kuongeza tija katika uzalishaji wa bidhaa. Katika mwaka 2008/2009, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa umeongezeka kama vile saruji, chuma, nguo, vyandarua, sigara na vifaa vya plastiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Serikali imetoa mafunzo kwa Wajasiriamali 1,989 wa Viwanda Vidogo vya Usindikaji wa Vyakula na Wajasiriamali 6,224 wa bidhaa nyingine mbalimbali ili kuwapa ujuzi maalum wa kiufundi na Teknolojia mpya. Aidha, Serikali imekamilisha maandalizi ya Mkakati Unganishi wa Biashara (*Tanzania Trade Integration Strategy*) ambao unalenga kukuza Sekta ya Biashara na kujenga uwezo wa kiushindani wa Wafanyabiashara wa ndani. Utekelezaji wa Mkakati huo unatarajiwa kuongeza mauzo nje kwa kutumia rasilimali zilizopo na kutumia vizuri fursa kubwa za Biashara za Kikanda na Kimataifa tulizo nazo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008 thamani ya mauzo ya bidhaa nje yaliongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani Milioni 3,036.7 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani Milioni 2,226.6 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Mwenendo huu wenye matumaini unatokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kutafuta Masoko ya Nje. Hata hivyo, bado ipo changamoto kubwa ya kutafuta Masoko zaidi, hasa katika Nchi za Ukanda wa Afrika ambapo kuna mahitaji makubwa ya bidhaa mbalimbali kutoka Tanzania. Ni wazi Nchi hizo zina masharti rahisi ya kibiashara ikilinganishwa na Nchi Zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tuelekeze nguvu zetu kwenye Masoko ambayo yana viwango vya ubora tunavyovimudu, kwa kuwa Nchi Zilizoendelea wakati mwingine zinaweka vikwazo visivyo vya lazima kwa lengo la kupunguza bidhaa zetu hasa kutoka

Nchi changa. Nina imani kuwa tukitumia vizuri mtaji wa Mahusiano mazuri ya Kidiplomasia tuliyonayo na Nchi nyingi za Afrika na kwingineko, tutakuwa na uwezo wa kufikia Masoko mengi na kuuza bidhaa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Maeneo Maalum ya uzalishaji kwa ajili ya uuzaji nje na Uwekezaji katika viwanda ndani ya maeneo hayo. Hadi sasa Mikoa 14 imeainisha maeneo maalum ya kuzalisha na kuuza bidhaa nje (*Export Processing Zones and Special Economic Zones).* Maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Kigoma, Tanga, Pwani, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Mara, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Morogoro, Kagera, Mbeya na Manyara.

Mheshimiwa Spika, Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kuendeleza maeneo hayo umeandaliwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Aidha, ujenzi wa miundombinu katika eneo maalum la uwekezaji la Benjamin William Mkapa Special Economic Zone lililoko Mabibo Jijini Dar es Salaam umekamilika. Eneo hili limewekewa miundombinu na huduma zote muhimu na Serikali. Natoa rai kwa Wafanyabiashara na Sekta Binafsi kwa ujumla wake kutumia kikamilifu fursa hizi ili kukuza Sekta ya Viwanda Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itapitia upya Sheria za Maeneo Maalum ya Kukuza Mauzo Nje ili kuandaa Sheria Unganishi itakayoboresha zaidi Mfumo wa usimamizi wa maeneo hayo na kuwawezesha Wawekezaji wa Sekta mbalimbali wanaolenga Soko la Ndani na Nje kuwekeza katika eneo moja. Vilevile, Serikali itaimarisha Mafunzo ya Ujasiriamali pamoja na kuhimiza kuanzishwa kwa Viwanda vya Usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini ili kuongeza thamani ya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Utalii. Sekta ya Utalii ina umuhimu mkubwa katika Uchumi wetu hasa katika kuiletea Nchi yetu Fedha za Kigeni. Utalii unachangia asilimia 28 ya Mapato ya Fedha za Kigeni yatokanayo na huduma zitolewazo nje ya Nchi. Katika mwaka 2008/2009, Serikali imeanza zoezi la kupanga Hoteli katika Madaraja na kuhakikisha zinakuwa katika hali ya unadhifu kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Zoezi hilo limeanzia Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kazi itaendelea kwa Mikoa ya Arusha, Manyara na sehemu nyingine. Vilevile, maeneo ya Fukwe kwa ajili ya Uwekezaji yalibainishwa katika Wilaya za Pangani, Tanga, Mkinga, Muheza, Lindi na Kilwa. Serikali pia, iliendelea kupanua wigo wa Utalii kwa kuainisha aina nyingine za Utalii kama vile Utalii wa Mikutano, Fukwe za Bahari, Ekolojia na Malikale.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaweka mkazo katika kutangaza zaidi vivutio vyetu na kutafuta masoko mapya. Aidha, itaendelea kutangaza Utalii wa Ndani, Utalii wa Mikutano na kuboresha viwango vya huduma zitolewazo kwa Watalii. Serikali pia, itaongeza juhudi zaidi katika kutangaza Utalii wa Utamaduni na

mambo ya Kale kama vile, Miji Mikongwe ya Kilwa na Mikindani ili iweze kuvutia Watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Nishati. Sekta ya Nishati bado ina changamoto kubwa katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa Umeme katika Gridi ya Taifa. Hali hii inasababishwa na Miundombinu chakavu inayohitaji ukarabati wa mara kwa mara. Pamoja na hali hiyo, mahitaji ya umeme ni makubwa kuliko uzalishaji na yanaendelea kukua. Ili kuendana na kasi ya ukuaji huo, Serikali imeandaa Mpango wa muda mrefu, kati na mfupi wa kuimarisha Sekta ya Nishati hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kukarabati na kununua mitambo mipya na kukamilisha mradi wa umeme wa Tegeta/Salasala wa MW 45. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itaimarisha Gridi ya Taifa, itaendelea na ukarabati wa Mitambo iliyopo na kununua Jenereta mpya kwa ajili ya maeneo yasiyokuwa na umeme wa Gridi. Aidha, Serikali itaandaa Programu ya Kupunguza Matumizi ya Umeme, hususan, Viwandani na Majumbani ili kupata umeme wa ziada kwa watumiaji wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Madini. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imeelekeza kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo katika nyanja mbalimbali ikiwemo kuimarisha usalama migodini. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Serikali imetenga maeneo katika sehemu mbalimbali Nchini likiwemo eneo lenye Hekta 4,000 huko Winza Wilayani Mpwapwa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wachimbaji Wadogo imeanza kuweka Utaratibu wa Uchimbaji Salama unaozingatia Sheria, Kanuni, uhifadhi wa mazingira na Uchimbaji unaotumia Teknolojia ya Kisasa.

Mheshimiwa Spika, mafunzo maalum kuhusu masuala hayo yameanza kutolewa kwa awamu. Awamu ya Kwanza ya mafunzo hayo yalifanyika mwezi Mei 2009, kwa Wachimbaji Wadogo wa Wilaya ya Geita. Serikali pia, imeanza mchakato wa kuaandaa mapendekezo ya Sheria ya Usonara na Uongezaji Thamani ya Madini ambayo itaweka mazingira ya kuwezesha kuongeza thamani ya Madini yetu kabla ya kuuza nje kwa bei kubwa zaidi. Utaratibu huu utaongeza Pato la Taifa na Ajira kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itapitia upya Sera na Sheria ya Madini ambayo itatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa na Wadau mbalimbali ikiwemo Kamati ya Jaji Mark Bomani. Serikali pia, itaendelea kuboresha uchimbaji mdogo kwa lengo la kuinua kipato cha Wachimbaji Wadogo na Uchumi kwa ujumla. Aidha, itatoa mafunzo yanayohusu njia salama za uchimbaji na kuwashawishi wajiunge katika Vikundi ili waweze kupata mitaji kwa urahisi. Nichukue tena fursa hii kutoa wito kwa Wachimbaji Wadogo kufanya shughuli zao kwa makini na uangalifu na washirikiane na Serikali katika jitihada inazofanya za kuimarisha na kuboresha usalama katika migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara. Serikali imeendelea kujenga na kuboresha mtandao wa barabara nchini kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Lengo ni kuunganisha Nchi nzima na mtandao mzuri wa barabara zinazopitika wakati wote. Pamoja na mahitaji makubwa ya Barabara nzuri, ujenzi wake ni wa gharama kubwa na una mchakato mrefu kuanzia upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, ujenzi wa baadhi ya Barabara Kuu na za Mikoa ulikamilika na ujenzi wa Barabara nyingine nyingi upo katika hatua mbalimbali. Serikali itaendelea kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kutangaza zabuni za ujenzi pamoja na ukarabati wa Barabara Kuu na za Mikoa. Nina uhakika kwamba ujenzi wa barabara hizo utakapokamilika, utafungua fursa nyingi za kiuchumi kwa Wananchi wa maeneo hayo na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tuna kazi kubwa ya ujenzi wa Barabara lakini pia namna ya kuzitunza. Barabara zetu zikiwa nzuri zitarahisisha mazao mengi ya Wakulima kupelekwa kwenye masoko ya Ndani na Nje na wao kupata bei nzuri na ari ya kuzalisha zaidi. Hivyo, ni jukumu letu sote kujenga na kutunza vizuri Barabara hizo. Matatizo ya kukarabati Barabara mara kwa mara yatapungua kama Teknolojia sahihi na Viwango vya Kitaalamu vitafuatwa katika hatua zote za ujenzi wa Barabara zetu. Natoa wito kwa Makandarasi kuzingatia Viwango vya Ubora katika ujenzi wa Barabara na kuzikamilisha kwa wakati. Aidha, Mamlaka husika kwa kushirikiana na Wananchi zisimamie kikamilifu utunzaji wa Barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vivuko. Serikali imedhamiria kuboresha Vivuko mbalimbali hapa Nchini kwa kuvifanyia ukarabati vilivyochakaa na kununua vipya. Katika mwaka 2008/2009, Kivuko kikubwa cha MV Magogoni (Dar es Salaam) kilianza kufanya kazi. Kivuko hiki kilizinduliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Juni 2009. Vivuko vya MV Kigamboni (Dar es Salaam) na MV Sengerema (Mwanza) vinaendelea kufanyiwa ukarabati mkubwa. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itakamilisha kutengeneza Vivuko vinne vya Musoma - Kinesi, Rugezi - Kisorya, Utete na Mto Pangani. Aidha, Vivuko vipya vya Kilambo (Mtwara), Msanga Mkuu (Mtwara) na Rusoma (Ngara) vitanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege. Serikali inaendelea na juhudi za kuboresha Sekta ya Uchukuzi ili kuongeza ufanisi na kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili Wananchi. Moja ya kazi zilizofanyika ni uboreshaji, upanuzi na matengenezo ya Viwanja vya Ndege. Katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea na Awamu ya Pili ya ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza umekamilika na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe unaendelea. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itaboresha Viwanja vya Ndege vya Ziwa Manyara, Arusha, Tabora, Shinyanga na Musoma. Aidha, Mitambo mbalimbali ya kisasa kwa ajili ya ukaguzi wa abiria na mizigo na ya kutoa taarifa za safari za ndege itafungwa katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza na Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, Mawasiliano. Kutokana na kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na umuhimu wa kuwa na miundombinu ya uhakika ya mawasiliano na yenye gharama nafuu, mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa ulianza rasmi mwezi Februari 2009. Mkongo huo wa Taifa unatarajiwa kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar. *(Makofi)*

Mradi huo utakapokamilika utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano ya Kikanda na Kimataifa kutokana na fursa yake ya kijiografia ya kuzungukwa na Nchi nyingi ambazo hazijapakana na Bahari. Sambamba na hatua hiyo, Serikali imekamilisha taratibu za kuanzisha Mfuko wa Huduma za Mawasiliano ambao unalenga kusaidia kufikisha huduma za Mawasiliano ya Simu na Internet hadi Vijijini, hasa sehemu ambazo hazina mvuto kibiashara. Nitumie fursa hii kuyapongeza Makampuni yote ya Simu kwa jitihada kubwa za kupanua kwa kasi huduma za mawasiliano ya simu Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za Mawasiliano Nchini ikiwemo huduma za Posta. Aidha, itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Ardhi. Serikali inatekeleza Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ili kuwawezesha Watanzania wengi kutumia ardhi kama dhamana ya kupata mikopo. Ardhi pia ni Rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Sekta nyingine. Katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea kutoa Hati za Kumiliki Ardhi na Vyeti vya Ardhi ya Vijiji kwa Wananchi. Utoaji wa Hatimiliki umerahisishwa kwa kuanzisha Ofisi za Makamishna wa Ardhi Wasaidizi katika Kanda sita ambazo zitatoa huduma kwa Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Ofisi hizo za Kanda ni pamoja na utoaji wa hati za Ardhi hasa zilizokuwa zinawasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya kusainiwa. Utaratibu huu umeongeza kasi ya utayarishaji na Usajili wa Hatimiliki. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itaziboresha Ofisi za Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Kanda kwa kuongeza Watumishi na vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Upimaji wa Vijiji na Viwanja Mijini. Serikali imeendelea kupima Viwanja Mijini na mipaka ya Vijiji. Tangu zoezi la Upimaji wa Vijiji lianze kutekelezwa, jumla ya Vijiji 9,500 vimepimwa kati ya Vijiji vipatavyo 11,000 Nchini kote. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Serikali ilipima Vijiji 450 na Ardhi za Wananchi sehemu mbalimbali Nchini.

Aidha, kutokana na kufunguliwa Ofisi za Ardhi za Kanda, kasi ya kuandaa na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji imeongezeka ambapo jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 910 vilitolewa katika Wilaya 25 Nchini. Vilevile, Serikali imeendelea kupunguza uhaba wa Viwanja kwenye Miji Mikubwa inayopanuka kwa kasi kama Jiji la Dar es Salaam,

Mwanza na Mbeya kwa kupima Viwanja vingi kwa mtindo wa kurejesha gharama za upimaji. Halmashauri za Miji na Wilaya zinahimizwa kutekeleza Miradi ya Upimaji wa Viwanja kwa kuzingatia dhana ya kuchangia gharama kama ilivyofanyika katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya, na Manispaa ya Dodoma na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya elimu. Elimu ya Msingi. Katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM-II) ambao utamalizika mwaka 2011. Mpango huu unaendeleza mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Awamu ya Kwanza pamoja na kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza hususan upungufu wa Walimu, Vitabu vya Shule pamoja na uhaba wa Nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Spika, chini ya Mpango huu, idadi ya Shule za Msingi za Serikali imeongezeka kutoka 15,122 mwaka 2007 hadi Shule 15,257 mwaka 2008. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wananchi na Wadau mbalimbali wa Elimu imeboresha kwa kiasi kikubwa mazingira na miundombinu mbalimbali ya Shule za Awali na Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuinua zaidi ubora wa Elimu ya Msingi Nchini, napenda kuzikumbusha Halmashauri zote kuendelea kuimarisha usimamizi na kuelimisha Jamii na Kamati za Shule ili watambue kuwa Mpango wa kuboresha Shule za Awali na Msingi ni endelevu na hivyo ni lazima wajihusishe nao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Chakula cha Mchana kwa Wanafunzi. Shule zetu za Awali na Msingi zinakabiliwa na changamoto ya kuwawezesha Watoto kupata chakula cha mchana Mashuleni. Tafiti zilizofanyika katika Mikoa ya Dodoma, Manyara, Singida na Arusha zimeonyesha kuwa Shule zinazotoa chakula cha mchana kwa Wanafunzi zimepata mafanikio ya kupunguza utoro Mashuleni na kuongeza kiwango cha ufaulu. Hata hivyo, fedha za kununua chakula hicho zimekuwa zinapatikana kwa kufanya matembezi ya hisani ambayo yalianzishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani. Lengo la matembezi hayo ni kutunisha Mfuko wa Kuondoa Njaa Mashuleni unaochangiwa na Wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo linalosikitisha ni kwamba kutokana na matembezi hayo, inaonekana baadhi ya Wazazi wamesahau wajibu wao wa kuhakikisha Watoto wetu wanapata mlo wa mchana wawapo Shuleni. Kama Mzazi, ninaamini kuwa Wajibu wa kwanza ni kuwalea na kuwakuza Watoto katika Maadili na Tabia njema pamoja na kuwapatia chakula bora. Siamini kuwa kama Mzazi anaweza kumpa Mtoto chakula cha asubuhi au jioni atashindwa kuchangia chakula cha Mtoto wake mchana pale Shuleni. Ninawasihi Wazazi wote wasikwepe wajibu wao wa kuhakikisha Watoto wao wanapata mlo wa mchana wawapo Mashuleni. Hivyo, natoa wito kwa Viongozi wa Shule kukaa pamoja na Wazazi ili kuona njia bora zaidi ya kuhakikisha Wanafunzi wanapata chakula cha mchana wawapo Mashuleni.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari. Wananchi wameitikia kwa ari kubwa wito wa Serikali wa kujenga Shule za Sekondari chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Hatua hii imeongeza nafasi kwa Wanafunzi wengi wanaohitimu Elimu ya Msingi kuendelea na Elimu ya Sekondari. Idadi ya Shule za Sekondari za Serikali imeongezeka kutoka Shule 2,806 mwaka 2007 hadi 3,039 mwaka 2008. Idadi ya Wanafunzi waliojiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule za Serikali imeongezeka kutoka Wanafunzi 401,011 mwaka 2007 hadi 528,149 mwaka 2008. Vilevile, idadi ya Wanafunzi waliojiunga Kidato cha 5 imeongezeka kutoka Wanafunzi 21,789 mwaka 2007 hadi 25,240 mwaka 2008. Ongezeko hili limefanya idadi ya Wanafunzi wote wa Shule za Sekondari Nchini kuanzia Kidato 1 – 6 kuongezeka kutoka Wanafunzi 1,205,510 mwaka 2007 hadi kufikia 1,222,403 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kuongeza ubora katika utoaji wa Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Mafunzo ya Ufundi. Juhudi zitaelekezwa katika kuongeza na kuimarisha Miundombinu muhimu ya Shule za Msingi na Sekondari kama vile ujenzi wa Madarasa, Maabara, Nyumba za Walimu, Maktaba na ununuzi wa Madawati na Vitabu vya kujifunzia na kufundishia. Serikali pia, itaongeza idadi ya Walimu Tarajali ili kukidhi mahitaji yanayotokana na ongezeko la Wanafunzi katika ngazi zote za Elimu na kuimarisha matumizi ya Vituo vya Walimu ili kuboresha ufundishaji hasa katika Masomo ya Sayansi, Lugha na Hisabati.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu. Serikali kwa kushirikiana na Wadau imeendelea kupanua Elimu ya Juu kwa kujenga na kukarabati Vyuo vya Elimu ya Juu. Kazi nyingine ni kuongeza ubora wa miundombinu ya Vyuo vilivyopo ili kukidhi mahitaji ya Elimu ya Juu ambayo yanaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Vyuo Vikuu vya Serikali imeongezeka kutoka Vyuo 8 mwaka 2005 hadi 11 mwaka 2008. Aidha, Vyuo Vikuu Binafsi vimeongezeka kutoka Vyuo 18 mwaka 2005 hadi 21 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu vya Serikali na Binafsi vinavyoendelea kujengwa vimeongeza fursa kwa Wanafunzi kujiunga na Elimu ya Juu. Idadi ya Wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu imeongezeka kutoka Wanafunzi 49,967 mwaka 2007 hadi kufikia 82,529 mwaka 2008. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa mikopo ya kugharamia Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambapo katika mwaka 2008 Wanafunzi 56,071 walipewa mikopo ikilinganishwa na 47,554 mwaka 2007. Sehemu kubwa ya mikopo hiyo imetolewa kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu wanaosoma Masomo ya Ualimu, Uhandisi, Sayansi, Kilimo, Tiba ya Binadamu na Tiba ya Wanyama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kukarabati na kupanua Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma ili Wanafunzi wengi zaidi waweze kujiunga na Vyuo hivyo. Vilevile, Serikali itaongeza kasi ya ujenzi wa Maabara ya Sayansi, Kumbi za Mihadhara, Hosteli, ukarabati wa Miundombinu, upanuzi wa Maktaba na

kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Kisasa (TEKNOHAMA) kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, itaandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambayo utekelezaji wake utaanza mwaka 2010. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wananchi na Wadau wetu wote wa Maendeleo kwa kushirikiana kikamilifu na Serikali katika kuendeleza Sekta ya Elimu Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Huduma za afya na maji. Mpango wa Taifa wa Chanjo. Katika mwaka 2008/2009, Serikali imepata Mpango wa Taifa wa Chanjo mafanikio makubwa katika kutoa huduma za Chanjo Nchini. Viwango vya Chanjo vimeongezeka na kufikia zaidi ya asilimia 80 kwa Chanjo zote. Katika kipindi hicho, Serikali iliendesha Kampeni ya kutokomeza Ugonjwa wa Surua Nchini kwa Kuchanja Watoto 10,567,104 wenye umri kati ya miezi 9 hadi miaka 10. Aidha, Chanjo ya Polio ilitolewa katika Wilaya 18 za Mipakani na zenye Viashiria vya kuambukiza Polio na Watoto 1,459,162 walipata chanjo hiyo. Hatua hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza Vifo vya Watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka Vifo 112 kwa kila Watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2005 hadi Vifo 91 mwaka 2008. Lengo la Milenia ni kupunguza Vifo vya Watoto hadi kufikia Watoto 54 kwa kila Watoto 1,000 ifikapo mwaka 2015. Nina hakika kwa jitihada zinazofanywa na Serikali tutafikia malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaimarisha huduma za Chanjo kwenye Kliniki zote za huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto, huduma za Mkoba na Kliniki Tembezi. Aidha, itatekeleza Mpango Maalum wa Kumfikia kila Mtoto katika Wilaya 48 ambazo zimeonekana kuwa na kiwango cha chini cha Chanjo.

Mheshimiwa Spika, Malaria. Ugonjwa wa Malaria bado unasababisha Vifo vingi kwa Wananchi wetu. Ili kukabiliana na Ugonjwa huo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali. Katika mwaka 2008/2009, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia kwa ajili ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria ulitoa fedha kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 90.5 kwa ajili ya ununuzi wa Dawa Mseto na kuelimisha watoa huduma wote Nchini.

Mheshimiwa Spika, dawa hizo zinatolewa katika Vituo 4,921 vya Tiba Nchini vikiwemo vya Serikali na Binafsi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi walitoa Vyandarua vyenye Viuatilifu kwa bei nafuu kwa Wanawake Wajawazito na Watoto chini ya umri wa miaka mitano waliohudhuria Kliniki ya Mama na Mtoto kupitia Mpango wa Hati Punguzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, ilipata kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 113 kupitia Mfuko huo kwa ajili ya kuwezesha kila Kaya yenye Watoto chini ya umri wa

miaka mitano kupata Vyandarua Viwili vyenye Viuatilifu kwa ajili ya Kinga dhidi ya Malaria. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea na ugawaji wa Vyandarua vyenye Viuatilifu bila malipo kwa Watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Zaidi ya Vyandarua Milioni 14 vitagawanywa kwa kila Kaya yenye Walengwa na kila Kaya itapata Vyandarua Viwili.

Mheshimiwa Spika, Maji. Dira ya Taifa ya Maendeleo, imeweka lengo la kuwapatia Wananchi wote waishio Vijijini na Mijini huduma ya Maji Safi na Salama ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka 2008/2009, utoaji wa huduma za Majisafi Mijini umeboreshwa kwa kukarabati na kupanua Miundombinu ya Mifumo ya Maji safi katika sehemu mbalimbali Nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya Miradi iliyokamilika ni ujenzi wa Mradi wa kutoa Maji Ziwa Viktoria kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na Vijiji 54 vilivyo kando ya Mabomba Makuu. Mradi huu ulizinduliwa na Mheshimwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Mei, 2009. Huu ndiyo Mradi Mkubwa wa maji katika Historia ya Nchi yetu ambao umegharamiwa na Serikali yetu kwa kutumia fedha zetu wenyewe. Hili siyo jambo dogo, kwa kuwa linaonyesha tukidhamiria na kuweka kipaumbele tunaweza kufanya mambo makubwa na ya manufaa kwa Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za Maji Vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati Miradi ya Maji Vijijini na kuchimba Visima. Mafanikio yaliyopatikana katika uboreshaji wa huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ni pamoja na ujenzi wa Vituo vya Kuchotea Maji 1,657 vyenye uwezo wa kuhudumia Wananchi 394,250; jumla ya Visima 407 vilichimbwa na Wananchi 379,609 walihamasishwa kuhusu Usafi wa Mazingira na Elimu ya Afya. Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kutekeleza Programu Ndogo ya Uboreshaji wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira katika Vijiji Kumi vilivyoainishwa kwa kila Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Habari. Sekta ya Habari Nchini imeendelea kukua na kutoa mchango mkubwa katika kuelimisha Jamii kuhusu mambo mbalimbali katika nyanja za Siasa, Demokrasia, Utawala Bora, Uchumi, Maendeleo ya Jamii, Burudani na kutoa habari za matukio mbalimbali. Hadi sasa Vituo 52 vya Redio na 27 vya Televisheni vimesajiliwa. Aidha, idadi ya magazeti na majarida yaliyosajiliwa imefikia 683. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kuna changamoto ya kuimarisha usimamizi wa Vyombo vya Habari na upatikanaji wa habari usioridhisha hasa Vijijini. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali inapitia upya Sera ya Habari ya mwaka 2003 na kukamilisha Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari. Natoa wito kwa Wawekezaji katika Sekta ya Habari kujitokeza kutoa huduma hii katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Michezo. Katika kuendeleza Sekta ya Michezo, Serikali imekamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo (*Sports Complex)* Jijini Dar es Salaam ambapo Viwanja vya Mpira wa Miguu na Riadha vyenye hadhi ya Olimpiki vimekamilika.

Uwanja huo ulizinduliwa rasmi tarehe 15 Februari 2009 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Hu Jin Tao, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China. Ili kuendeleza taaluma ya michezo katika ngazi ya kati, Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya kitaimarishwa kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama. Katika mwaka 2008/2009, Serikali imeendelea kuliwezesha Jeshi la Ulinzi kuimarisha uwezo wake wa kulinda mipaka ya Nchi yetu pamoja na kuimarisha Amani na Utulivu baina ya Tanzania na Nchi nyingine Duniani na hasa Nchi jirani. Hali katika mipaka ya Nchi yetu ni shwari na Wananchi wako huru kutekeleza shughuli zao za kujiletea maendeleo. Watendaji wa Jeshi la Wananchi wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya kuendeleza taaluma zao Ndani na Nje ya Nchi. Aidha, Jeshi limepatiwa Vitendea Kazi mbalimbali ili liweze kutekeleza wajibu wake kikamilifu, hususan kufanya Doria Mipakani, Baharini, kwenye Maziwa na kutoa misaada ya kukabiliana na Maafa au Majanga pindi yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili liwe na taswira ya uzalishaji mali na kutoa mchango kwa Ulinzi wa Taifa. Vijana wa Kitanzania 6,500 wameendelea kupatiwa mafunzo mbalimbali katika Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Lengo ni kufikisha Vijana 10,000 katika mwaka 2010/2011, ambapo Wahitimu wa Kidato cha Sita wataanza kuchukuliwa tena kwa mujibu wa Sheria. Vijana hao, zaidi ya kupata mafunzo ya awali ya Ulinzi na Usalama, watapewa mafunzo katika Stadi mbalimbali zikiwemo za Kilimo, Ufugaji na Ufundi wa aina mbalimbali kwa lengo la kuwafanya wawe na uwezo wa kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kuwa Vijana hao watakapomaliza mafunzo yao watakuwa chachu kwa Vijana wenzao katika kushiriki shughuli mbalimbali za uzalishaji mali Vijijini na Mijini na Ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kulinda mipaka ya Nchi yetu pamoja na kuimarisha Amani na Utulivu Nchini. Serikali pia, itaimarisha na kuliongezea uwezo Jeshi la Wananchi kwa kulipatia Vifaa na Zana Bora za Kisasa; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na Makazi; na kuimarisha upatikanaji wa huduma, mahitaji na Stahili kwa Wanajeshi. Aidha, itaimarisha jukumu la kulea Vijana wa Kitanzania katika Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa na kuimarisha Ushirikiano wa Kijeshi na Kiulinzi na Nchi nyingine Duniani kupitia Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na ushirikiano na Nchi moja moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kulinda Usalama wa Raia na Mali zao. Katika mwaka 2008/2009, jitihada kubwa ziliwekwa katika kuendesha Operesheni za Kudhibiti ongezeko la Ujambazi na vitendo vya uhalifu kwa kushirikiana na Wananchi. Kutokana na jitihada hizo Majambazi Sugu na Wahalifu wengi wamekamatwa. Hii imewezekana kutokana na ushirikiano wa karibu baina ya Vyombo mbalimbali vya Ulinzi na Usalama na Raia Wema kupitia dhana ya Ulinzi Shirikishi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali imeongeza Bajeti ya Jeshi la Polisi ili kuliwezesha kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu Nchini. Dhana ya Ulinzi Shirikishi wa Jamii kupitia Polisi Jamii itaimarishwa; kinachotakiwa ni kuimarisha ushirikiano na Wananchi katika kuwafichua Wahalifu tunaoishi nao, ili mafanikio tuliyoyapata yawe makubwa zaidi. *(Makofi)*

Hivyo, natoa wito kwa Watanzania wote kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kuimarisha Usalama, Utulivu na Amani katika maeneo tunayoishi. Sote tujivunie kuwa Walinzi imara wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Ajira. Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 pamoja na masuala mengine, iliahidi kupatikana kwa ajira mpya zaidi ya Milioni Moja katika kipindi cha miaka mitano. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Umma zinatekeleza Mpango wa Taifa wa Kukuza Ajira pamoja na Programu mbalimbali za Kukuza Ajira na kuwezesha Wananchi Kiuchumi. Hatua hizi zimewezesha kuongeza Ajira Nchini. Hadi kufikia Mwezi Mei 2009, Ajira mpya zaidi ya Milioni 1.3 zilipatikana Nchini.

Mheshimiwa Spika, ajira hizi ni mbali ya zile zinazotokana na Ajira Binafsi katika Kilimo, Ufugaji na Uvuvi. Aidha, ili kuendelea kuongeza Ajira zaidi, Ofisi za Mikoa na Wilaya zimeelekezwa kuunda Kamati za Kukuza Ajira na kuteua Maafisa Waratibu wa Ajira katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Kata. Naipongeza Mikoa ya Mtwara, Lindi na Morogoro kwa kuunda Kamati hizo. Natoa wito kwa Mikoa ambayo bado haijaunda Kamati hizo iongeze kasi ili iweze kukuza na kuratibu Ajira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Kazi. Serikali imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kudumisha mahusiano mema mahali pa kazi, ili kuongeza tija. Ili kutekeleza wajibu huo, Bunge limepitisha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi mwezi Novemba 2008. Sheria hii inatoa utaratibu wa ulipwaji wa fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia kazini pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Fidia. Aidha, Serikali imefanya kaguzi za kazi 277 katika maeneo mbalimbali ya kazi Nchini. Pia, imefanya utatuzi wa migogoro ya kikazi chini ya Sheria za Kazi Na. 6 na 7 za mwaka 2004, kwa mafanikio kwa kupunguza au kuondoa kero ya kulundikana kwa migogoro ya kikazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya migogoro 7,303 iliyopokelewa katika kipindi cha Julai 2008 mpaka Mei 2009, migogoro 5,220 sawa na asilimia 72 imepatiwa ufumbuzi. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imesimamia uanzishwaji wa vyombo vya Ushirikishwaji wa Wafanyakazi kwa kuunda Mabaraza ya Wafanyakazi 170 katika Taasisi za Umma na za Binafsi. Tume imeendesha mafunzo ya kujenga uelewa juu ya matumizi sahihi ya Sheria mpya ya Kazi na Kanuni zake za mwaka 2007 ikiwa ni pamoja na kutafsiri Kanuni hizo kwa Lugha ya Kiswahili. Mafunzo haya yamefanyika katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, suala la migomo ya Wafanyakazi limekuwa likijitokeza mara kwa mara katika Makampuni, Viwanda na Mashirika humu Nchini. Pamoja na kwamba Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini imetoa haki kwa Wafanyakazi kugoma, migomo inapotokea sehemu za kazi hasa zile zinazohusika na utoaji wa huduma muhimu kwa jamii, inaleta athari nyingi kwa Wananchi, kusababisha hasara kubwa kwa Taasisi husika na Uchumi wa Nchi kwa ujumla. Vyanzo vya migomo hii ni mawasiliano duni kati ya Waajiri na Waajiriwa na wakati mwingine Wafanyakazi kutofuata taratibu za Kisheria za kudai haki zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikiana na Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi kutafuta suluhisho la migogoro mbalimbali ili kuepusha migomo ambayo hatimaye huathiri huduma za kibiashara na kijamii. Nawasihi Wafanyakazi kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi pamoja na kujadiliana na Waajiri pale wanapoona haki haitendeki. Aidha, Vyama vya Wafanyakazi, pamoja na wajibu wao wa kutetea maslahi ya Wafanyakazi, vinao wajibu mkubwa wa kuepusha migomo isiyo ya lazima. Nina imani tukikaa pamoja, tukizungumza na kujadiliana hatutafikia hatua ya kugoma kwa kuwa mijadala huleta suluhisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendeleza juhudi za kudumisha mahusiano mema mahali pa kazi ikiwa ni pamoja na kutatua mapema iwezekanavyo migogoro inayoibuka sehemu za kazi. Aidha, itaendelea kuhakikisha kuwa juhudi zilizoanzishwa za kuongeza ajira nchini zinaendelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kimataifa. Katika mwaka 2008/2009, uhusiano wa Nchi yetu na Mataifa mengine Duniani pamoja na Mashirika ya Kimataifa na Kikanda umeimarika kwa kiwango kikubwa. Katika kipindi hicho, tumeshuhudia Viongozi Mashuhuri na Wakuu wa Nchi mbalimbali, wakiambatana na Wawekezaji na Wafanyabiashara kutembelea Tanzania kwa malengo mbalimbali ya kiuchumi na kuimarisha ushirikiano wetu. Maeneo ya Kipaumbele ambayo Viongozi na Wawekezaji hao wameonyesha nia na dhamira ya kukuza ushirikiano ni katika Nyanja za kilimo, elimu, utalii, viwanda, miundombinu na kukuza mauzo nje. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Tanzania ina mahusiano mazuri na Mataifa yote Duniani na Mashirika ya Kimataifa na Kikanda, ikiwemo Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kutambua juhudi kubwa zilizofanywa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Ni dhahiri alipokuwa Mwenyekiti wa Umoja huo, Mheshimiwa Rais aliwezesha Nchi yetu kung'ara katika medani za Siasa za Bara la Afrika na Mataifa mengine Duniani. Vilevile, katika kipindi chake cha Uongozi, Umoja wa Afrika ulipata mafaniko makubwa ya kushughulikia changamoto nyingi za Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii zinazolikabili Bara la Afrika katika nyanja mbalimbali, zikiwemo za Ulinzi, Usalama, Ushirikiano na Kanda nyingine pamoja na kutafuta ufumbuzi wa migogoro iliyopo katika Bara hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ambayo inasisitiza zaidi Diplomasia ya Uchumi. Aidha, uimarishaji wa Ofisi za Balozi za Tanzania zilizopo utapewa kipaumbele. Sambamba na hatua hiyo, Serikali itaangalia namna bora ya kuwawezesha Watanzania wanaoishi Ughaibuni (Diaspora) kushiriki kikamilifu katika kuchangia shughuli za Kiuchumi na Kijamii hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kutokana na mikakati ambayo Serikali ilijiwekea katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Tanzania imeendelea kunufaika kutokana na kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Biashara baina ya Nchi Wanachama imeshamiri na inaongezeka mwaka hadi mwaka. Mfano, mauzo ya bidhaa za Tanzania katika Soko la Afrika Mashariki yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani Milioni 173.1 mwaka 2007, hadi kufikia Dola za Kimarekani Milioni 315.5 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 82.3. Inatarajiwa kuwa mauzo ya bidhaa za Tanzania ndani ya Soko hili la Afrika Mashariki yataongezeka zaidi kuanzia mwezi Julai 2009 ambapo Nchi za Burundi na Rwanda zitaanza kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Spika, Nchi hizi tayari zimekubali kupunguza Ushuru wa Forodha kwa asilimia 80 kwa bidhaa kutoka Tanzania ikiwa ni hatua za utekelezaji wa Itifaki hiyo. Vilevile, ikumbukwe kuwa Nchi za Rwanda na Burundi ni Soko kubwa na muhimu kwa bidhaa nyingi kutoka Tanzania kama vile saruji, chumvi, samaki wabichi na wakavu, mpunga na mchele, kahawa, mahindi, mtama, mafuta ya mawese na nguo zitokanazo na pamba. Hivyo, natoa wito kwa Wafanyabiashara wa Tanzania kujiandaa na kuchangamkia fursa za kibiashara zinazopatikana katika Nchi hizo bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya uundaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambalo litafungua fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, itashirikiana na Wadau mbalimbali kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa na Mikakati ya kisekta ili kuhakikisha kuwa Tanzania imejipanga vizuri kunufaika ipasavyo na fursa za Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ilikamilisha Mradi Mkubwa wa Upigaji Picha za Anga kwa eneo la Hekta 276,910 la Mji Mkuu linalojumuisha eneo lote la Kiutawala la Wilaya ya Dodoma Mjini. Aidha, imekamilisha Mpango wa ujenzi wa Mji Mpya wa kisasa wa Iyumbu utakaohuisha maendeleo yote ya Kimji yanayotosheleza kasi ya kukua kwa mahitaji ya makazi na shughuli za kiuchumi na huduma za kijamii. Mamlaka pia, ilipima Viwanja 4,000 na kukamilisha uandaaji wa mipango ya uendelezaji yenye jumla ya Viwanja vya Makazi na shughuli nyingine vipatavyo 20,000. Viwanja hivyo vitapimwa katika maeneo ya Ntyuka, Mkonze, Nzuguni, Ndachi, Msalato na Kiterera.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu itaanza mapitio ya Mpango Kabambe wa Mji wa Dodoma ili kuurekebisha na kuufanya uendane na mabadiliko makubwa yaliyopo pamoja na mahitaji ya ukuaji wa Mji. Aidha, itapima Viwanja katika maeneo mbalimbali ambayo yamekwisha tayarishiwa Michoro ya Viwanja, kujenga Miundombinu katika maeneo ya Ipagala, Area E, Chang’ombe, Mwangaza na Ilazo. Pia, itaanza ujenzi wa Awamu ya Kwanza ya Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Katika mwaka 2008/2009, Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali ilichapisha kwa wakati Nyaraka na Hotuba za Bunge la Bajeti za mwaka 2008/2009, Chaguzi Ndogo za Wabunge na Madiwani na Nyaraka nyingine za uendeshaji wa shughuli za Serikali. Ili kuongeza ufanisi, Serikali imenunua mtambo mpya wa kisasa utakaosaidia katika kuboresha kazi za uchapaji wa Nyaraka za Serikali. Lengo ni kuhakikisha kwamba Nyaraka zote za Serikali zinachapishwa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Katika mwaka 2009/2010, Idara itakuwa na jukumu kubwa la kuchapisha Nyaraka za Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Ninapenda kuwahimiza Watendaji Wakuu wote Serikalini kuhakikisha kuwa wanatumia ipasavyo Idara hiyo katika uchapishaji wa Nyaraka za Serikali ili kudhibiti uvujaji siri wa Nyaraka na maamuzi mbalimbali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Masuala mtambuka. Ushiriki wa Wanawake katika Uongozi. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, imeweka malengo ya kuondolewa kwa ubaguzi wa aina yoyote wa jinsia katika uongozi na utoaji maamuzi. Ili kufikia malengo hayo, Serikali imeandaa mkakati wa kuwajengea uwezo na kuwapatia fursa Wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za uongozi. Aidha, Serikali imeendelea kuingiza masuala ya jinsia kwenye Sera, Mipango na Bajeti. Vilevile, imetoa mafunzo ya uelewa wa masuala ya Jinsia kwa Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kukamilisha Mkakati wa kuongeza ushiriki wa Wanawake kufikia asilimia 50 katika Uongozi na maamuzi, pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa UKIMWI. UKIMWI umeendelea kuwa tishio la Taifa na madhara yake yataendelea kuathiri Uchumi wa Nchi. Jitihada za kupunguza maambukizi mapya na kuwepo kwa mpango wa matunzo na matibabu kwa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI yamechangia katika kupunguza kasi ya madhara ya UKIMWI Nchini. Hata hivyo, Watanzania takriban Milioni 2 wanaishi na Virusi vya UKIMWI na bado maambukizi mapya yanaongezeka. Idadi hii bado ni kubwa na ni changamoto kwetu sote; hivyo jitihada za dhati zinahitajika kutoka katika Sekta zote na Wananchi wote ili kudhibiti maambukizi mapya na kuhakikisha kwamba huduma zaidi zinapatikana kwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea kuwezesha Sekta mbalimbali kifedha na kitaalamu katika kupanga na kutekeleza afua za kuthibiti UKIMWI sehemu za kazi. Aidha, ilifanya mapitio ya Mkakati wa kwanza wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI na kuandaa Mkakati wa Pili wa mwaka 2008 – 2012. Mkakati huo umetoa mwongozo wa maeneo ya kipaumbele katika kudhibiti UKIMWI. Eneo mojawapo ni kuongeza juhudi za kupunguza maambukizi mapya hasa kwa kuwalenga Vijana wa miaka 15 – 24. Eneo lingine ni kuhakikisha Watanzania wote wanapata elimu kuhusu kuzuia maambukizi mapya, matunzo na matibabu. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itapitia upya Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001, kusambaza kwa Wadau mbalimbali Mkakati Mpya wa Kudhibiti UKIMWI, na Matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya Rushwa. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kupambana na Rushwa kubwa na ndogo hapa Nchini. Katika kutimiza azma hiyo, Taasisi imeendesha tafiti 10 ndogo za kubaini mianya ya rushwa katika ngazi za Mikoa na kutoa mapendekezo Serikalini.

Vilevile, imefanya uchunguzi kuhusu Rushwa Kubwa zilizoripotiwa na kuwasilisha mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi. Aidha, Taarifa 1,338 za Rushwa kutoka kwa Wananchi zimepokelewa na kufanyiwa kazi ambapo jumla ya kesi 321 ziliendeshwa Mahakamani. Katika mwaka 2009/2010, Taasisi itaendelea kufanya utafiti na uchunguzi ili kubaini Mianya ya Rushwa Kubwa na Ndogo na kutoa elimu juu ya Mapambano Dhidi ya Rushwa. Aidha, itawafungulia mashtaka wote wanaobainika kujihusisha na vitendo vya Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Mazingira. Tafiti na Taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na kasi ya ongezeko la Joto Duniani. Kutokana na hali hii, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Serikali imeendelea kutekeleza Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi kwa kuelimisha na kuhamasisha Wananchi kuhusu athari za mabadiliko ya Tabianchi na changamoto za kukabiliana nazo. Mafunzo kwa Wananchi na Watendaji yameendeshwa katika Mikoa ya Iringa, Tanga na Pwani kuhusu mabadiliko ya Tabianchi pamoja na nafasi ya Ushiriki wa Wananchi katika shughuli za Upandaji Miti ambazo zinaweza kuwaongezea kipato kupitia biashara ya hewa mkaa. Maeneo ya Kipaumbele

yamebainishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya kupunguza utoaji wa Gesijoto utokanao na Ukataji na Uharibifu wa Misitu. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kuratibu shughuli zote zinazohusu mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Maafa. Katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea kuelimisha Jamii kuhusu mbinu za kukabili Maafa, kutathmini maeneo ya Maafa Nchini na kuijengea uwezo Idara ya Maafa. Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ilifanya tathmini ya kina ya Hali ya Chakula Nchini na kubaini kuwa, baadhi ya maeneo yameathirika kwa ukame na hivyo kusababisha upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wilaya 36 katika Mikoa 12 zimeathirika kwa ukame. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Pwani, Mwanza, Dodoma, Lindi, Tanga, Manyara, Morogoro, Mara, Mtwara na Iringa. Katika kukabiliana na hali hii, Serikali ilitoa jumla ya Tani 28,684 za mahindi kwa Walengwa. Aidha, ilitoa jumla Shilingi Bilioni 1.8 kwa ajili ya kununua mbegu za mahindi na mtama kwa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mwanza Dodoma, Lindi, Tanga, Manyara, Morogoro, Mara, Mtwara, Shinyanga na Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba 2008 hadi Mei 2009, Nchi yetu imekumbwa na Maafa mengine yakiwemo kuporomoka kwa Machimbo ya Madini katika Kijiji cha Mugusu (Geita), ambapo zaidi ya Watu Sita wanahofiwa Kufa. Maafa mengine ni Ajali ya Treni Dodoma iliyosababisha Vifo vya Watu Saba na yale yaliyotokea katika Ukumbi wa Starehe tarehe 1 Oktoba, 2008 Mjini Tabora ambapo Watoto 19 walipoteza maisha na wengine 16 walinusurika katika tukio hilo. Aidha, hivi karibuni kulitokea Ajali za kuzama kwa Boti huko Tanga na Meli Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ajali za Barabarani zimeendelea kupoteza nguvu kazi kutokana na Vifo na kuongeza idadi ya Walemavu. Kwa mfano, kati ya kipindi cha Januari hadi Aprili 2009, jumla ya ajali 6,647 ziliripotiwa Nchini kote ikilinganishwa na 5,111 kipindi kama hicho mwaka 2008. Kati ya Ajali hizo, Ajali 880 zilisababisha Vifo vya Watu 1,190. Hizi ni Ajali na Vifo vingi ambavyo vingeweza kuepukika kama Madereva, Abiria, Watembea kwa miguu na Askari wa Usalama Barabarani wangetimiza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Maafa mengine ni yale ya Mlipuko wa Mabomu yaliyotokea tarehe 29 Aprili, 2009, katika Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) iliyopo Mbagala, Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika tukio hilo madhara makubwa yalitokea na kusababisha Watu 26 kupoteza Maisha, ambapo Raia walikuwa 20 na Askari wa JWTZ ni Sita. Watu 338 walijeruhiwa. Serikali iliunda Kamati Maalum ya Wataalam kufanya tathmini ya nyumba zilizoharibika. Taarifa ya tathmini inaonyesha kuwa jumla ya nyumba 9,049

zimeharibika. Kati ya hizo, nyumba zipatazo 286 zilibomoka kabisa na zilizobaki 8,763 zimeezuliwa paa, kuvunjika au kupata nyufa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imechukua hatua za kuwapatia Waathirika Misaada ya Chakula, Mahema na Vifaa vya Nyumbani. Aidha, Serikali inaandaa utaratibu wa kuwalipa fidia Waathirika wa maafa hayo. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wote waliotoa Misaada ya Hali na Mali katika kuwasaidia Walioathirika. Aidha, nawapa pole wale wote waliopoteza Ndugu na Jamaa zao katika Matukio hayo na Mwenyezi Mungu Azilaze Roho za Marehemu Mahali Pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kuijengea uwezo Idara ya Maafa ili iweze Kuratibu na Kujenga uwezo wa Wadau mbalimbali katika kukabili Maafa Nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuiwezesha Idara hiyo kutoa Elimu kwa Jamii juu ya Mbinu za Kujikinga na Maafa kupitia Vyombo vya Habari na kutoa mafunzo kwa Kamati za Maafa za Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mauaji ya Walemavu wa Ngozi. Kwa takriban miaka miwili kuanzia mwezi Juni 2007, Nchi yetu imeshuhudia kuibuka kwa wimbi kubwa na kushamiri kwa Mauaji ya kutisha ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi, yaani Albino. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa linachochewa na Imani za Kishirikina na udanganyifu kwamba Viungo vya Mlemavu wa Ngozi ni Dawa ya kusaidia kuleta Utajiri wa haraka haraka, hasa kwa Watu wachache wenye tamaa ya fedha wanaojishughulisha na biashara na Uchimbaji wa Madini na Uvuvi wa Samaki.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imechukua hatua mbalimbali ili kwa pamoja kuweza kupata njia sahihi ya kukabiliana na Ukatili dhidi ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi. Serikali imefanya Sensa ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi Nchini ili kuwatambua pamoja na kuendesha zoezi la Upigaji Kura dhidi ya Wahalifu na Wanaojishughulisha na Mauaji hayo. Uchambuzi na uhakiki wa waliotajwa katika zoezi hilo unafanywa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Watuhumiwa katika baadhi ya Mikoa wamepelekwa Mahakamani na kesi zimeanza kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Dawa za Kulevya. Nchi yetu bado inakabiliwa na tatizo la matumizi na biashara haramu ya Dawa za Kulevya. Hali hii inatishia Ustawi na Usalama wa Taifa letu. Tatizo hili linadhihirishwa na takwimu za watumiaji wa Dawa za Kulevya waliojitokeza kwenye Hospitali na Vituo vya Tiba pamoja na zile za ukamataji wa Dawa za Kulevya na uteketezaji wa Mashamba ya Bangi. Kwa mfano, mwaka 2007/2008 Waathirika wa Dawa hizo wapatao 4,723 walipata tiba. Halikadhalika, mwaka 2008 Tani 76 za Bangi zilikamatwa ikilinganishwa na Tani 59 zilizokamatwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2008, jumla ya Ekari 72 za Mashamba ya Bangi ziliteketezwa. Ukamataji wa Dawa za Kulevya aina ya *Heroin* na *Cocaine* ulipungua kwa mwaka 2008 ambapo jumla ya Kilo 7 zilikamatwa ikilinganishwa na jumla ya Kilo 22.8 za Dawa hizo zilizokamatwa mwaka 2007. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2008 Watanzania wapatao 103 walikamatwa Nje ya Nchi kwa kujihusisha na Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya, jambo ambalo linaleta taswira mbaya ya Nchi yetu kwa Jamii na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kupambana na tatizo hili la Dawa za Kulevya. Hatua hizo ni pamoja na uelimishaji kwenye Maonyesho na katika Matukio mbalimbali ya Kitaifa na Vyombo vya Habari kama vile Redio, Televisheni, Magazeti pamoja na Machapisho mbalimbali. Aidha, Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo inatoa Mwongozo wa namna ya Kudhibiti Matumizi na Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kuelimisha Umma kuhusu madhara ya Dawa za Kulevya. Aidha, itaongeza uwezo wa Idara na Wakala wa Serikali katika kusimamia Mipaka, Bandari na Viwanja vya Ndege ili visitumike kupitishia Dawa Haramu za Kulevya. Pia, Serikali itaendelea kusimamia na kuendesha Operesheni Maalum za kuwabaini na kuwakamata Wafanyabiashara wa Dawa za Kulevya Nchini pamoja na kuteketeza Mashamba ya Bangi. Kutokana na matumizi ya Dawa za Kulevya kuchochea Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Serikali itaendelea kutekeleza Mikakati ya Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI miongoni mwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya.

Hata hivyo, ningependa kusisitiza kuwa, wajibu mkubwa wa kupambana na utumiaji wa Dawa za Kulevya upo kwa Wazazi na Walezi ambao wanawajibika kuwaelimisha na kufuatilia kwa karibu tabia za Watoto kabla hawajaingia katika mtego wa kutumia Dawa hizo. Wazazi na Walezi wawe karibu na Watoto wao. Tusiwaache Watoto walelewe na Televisheni na *Internet*.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nimeelezea kwa muhtasari shughuli mbalimbali ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, na pia nimetoa mwelekeo wa kazi zitakazofanyika katika mwaka 2009/2010. Katika kuhitimisha Hotuba hii ningependa kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:

(a) Sote tunatambua kuwa mwaka wa fedha ujao ni wa mwisho kabla ya kuelekea kwenye kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Hivyo, tunahitaji ushirikiano mkubwa na Wadau wote wa Maendeleo na Wananchi kwa ujumla ili kutekeleza kwa dhati na kwa makini Kazi za Serikali zilizopangwa na hatimaye tuweze kuhitimisha utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala na yale ya MKUKUTA. Nawaombeni tudumishe Utulivu, Amani na Mshikamano wetu. Demokrasia pana na Uhuru wa kuzungumza uliopo usitumike vibaya

na wachache wetu. Tuendelee kudumisha Umoja wetu kama Taifa wakati huu wa kuelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na kujiandaa kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

(b) Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi ya kweli katika Sekta ya Kilimo. Hivyo, tunayo kazi kubwa mbele yetu ya kuwahamasisha Wananchi kuzingatia Kanuni bora za Kilimo na kutumia zana bora na mbolea ili wazalishe kwa tija na kuongeza uzalishaji kuwezesha Taifa letu kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada. Natoa rai kwamba ni wajibu wa kila mmoja wetu kuchangia kwa nguvu zote jitihada hizi ili kufanikisha azma yetu ya kuleta Mapinduzi katika Kilimo. Kauli Mbiu yetu na Wimbo wetu sasa uwe ni "KILIMO KWANZA". Kipaumbele chetu cha kwanza kiwe ni Kilimo. Kipaumbele chetu cha Pili ni Kilimo na Kipaumbele chetu cha Tatu kiwe ni Kilimo. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kufikia lengo la Maisha Bora kwa kila Mtanzania.

(c) Serikali itaendelea kudhibiti matumizi ya fedha yasiyo ya lazima katika baadhi ya maeneo ili kuweka nguvu zetu katika Kilimo, hususan cha Umwagiliaji. Makongamano, Warsha na Semina zisizo na tija zitaendelea kusitishwa pamoja na ununuzi wa magari ya kifahari ili fedha hizo zielekezwe kwenye Kilimo. Natoa wito kwa Viongozi katika ngazi zote, Wadau wetu wa Maendeleo na Wananchi wote tushirikiane kuisaidia Serikali kutoa msukumo katika Kilimo. Napenda kusisitiza kuwa Viongozi wa Mikoa na Halmashauri wana wajibu mkubwa kuwasaidia Wananchi kuibua Miradi bora ya Kilimo, na kutafuta vyanzo zaidi vya fedha za kununulia pembejeo hasa Matrekta na Vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ili kuongeza tija na uzalishaji katika Kilimo.

(d) Serikali inathamini na kuheshimu mchango wa Wakulima na Wafugaji na inaheshimu haki zao. Tushirikiane na Serikali katika juhudi zinazofanywa za kutenga maeneo kwa ajili ya Malisho ya Mifugo na ya Wakulima. Wakulima na Wafugaji wote Nchini waheshimu Haki na Mipaka ya kila mmoja ili waendelee kuishi kwa amani na kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kwa uhakika.

(e) Ili kufanikisha utekelezaji wa Majukumu na Kazi za Serikali zilizopangwa kwa mwaka 2009/2010 na kutoa huduma bora kwa Wananchi ni muhimu Watumishi wote wa Serikali wawajibike ipasavyo katika kuwatumikia Wananchi na kuondoa Kero zinazowakabili. Nahimiza Watumishi wote kuzingatia Maadili ya Kazi, Kanuni na Sheria pamoja na kufanya Kazi kwa Bidii na Ubunifu na kuepuka vitendo vya Rushwa. Watumishi wa Umma wasio Waaminifu na Wababaishaji wabanwe na kuchukuliwa hatua za Kinidhamu.

(f) Pamoja na Msukosuko wa Masoko ya Kifedha na kuyumba kwa Uchumi Duniani, bado tunazo fursa nyingi za kukuza Uchumi wetu kwa kuongeza uzalishaji na pia zipo fursa za kufanya hivyo kupitia Medani ya Ushirikiano wa Kimataifa. Tunazo bidhaa nyingi zinazoweza kupenya na kushindanishwa katika Masoko ya Kimataifa, Masoko ya Kikanda na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Nawasihi Wananchi wetu

tutumie fursa hizi vizuri kwa kujiandaa vyema na kushiriki katika biashara za Kimataifa na kuhamasisha Utalii na fursa nyingine za Kiuchumi ili tuiingizie Nchi yetu Pato kubwa zaidi na kuondoa Umaskini kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu, nimwombe Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atoe maelezo ya Mapitio ya Kazi Zilizofanyika katika mwaka 2008/2009 na Mwelekeo wa Kazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2009/2010. Ni matumaini yangu kwamba maelezo hayo yatawezesha Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kufahamu kwa upana shughuli zinazotekelezwa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya awali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa hatua hiyo ya awali. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwamba kwa mujibu wa Kanuni, ana dakika 45 za kuwasilisha hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyotoa mwelekeo na malengo ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2009/2010. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake kuhusu hali ya uchumi na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010. Hotuba zake zimeweka misingi ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa ujumla kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kuwasilisha maelezo ya kiutendaji ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwaka 2008/2009 na mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2009/2010 – 2011/2012 yamezingatia malengo yaliyomo katika Mipango Mikakati, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini pamoja na ahadi mbalimbali za Viongozi. Aidha, maelekezo ya mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2009/2010 – 2011/2012 yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Bajeti unasisitiza kuwa Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zipange mipango yao kwa kuzingatia vipaumbele na hasa majukumu ya msingi (*Core business*) yaliyoainishwa kwenye Mipango Mikakati yao. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina vipaumbele vingi. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti, fedha nyingi zimetengwa kwenye vipaumbele muhimu kitaifa na vilivyoibuliwa na wananchi kwa kutumia mbinu shirikishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kueleza majukumu ya kisera na ya kiutendaji kama ifuatavyo:-

(a) Majukumu ya Kisera

(i) Kuendeleza umoja na mshikamano wa Kitaifa;

(ii) Kuendeleza hali ya amani na utulivu nchini;

(iii) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla;

(iv) Kusimamia maendeleo ya kijamii hususan elimu, afya, maji na barabara;

(v) Kujenga na kuimarisha demokrasia na utawala bora.

(b) Majukumu ya Kiutendaji

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kisera kama yalivyoainishwa hapo juu, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itatekeleza majukumu ya kiutendaji kama ifuatavyo:-

(i) Kujenga uwezo wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI wa kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza wajibu wake;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini na Mikakati yake;

(iv) Kuendeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa nchini ili kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma bora kwa Wananchi;

(v) Kuzijengea Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato na matumizi;

(vi) Kuboresha miundo na taaluma ya watumishi na mifumo ya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vii) Kusimamia Taasisi, Mashirika ya Umma na Miradi inayotekelezwa chini ya Waziri Mkuu – TAMISEMI;

(viii) Kuratibu shughuli za hifadhi ya mazingira;

(ix) Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya UKIMWI na VVU; na

(x) Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekabidhiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Majukumu ya Mikoa

(i) Kuzijengea Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

(ii) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iii) Kuhakikisha kunakuwepo amani na utulivu katika Mikoa;

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na maagizo ya Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Kijamii, Kiuchumi na Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora;

(vii) Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya UKIMWI na VVU; na

(viii) Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya Rushwa.

(b) Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI

(i) Kuendesha vikao vya kisheria katika ngazi zote za Serikali za Mitaa ili kuimarisha na kuendeleza demokrasia;

(ii) Kuhimiza na kuendeleza sekta ya kilimo hasa upatikanaji wa pembejeo na zana bora za kilimo;

(iii) Kuendeleza sekta ya elimu hususan majukumu mapya ya elimu ya sekondari;

(iv) Kuendesha Uchaguzi wa Viongozi wa Ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kukarabati na kujenga ofisi katika ngazi zote za Serikali za Mitaa;

(vi) Kushughulikia masuala ya maafa na usimamizi wa mazingira;

(vii) Kujenga uwezo wa Watendaji ngazi za msingi ili kusimamia rasilimali za umma kwa ufanisi;

(viii) Kuwashirikisha wananchi katika kupanga, kufuatilia na kutekeleza Mipango ya Maendeleo katika maeneo yao;

(ix) Ununuzi wa nyenzo za kufanyia kazi kama magari ya zimamoto, wagonjwa, taka na ya utawala;

(x) Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI na VVU;

(xi) Kuboresha Mikataba ya Huduma kwa Wateja;

(xii) Kuboresha miundombinu ya barabara;

(xiii) Kuboresha huduma za afya kwa wananchi;

(xiv) Kuwajengea uwezo watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo mbalimbali;

(xv) Kuimarisha na kubuni vyanzo vya mapato ya Halmashauri ambavyo ni vya uhakika; na

(xvi) Kuanza maandalizi ya mradi wa Mkakati wa kuendeleza Miji - Tanzania *Strategic Cities Project.*

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa Madaraka kwa Umma chimbuko lake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 8, 145 na 146. Utekelezaji wake unafafanuliwa kwa kina zaidi na Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1998. Katika Sera hii madaraka ya kisiasa, majukumu, rasilimali fedha na rasilimali watu vinagatuliwa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako ndiko utekelezaji wa Sera na Mipango ya Kitaifa unafanyika. Utekelezaji wa programu hii ulianza tangu mwaka 1998 hadi 2008 na imekuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuimarika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama chombo cha kupeleka madaraka kwa wananchi na kuinua uelewa wa misingi ya Utawala Bora miongoni mwa wananchi;

(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa kutambua umuhimu wa kuwajibika kwa wananchi na kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii;

(iii) Kuongezeka kwa ruzuku inayopelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iv) Viongozi wa kisiasa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuelewa majukumu na mipaka ya madaraka yao; na

(v) Kuongezeka kwa ari ya wananchi kushiriki katika kutekeleza shughuli za maendeleo ambapo sasa wananchi wanajitolea kwa mfano, kujenga barabara, zahanati, shule za Msingi na Sekondari. Aidha, kuunda kamati za kufuatilia wakisubiri nguvu ya Serikali kuwasaidia kufanikisha miradi waliyoibua wao wenyewe; na Kuboreshwa kwa utunzaji wa vitabu vya hesabu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, shughuli zilizotekelezwa chini ya Programu ni kukamilisha kazi ambazo hazikukamilika katika Awamu ya Kwanza ya Programu ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuendesha mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa 4,333;

(ii) Kukamilisha andiko la Awamu ya Pili ya Programu;

(iii) Kuwashawishi Wabia wa Maendeleo ili watoe mihadi ya kuchangia Awamu ya Pili ya Programu; na

(iv) Kufungamanisha utekelezaji na uratibu wa programu katika Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na katika Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ambayo itatekelezwa katika kipindi cha 2009 -2013, imeandaliwa kwa kuzingatia changamoto pamoja na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Kwanza. Mambo yatakayotekelezwa katika Programu hii yamegawanyika katika maeneo manne.

Kwanza; Kujenga mazingira ambayo yatawezesha Serikali kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kupeleka madaraka kwa wananchi.

Pili; Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan ngazi za msingi wa kutekeleza majukumu yake katika maeneo yafuatayo:- Uongozi na Menejimenti; Maendeleo ya Watumishi kitaaluma na kitaalam; Ukusanyaji, usimamizi na matumizi bora ya mapato; Uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ya utekelezaji na Matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Tatu; Kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika kupambana na umaskini. Katika eneo hili wananchi watawezeshwa kutumia Mbinu Shirikishi ya Fursa na Vikwazo vya Maendeleo, (O & OD) katika kupanga na kutekeleza miradi yao.

Nne; Kujenga uwezo wa kitaasisi wa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu katika ngazi zote Serikalini. Katika eneo hili yafuatayo yatatekelezwa:- Kujenga uwezo wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Wizara nyingine, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na ngazi za msingi hususan ngazi za Kijiji na Mtaa. Halikadhalika kuweka Mfumo imara wa Ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kusimamia utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya dhana ya upelekaji wa Madaraka kwa Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Sera ya Ajira na Menejimenti katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na Sheria ya Utumishi wa Umma na. 8 ya 2002 ni mamlaka za ajira na nidhamu kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibika pia kuwaendeleza watumishi wake ili watoe huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo Wizara za Kisekta zikiratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI zina wajibu wa kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zina watumishi wenye sifa za kitaaluma na uzoefu ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.Hadi kufikia mwezi Machi 2009, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na Watumishi 238,107 wanaolipwa mishahara kupitia *Computer Payroll* ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imefanya jitihada zilizolenga kuziwezesha Halmashauri kuwa na watumishi wenye sifa na wa kutosha ili kuimarisha utumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2008/09, watumishi wafuatao wamepangiwa kazi moja kwa moja kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa:

| | |
|---|---|
| Afya | 2,380 |
| Kilimo | 856 |
| Mifugo | 168 |
| Uhasibu na Ukaguzi | 200 |

Aidha, Halmashauri zimejaza nafasi 1005 za Wakuu wa Idara kufikia mwezi Februari, 2009 ambayo ni wastani wa asilimia 76 ya nafasi zote katika Halmashauri 133. Kati ya Wakuu wa Idara hao, 125 ni wanawake. Katika kipindi cha mwaka 2008/09 Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 zimechukua hatua za kinidhamu kwa watumishi 73. Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa 36 zimewafikisha Mahakamani watumishi 66 kwa tuhuma za makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Katika kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora Nchini, Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Viongozi wa ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa utafanyika Oktoba, 2009. Ili kufanikisha uchaguzi huu, maandalizi mbalimbali yamefanyika ikiwa ni pamoja na Mikutano ya wadau kama vile Vyama vya Siasa na Asasi za Kiraia.

Mikutano hiyo imewezesha kupata maoni ya kuboresha Kanuni na Taratibu za kuendesha Uchaguzi huo. Kazi nyingine zilizofanyika ni kuandaa Orodha ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa ambayo itachapishwa kwenye Gazeti la Serikali (GN) kwa ajili ya Uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa hadi Oktoba 2009 kazi zitakazofanyika ni kusambaza Kanuni za Uchaguzi na Fomu mbalimbali za wagombea, kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kununua masanduku mapya ya kupigia kura na kusafirisha vifaa vya uchaguzi. Vile vile, kuandikisha wapiga kura, kutoa mafunzo kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi na mwisho kufanya Uchaguzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Utendaji wa Madiwani. Serikali inatambua mchango wa Waheshimiwa Madiwani katika utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Maendeleo katika maeneo yao. Kama ilivyoelezwa katika bajeti ya mwaka 2008/2009 katika Bunge lako Tukufu, Serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya utendaji wa Madiwani ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Sheria ya Bima ya Afya ilifanyiwa marekebisho ambapo sasa imewajumuisha Waheshimiwa Madiwani katika Mpango wa Bima ya Afya. Huduma hii inatarajiwa kuanza Julai 2009. Aidha, posho mbalimbali za Madiwani zimerekebishwa na hivi sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kuwawezesha kupata unafuu wa kodi wanaponunua vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Kwa kuzingatia Dhana ya upelekaji Madaraka kwa Umma, jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu ya sekondari limehamishiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutokana na jukumu hili kuhamia kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, muundo wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI unafanyiwa marekebisho ili kuanzisha Idara ya Uratibu wa Elimu itakayoratibu na kusimamia jukumu hili ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mikoa. Kutokana na jukumu jipya la uratibu wa Elimu ya Sekondari muundo wa Sekretarieti za Mikoa unaangaliwa upya sambamba na muundo wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili kuanzisha seksheni itakayoratibu na kusimamia jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa. Muundo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pia umefanyiwa marekebisho kwa kuongeza Idara ya Elimu ya

Sekondari. Lengo la kuanzisha Idara hii ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma ya elimu ya sekondari kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Maeneo Mapya ya Utawala. Serikali imekuwa ikipokea maombi ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala ikiwemo Mikoa, Wilaya, Tarafa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Mei 2009, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imepokea maombi matano (5) ya Mikoa, 58 ya Wilaya, 24 ya Tarafa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 83 zimewasilisha maombi 575 ya kuanzisha Kata mpya. Aidha, maombi yapatayo 1,469 ya kuanzisha Vijiji vipya kutoka Mamlaka za Wilaya 69 na maombi 685 ya kuanzisha Mitaa mipya kutoka Mamlaka za Miji 11 yamepokelewa. Uchambuzi wa maombi ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji umekamilika na sasa viko kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukarabati na ujenzi wa Hospitali za Mikoa. Serikali imeendelea kufanyia ukarabati Hospitali za Mikoa nchini kwa lengo la kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya. Kazi za ukarabati zilizokua zimepangwa katika hospitali 11 zimeanza na nyingine zimekamilika. Mikoa hiyo ni pamoja na Tabora, Lindi, Dodoma, Kigoma, Shinyanga, Singida, Rukwa, Mara, Iringa, Ruvuma na Tanga. Ukarabati huo ulianza mwaka 2007/2008 na karibu hospitali zote ukarabati huo umekamilika. Aidha ujenzi wa Hospitali mpya ya Singida, Manyara na Mbeya utaendelea kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na kwa mwaka 2009/2010 Hospitali za Mikoa ya Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza na Ruvuma, zitakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) katika Kutekeleza Shughuli za Serikali. Upatikanaji wa taarifa sahihi na takwimu zenye uhakika ni kichocheo muhimu katika upangaji mipango ya maendeleo. Serikali ilipitisha Sera ya Matumizi ya TEKNOHAMA mwaka 2003 iliyoelekeza uboreshaji wa shughuli za Serikali kwa kutumia TEKNOHAMA.

Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 katika ibara ya 46 ilielekeza kuongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika kutekeleza agizo hilo, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imeanza kuweka na kuboresha Mifumo ya Habari ya Menejimenti ili wadau waweze kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mifumo ya Habari ya Menejimenti inaboreshwa kuwezesha matumizi ya kisasa ya teknolojia ya kompyuta katika mipango, ufuatiliaji, tathmini, kupashana habari, taarifa na utoaji huduma. Aidha, Wadau watapata nafasi ya kufahamu masuala mbalimbali ya kisera na maelekezo yanayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alizindua rasmi tovuti za Mikoa akiwa Mkoani Kilimanjaro tarehe 18 Machi 2009. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa tovuti za Mikoa yote 21 ziko hewani na tutaendelea kuziboresha na kuweka taarifa za vivutio vya Mikoa husika. Tovuti hizi zitakapoimarika tutaweza kupata taarifa mbalimbali za Fedha na Bajeti, Mipango, Kilimo na Mifugo, Maliasili na Mazingira, Elimu, Afya, Maji, Ushirika na Biashara. Aidha, mfumo wa kielektroniki wa kuharakisha uandaaji wa Sheria Ndogo umesimikwa ambao hatimaye utatumiwa na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Kwa kuanzia majaribio yamefanyika katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma na utazinduliwa wakati wa kilele cha Sikukuu ya Serikali za Mitaa ambazo mwaka huu zitafanyika huko Musoma.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mtiririko wa mapato ya miaka mitatu unaonyesha mwenendo wa ongezeko la ukusanyaji wa mapato kutoka shilingi bilioni 49.3 mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi bilioni 79.8 mwaka 2007/2008 ikiwa ni ongezeko la asilimia 61.8. Kwa mwaka 2008/2009, hadi kufikia Machi 2009 jumla ya shilingi bilioni 75.3 zimekusanywa sawa na asilimia 68.9 ya makadirio ya mwaka 2008/2009 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 109.8. Kwa mwaka 2009/2010 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekadiria kukusanya kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, jumla ya shilingi bilioni 138.1. Pamoja na ongezeko hilo la mapato, bado Halmashauri hazijakusanya mapato ipasavyo katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kodi ya majengo;

(ii) Ushuru wa Huduma;

(iii) Ushuru wa Mazao;

(iv) Ushuru wa Hoteli; na

(v) Mabango na Matangazo.

Mheshimiwa Spika, upo upungufu katika mikataba inayoingiwa kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mawakala wa ukusanyaji wa mapato. Serikali inaangalia kwa kina eneo hili ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata mapato zaidi kwa kusimamia makusanyo na mikataba kwa ufanisi zaidi. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imeziagiza Halmashauri kufanya utafiti wa kina ili kupata kiasi kinachopaswa kukusanywa kabla ya kuwekeana mikataba na Mawakala. Hata hivyo kwa kuzingatia wajibu wa Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi tunatoa mafunzo kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa wanaoshughulikia mapato ili kuwaongezea ujuzi wa kukusanya na kusimamia mapato.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hali ya usimamizi na utunzaji wa vitabu vya hesabu za fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuwa ya kuridhisha. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati safi mwaka 2004/2005 zilikuwa 62 kati ya 117, mwaka 2005/2006 zilikuwa 52 kati ya 124, mwaka 2006/2007 zilikuwa 100 kati ya 124 na mwaka 2007/2008 zilikuwa 72 kati ya 133. Vile vile, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati isiyoridhisha ziliendelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 zilikuwa 20, mwaka 2005/2006 zilikuwa 4, mwaka 2006/2007 na 2007/2008 hakuna Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyopata hati isiyoridhisha. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati za kutoridhisha zimeendelea kujengewa uwezo ili kuimarisha utunzaji wa vitabu vya fedha. Changamoto iliyobaki ni kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Upimaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kupata Ruzuku ya Maendeleo. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imekuwa na utaratibu wa kuzifanyia upimaji Mamlaka za Serikali za Mitaa, ili kubaini iwapo masuala ya Utawala Bora na hali ya utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa vinazingatiwa. Matokeo ya upimaji huu yamekuwa ya kuridhisha na idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazofuzu vigezo vya upimaji imekuwa ikiongezeka.

Mwaka 2006/2007 jumla ya Halmashauri 121 zilipimwa ili kufuzu kupata ruzuku ya maendeleo. Halmashauri 84 sawa na asilimia 69.4 zilifuzu. Mwaka 2007/2008 Halmashauri 121 zilipimwa ambapo Halmashauri 109 sawa na asilimia 90.1 zilifuzu. Aidha, kwa mwaka 2008/2009 Halmashauri 132 zilipimwa na Halmashauri 127 sawa na asilimia 96.2 zilifuzu. Kwa mwaka 2009/2010 Halmashauri 132 zilipimwa ambapo Halmashauri 129 sawa na asilimia 97.7 zimefuzu. Athari za kushindwa kufuzu vigezo vya upimaji vilivyowekwa ni kupata Ruzuku ya Maendeleo chini ya kiwango kilichokusudiwa.

Hata hivyo, uko utaratibu wa kufanya ufuatiliaji katika Halmashauri zinazofanya vibaya ili kuzipa maelekezo na kuzijengea uwezo. Changamoto kwa wadau wote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa katika maeneo yao ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha inayotumika.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Matumizi ya Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali inaendelea kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo, kuajiri Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani na kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Aidha, Kamati za Ukaguzi zinazojumuisha wajumbe kutoka nje ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kama Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Umeme Tanzania, Shirika la Posta, Benki na Taasisi nyingine

zimeanzishwa. Hadi sasa kuna Mamlaka za Serikali za Mitaa 85 zinazotumia mfumo wa *Epicor* na Mamlaka za Serikali za Mitaa 48 zitaingizwa kwenye mfumo huo mwaka 2009/2010 na 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa Awamu ya Pili, inapitia upya Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa *(Local Authority Financial Memorandum - LAFM)* na Mwongozo wa Fedha za Serikali za Mitaa (*Local Authority Accounting Manual - LAAM*) ili zilingane na mifumo ya kisasa ya utunzaji na utayarishaji wa taarifa za fedha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini umeweka mifumo mbalimbali ya ukaguzi wa fedha kuanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Taifa. Kwenye ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ukaguzi hufanywa na Menejimenti zenyewe ikiwa ni pamoja na Mkaguzi wa Ndani, Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri. Katika ngazi za Mkoa timu ya wataalam hufanya ukaguzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Vilevile, katika ngazi ya Wizara chini ya Idara ya Serikali za Mitaa kipo Kitengo cha Ukaguzi ambacho kwa kusaidiana na timu za Mikoa hufanya ukaguzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika ngazi ya Taifa, ukaguzi wa hesabu za Serikali za Mitaa hufanywa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Kwa hiyo uwazi na uwajibikaji kwa kiasi kikubwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeimarika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Maeneo yenye Mazingira Magumu. Kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa inatafuta utaratibu ambao unaweza kusaidia kupunguza matatizo yanayojitokeza katika maeneo yenye mazingira magumu. Kwa kuanzia Mamlaka za Serikali za Mitaa 36 zimeainishwa na zimeonekana zipo katika mazingira magumu zaidi. Mazingira hayo ni pamoja na matatizo ya miundombinu, mawasiliano, huduma za kiutumishi, vyanzo vya mapato na huduma duni za kijamii. Katika bajeti ya mwaka 2009/2010 Mamlaka hizo zimetengewa fedha za kujenga nyumba 10 kwa gharama ya shilingi milioni 30 kila moja.

Mheshimiwa Spika, nyumba zitakazojengwa zitakuwa katika muundo wa mbili kwa moja ili kuwezesha watumishi wengi zaidi kunufaika na huduma hii. Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo usafiri wa majini ni mgumu zitapatiwa Boti. Mamlaka hizo ni pamoja na Mafia, Kigoma, Muleba, Nkasi Ukurewe, Ludewa, Sengerema, Rufiji, Mpanda na Kilwa. Boti hizo zitatumika kusaidai watumishi kusafiri katika visiwa hivyo pia katika azma ya kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo kwenye mazingira magumu na ambazo hazina umeme zitapatiwa vifaa vya kuzalisha umeme wa

Nishati ya Jua badala ya Jenereta. Vifaa hivi vitawekwa kwenye maeneo yenye mahitaji muhimu kama vile shule za sekondari na vituo vya kutolea huduma za afya. Mamlaka hizo ni pamoja na Nkasi, Tunduru, Kigoma, Newala, Ruangwa, Liwale, Kilindi, Namtumbo, Tandahimba, Mafia, Nachingwea Ngara, Ngorongoro, Chunya, Ileje, Tarime, Muleba, Longido, Ludewa, Kasuru, Kibondo; Sengerema yenyewe itapatiwa jenereta kwa sababu wameshaanza kutumia umeme wa jenereta ikiwa ni pamoja na Ukerewe pamoja na Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo majengo yake yapo katika hali mbaya sana na yanahitaji ukarabati na mengine kujengwa upya na fedha hizo zitapelekwa moja kwa moja kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zifuatazo zitapewa fedha hizo:- Nkasi, Kilindi, Muleba, Nachingwea pamoja na Tunduru. Hata hivyo, imekubalika kuwa kuwe na ramani ziwe zinazoshabihiana kwa majengo yote ya Serikali. Suala hili linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri zitapewa fedha za kujenga hoteli hasa zile Halmashauri zilizoko karibu na Mbuga za wanyama kama vile Tunduru Namtumbo, Liwale, Ulanga, Nanyumbu na kadhalika na zile zilizoko maneo ya wafugaji wanaohamahama kama vile Longido, Ngorongoro na kadhalika. Hali kadhalika, zile Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ziko pembezoni kabisa mwa nchi hii kama vile Kasulu, Kibondo na kadhalika nazo zitapatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii pia ununuzi wa magari ya wagonjwa umezingatiwa na kuna Wilaya ambazo hazina kabisa magari ya wagonjwa, katika bajeti hii suala hili limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii pia, suala la shule maalum za walemavu, limezingatiwa na fedha hizo zimetengwa moja kwa moja kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Wilaya zenye mazingira magumu zimebainishwa katika utafiti uliofanyika mwaka 2005 na kuwasilishwa Serikalini. Ilibainishwa kwamba watumishi wengi hawapendi kwenda katika Wilaya hizo kwa sbabu mbalimbali. Kwa hiyo utafiti huu ndio umefanyiwa kazi katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na Zanzibar. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa vikao viwili vya Ushirikiano kati ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI vimefanyika. Vikao hivi vimetoa fursa ya kujifunza mafanikio na changamoto mbalimbali zinazotokea katika pande zote mbili katika kutoa huduma kwa wananchi. Vikao hivi vinafanyika kwa mujibu wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuendeleza na kuimarisha Muungano. Kikao cha kwanza kilifanyika huko Mjini Zanzibar mwaka 2006, na kikao cha pili

kilifanyika hapa Dodoma mwaka 2008. Kikao cha tatu kitafanyika huko Pemba mwaka 2009. Yote hiyo ni katika kuimarisha na kudumisha ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Kwa mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea na Ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge ambao ulianza kutekelezwa katika mwaka 2007/2008. Jumla ya Ofisi 50 za Wabunge zikiwemo 40 Tanzania Bara na 10 Tanzania Zanzibar zinaendelea kujengwa na zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Katika mwaka 2009/2010, Serikali imetenga fedha ili kuendelea na Awamu ya Tatu ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge, ambapo Ofisi nyingine 20 zitajengwa, 16 Tanzania Bara na 4 Tanzania Zanzibar. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote wanaosimamia kwa karibu ofisi hizi hadi hapo zilipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Ulinzi na Usalama kwa Kushirikisha Jamii. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ina jukumu la kuhakikisha kuwa kunakuwepo amani na utulivu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ili kutekeleza jukumu hili, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeimarisha ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Ndani katika kutekeleza Mpango wa Ulinzi Shirikishi. Aidha, kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, ibara ya 111 na matakwa ya MKUKUTA, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, inatekeleza Mpango wa Miji Salama kwa lengo la kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza jukumu hili. Mwezi Julai, 2008 Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilizindua Mpango Mkakati wa kuzuia uhalifu Mijini unaotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa kuzipelekea Mamlaka za Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Wabia wa Maendeleo kutoka nchi mbalimbali na Benki ya Dunia inaendesha Mfumo wa Kuzipelekea Mamlaka za Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbali mbali katika maeneo yao. Mfumo unafanya Tathmini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kila mwaka na Ruzuku ya Maendeleo hupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofuzu vigezo vya kupata ruzuku hiyo kulingana na jinsi zilivyofuzu. Mamlaka za Serikali za Mitaa pia zinapata Ruzuku ya Kujenga Uwezo katika maeneo ambayo zitakuwa zimebaini kuwa zina upungufu. Mfumo ulianza rasmi mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009, jumla ya shilingi bilioni 153.4 kati ya shilingi bilioni 232.6 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mfumo huo unaopeleka Ruzuku ya Maendeleo na ya Kujenga Uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazofuzu vigezo vya upimaji. Fedha hizo zinajumuisha Ruzuku isiyokuwa na masharti *(Capital Development Grants)* na ruzuku kutoka Sekta nne zilizojiunga kwenye mfumo huu ambazo ni Elimu kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo ya Elimu, Maji kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo ya Maji Vijijini, Afya kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo ya Afya na Kilimo kwa ajili ya Maendeleo ya Kilimo.

Ruzuku hiyo ya Maendeleo inajumuisha shilingi bilioni 18 ambazo ni mchango wa Serikali ambapo shilingi bilioni 5 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya *Capital Development Grants*, shilingi bilioni 5 kwa ajili ya Ruzuku ya maendeleo ya Elimu na shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya Maendeleo ya Afya. Fedha hizi zimetumika kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika maeneo yao. Kwa mwaka 2008/2009 fedha za ruzuku ya maendeleo isiyokuwa na masharti zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na zimetumika kutekeleza miradi katika sekta zifuatazo:-

(i) Elimu 47%;

(ii) Afya 10%;

(iii) Utawala 23%; na

(iv) Sekta nyingine 20%.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzisaidia Serikali za Mitaa. Mradi huu alianza rasmi mwaka 2004/2005. Shughuli zake ni pamoja na kushirikiana na Wabia wa maendeleo na Serikali katika kutekeleza majukumu yafuatayo:- Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kupeleka ruzuku ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kutekeleza shughuli zake za kimsingi za utoaji huduma bora kwa wananchi wa maeneo yake, Kuboresha miundombinu ya Halmashauri za Jiji la DSM, Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Jiji la DSM na kuwezesha kujenga uwezo kwenye maeneo yanayohitaji kujengewa uwezo ili Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kuzingatia masuala ya utawala bora, usimamizi wa fedha ulio bora na unaokubalika na kujihakikishia kwamba zitaendelea kufuzu kupata stahili yake kwa asilimia 100 ya ruzuku ya maendeleo mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka 2009/2010 Mradi unatarajia kuendelea kutekeleza shughuli za mradi kama nilivyoelezwa hapo juu na hii ikiwa ni pamoja na maandalizi ya uanzishaji wa Mradi mpya wa Tanzania *Strategic Cities*. Mradi huu unalenga kuboresha na kupanua miundombinu pamoja na kuboresha utoaji huduma za jamii katika baadhi ya miji Tanzania Bara. Mradi unategemewa kuanza rasmi mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM). Ili kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inaratibu ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 jumla ya shilingi bilioni 32.4 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi. Hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 11.1 zimepatikana na zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 132. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wabia wa Maendeleo imeanzisha Mfuko Maalum wa Afya kwa Mfumo wa Utoaji Ruzuku katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfuko huu ni moja ya njia za

kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi. Wabia wa Maendeleo wanaochangia katika Mfuko huu ni Ujerumani pamoja na Denmark. Tunatarajia kwamba Wabia wa Maendeleo wengine wataanza kuchangia katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ibara ya 60, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa kushirikiana na Jamii na Wabia wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2009, kiasi cha shilingi bilioni 44.7 kimetolewa kati ya shilingi kiasi cha shilingi bilioni 48.6 zilizotengwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa shule za msingi. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wananchi wametumia shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya kujenga madarasa 480, nyumba jumla ya nyumba za walimu 571, matundu ya vyoo 249 na kutengeneza madawati 138,217.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 Mpango unalenga kuendelea kujenga miundombinu yaani madarasa, nyumba za walimu, vyoo na kutengeneza madawati katika shule za msingi. Fedha za kutekeleza Mpango huu zimetengwa kwenye bajeti za kila Mamlaka za Serikali za Mitaa moja kwa moja kama njia mojawapo ya kuendeleza mfumo wa kugatua majukumu na rasilimali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mpango unalenga kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa moduli za kufundishia Kamati za Shule zaidi ya 15,000.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Sekondari. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaanza rasmi jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendesha Shule za Sekondari. Maandalizi ya kupokea jukumu hilo yamefanywa na kazi zilizofanyika mwaka 2008/2009 katika maandalizi ya kupokea jukumu hilo ni:-

(i) Kuandaa mgawanyo wa majukumu ya Utoaji wa Elimu ya Sekondari baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Shule na Wazazi.

(ii) Bajeti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeandaliwa kwa kuzingatia wajibu mpya wa Usimamizi na Uendeshaji wa Shule za Sekondari; Kuundwa Idara mpya ya Elimu ya Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(iii) Kuundwa Idara mpya ya Elimu ya Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(iv) Kuteua Maafisa Elimu wa Idara ya Elimu ya Sekondari na Mafisa Elimu Taaluma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(v) Ili kupata ufumbuzi wa tatizo la chakula kwa shule za bweni utafiti umefanyika kwa lengo la kupata njia bora zaidi ya kuzihakikishia shule zinakuwa na chakula wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI pamoja na Sekretarieti za Mikoa zitaendelea kutoa mafunzo kwa ajili Maafisa Elimu na Maafisa Elimu Taaluma walioteuliwa kwa ajili ya Idara ya Elimu ya Sekondari, kufuatilia na kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Shule za Sekondari, kufuatilia na kutathmini mipango na miradi ya Elimu ya Sekondari, kuangalia changamoto zinazozikabili shule za Sekondari, kutambua sababu zinazosababisha migogoro ya mara kwa mara na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa shule zote nchini zinakuwa na Waalimu wa kutosha Serikali itahakikisha kuwa Waalimu na Watumishi wengine wamepangiwa Kazi katika maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa Waalimu. Kuanzia sasa Mamlaka za Miji hazitapangiwa waalimu wapya ili kutoa mwanya kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zina upungufu mkubwa kupata Waalimu wa kutosha watakaoweza kuhudumia Wanafunzi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Barabara zilizopo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zina urefu wa jumla ya kilomita 56,626 kati ya hizo kilomita 33,000 ziko kwenye hali nzuri na kawaida. Madhumuni ya Mfuko wa Barabara ni kuhakikisha kuwa barabara zilizoko kwenye hali nzuri zinafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ili zisiharibike. Kilomita 23,626 ziko katika hali mbaya na zinahitaji ukarabati mkubwa kwa kutumia fedha za maendeleo ambazo ni chache.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ibara ya 44 (a) na (m) inaelekeza kuendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* na kuanzishwa Programu ya Taifa ya Usafirishaji Vijijini. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Mfuko wa Barabara uliidhinishiwa shilingi bilioni 65.5 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 31,100 pamoja na ununuzi wa magari. Hadi mwezi Machi 2009 kiasi cha shilingi bilioni 34.4 kilikuwa kimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na shilingi bilioni 1.2 zilinunulia magari kwa ajili ya usimamizi. Hadi sasa kilomita 6,000 za barabara zimefanyiwa matengenezo na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, chini ya Programu ya Usafiri katika Serikali za Mitaa *(Local Government Transport Programme)* Shilingi bilioni 23 ziliidhinishwa kwa mwaka uliopita na hadi sasa tumepokea shilingi bilioni 5 nazo zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kazi zinaendelea kutekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, chini ya Programu ya Usafiri na Uchukuzi Vijijini *(Village Travel and Transport Programme)*, kiasi cha shilingi bilioni 1.9 kilitengwa kwa ajili ya kukarabati km 500 za barabara za waenda kwa miguu, mikokoteni inayovutwa na wanyama kazi, baiskeli na mafunzo ya wasimamizi wa barabara hizo 115 kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 55. Hadi Machi 2009 Shilingi bilioni 1.1. zimepokelewa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 27 na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010, Serikali imetenga Shilingi bilioni 85 za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya km. 30,000 za barabara. Vilevile, katika Mpango wa *Local Government Transport Programme*, kiasi cha shilingi bilioni 25 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa km. 1,000 za barabara. Aidha, Mpango wa Usafiri na Uchukuzi Vijijini umetengewa Shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ukarabati wa barabara za waenda kwa miguu, mikokoteni inayovutwa na wanyamakazi na baiskeli katika Halmashauri 27.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira. Katika nchi yetu suala la kuhifadhi Mazingira ni jukumu la kila mwananchi ili kupambana na changamoto hii kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na Mikoa zinalo jukumu la kuratibu usimamizi na uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, Miradi ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Ardhi-Oevu, katika Mikoa 11 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 62. Jumla ya shilingi bilioni 5.3 ziliidhinishwa. Hadi Machi, 2009 kiasi cha shilingi bilioni 1.4 zilitolewa kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji, tathmini na uwezeshaji wa Halmahauri katika uandaaji wa mipango, bajei na taarifa za utekelezaji, uhifdhi wa misitu ya jamii, ardhi-oevu na upandaji miti.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa 2009/2010, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, imepengiwa jumla ya shilingi 333,792,000 kwa ajili ya kazi hiyo. Ofisi pia itaendelea na uratibu wa utekelezaji wa Miradi ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu, Ardhi-oevu na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2005 Ibara 31 inazungumzia maendeleo ya kilimo ambacho kina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na vita dhidi ya umaskini. Ili kufikia azma hiyo, Serikali inatekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo kupitia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* wenye lengo la kuwawezesha wakulima na wafugaji ili kuongeza tija kutokana na kuwapatia elimu na teknolojia bora, uhakika wa masoko na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji. Pia kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo kwa kujenga mazingira bora ya kisera na kisheria.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* imeongezeka kutoka shilingi bilioni 14.0 mwaka 2006/2007 mpaka bilioni 57 kwa mwaka 2007/2008. Kati ya hizo *DADPs* zilitengewa shilingi bilioni 49.6 na Umwagiliaji shilingi bilioni 7.4. Kwa mwaka 2008/2009 shilingi bilioni 58.8 zilitengwa na kati ya hizo, *DADPs* zilitengewa shilingi bilioni 54.2 na umwagiliaji shilingi bilioni 4.6.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 83.6, kati ya fedha hizo Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya imetengewa shilingi bilioni 59.8 kwa ajili ya kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, Umwagiliaji umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 23. Hilo ni ongezeko la asilimia 42 ukilinganisha na fedha iliyotolewa kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo ya sekta ya kilimo. Kupitia Mipango ya kilimo ya Wilaya, wananchi wamekuwa wakihimizwa kujiunga katika vikundi vya uzalishaji na wengi wameitikia wito huo. Serikali inavijengea uwezo vikundi hivyo kwa kutoa mafunzo yanayolenga kuboresha uendeshaji na usimamizi wa shughuli zao za kila siku. Utekelezaji wa *ASDP* unafanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ambayo inaibuliwa kwa kutumia mbinu shirikishi katika ngazi za msingi. Kwa sababu hiyo, utekelezaji wa *ASDP* unazingatia sera ya Serikali ya Kupeleka Madaraka kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo Mijini na Usimamizi wa Mazingira (UDEM), iliyoanza kutekelezwa mwaka 2006/2007, ina lengo la kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa wa kusimamia maendeleo ya Miji sambamba na hifadhi ya mazingira na kuziwezesha kifedha kutekeleza miradi ya maendeleo inayolinda mazingira mijini. Programu inatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark. Kwa mwaka 2008/2009, shilingi bilioni 1.8 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Miji 19 kwa ajili ya kuzijengea uwezo katika maandalizi ya mipango shirikishi, kuweka mfumo wa kumbukumbu za habari za kimenejimenti zinazohusu masuala ya mazingira katika miji, ukusanyaji na uchambuaji wa takwimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Programu itaendelea kukamilisha mchakato wa kuunda Sera ya Usimamizi wa Maendeleo Mijini ili kuweesha kutekeleza Malengo ya Milenia katika Sekta ya Miji. Katika kipindi cha 2009/2010, shilingi bilioni 3.8 zimetengwa na zitapelekwa kwenye Mamlaka za Miji. Fedha hizi ni kwa ajili ya Mamlaka za Miji kuendeleza shughuli za kujenga uwezo na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo. Jukumu la Chuo Cha Serikali za Mitaa Hombolo ni kuimarisha utendaji wa Watumishi na Uongozi wa ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika harakati za kuboresha utendaji wa chuo

kwa mwaka 2008/2009 Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi Maafisa Watendaji wa Mitaa na Vijiji katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Dar es Salaam n.k. Ili kuweza kutimiza majukumu yake na kutoa huduma bora, Chuo kimepanua Ikama kutoka watumishi 61 hadi 79 katika mwaka 2008/2009. Pia eneo la Chuo limeongezwa toka hekta 45.7 hadi hekta 310. Lengo ni kuwa Chuo kiwe na ukubwa wa hekta 400. Ili kuhakikisha kwamba chuo kinatoa mafunzo kwa kuzingatia taaluma inayokubalika, Wahadhiri wapya 14 wameajiriwa na hivyo kufanya jumla ya Wahadhiri wote kufikia 30.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi ya maendeleo, Chuo kiliidhinishiwa shilingi bilioni 1.1. Hadi Machi, 2009 kiasi cha shilingi bilioni 1.1 kilipokelewa ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bweni moja na ukumbi wa mihadhara. Mpaka sasa kazi hiyo inaendelea na ujenzi utaanza mwishoni mwa mwaka huu. Mtaalamu Mshauri alishapatikana na Mkandarasi anatarajiwa kupatikana mwishoni mwa mwezi Juni, 2009. utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi kupitia Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* uko katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi ili kuboresha ujuzi kwa watendaji wa ngazi za msingi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Chuo kitaendelea kutoa  na pia kitaongezea udahili wa wanafunzi kutoka 249 waliopo hadi  400 mwaka 2009/2010. Lengo ni kufikia wanafunzi 2,000 ifikapo mwaka 2011/2012.

Aidha, chuo kitaendelea kuboresha miundombinu kwa kuendeleza ujenzi wa majengo mapya. Fedha za Maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2009/2010 ni shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa bweni moja, ukumbi wa Mihadhara na kuanzisha ujenzi wa nyumba nne za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha linachangia katika kupambana na adui Maradhi, Ujinga na Umaskini. Ili kuboresha huduma zake kwa mwaka 2008/2009 Shirika limepanga kufanya ukarabati wa miundombinu. Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Hospitali ya Tumbi na kuendelea na ukarabati wa miundombinu na kazi hizo zimeanza.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Shirika kwa mwaka 2009/2010 ni pamoja na; kuendelea na upanuzi wa Hospitali ya Tumbi; kuendelea kutoa mafunzo ya Maafisa Tabibu 120. Malengo mengine ni pamoja na kutoa elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na malezi bora kwa wanafunzi 2,594. Kuendelea kutoa elimu katika fani mbalimbali katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha kwa wananchuo 220; kuendelea kutunza mazingira; na kuendelea kutoa elimu ya nadharia na vitendo juu ya ufugaji bora wa kuku na ng’ombe wa maziwa. Kwa mwaka huu pia hospitali ya Tumbi imetengewa fedha kwa ajili ya upanuzi.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* Na. 9 ya mwaka 2006, Mfuko umeimarika kwa kiwango kikubwa katika masuala ya kuboresha mafao ya wanachama wake, kukusanya michango na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma zake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009,Mfuko umeweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 32.8 sawa na asilimia 116 ya lengo walilojiwekea la shilingi bilioni 28.3. hadi mwezi Machi 2009, Mfuko pia umewalipa wastaafu 644 na warithi wa wanachama waliofariki 256 shilingi bilioni 8.0.

Vile vile, Mfuko ulilipa jumla ya shilingi milioni 920.7 mafao ya kila mwezi kwa wastaafu. Aidha, mfuko umeongeza wanachama 6,327 sawa na asilimia 141 ya lengo la kuandikisha wananchama 4,500. Kwa sasa Mfuko una wanachama 64,585. Idadi hii inatarajiwa kuongezeka kwa kiwango cha asilimia 10 kila mwaka hasa baada ya kuanza kuandikisha Madiwani na makundi mengine ya jamii. Mfuko umezidi kuongeza wanachama na kwa mwaka huu umekusanya fedha zaidi ya kile kiwango kilichotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, Ibara ya 52 inaielekeza Serikali kuona umuhimu wa kufikiria uwezekano wa kutumia uwezo mkubwa wa fedha katika Mashirika ya Hifadhi ya Jamii. Katika kutekeleza azma hiyo, Mfuko huu umechangia ujenzi wa Kitivo cha Sayansi ya Afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma na upanuzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. Miradi hiyo imeishaanza na iko katika hatua ya utekelezaji. Miradi hiyo imeanza kwa uteuzi wa Wataalam waelekezi ambao wamekamilisha kazi za usanifu wa michoro. Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa vyuo hivi inatarajia kuanza rasmi mwaka ujao wa fedha na inakisiwa kuwa mradi wa Chuo cha Serikali za Mitaa utagharimu shilingi bilioni 46.2 na shilingi bilioni 30 kwa mradi wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Pia Mfuko unayo miradi mbalimbali ambayo itatekelezwa kwa ubia na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Miradi hiyo ni ujenzi wa Soko Kuu la Mwanza, Kituo cha Mabasi Msamvu (Morogoro), Kituo cha Malori na Soko la Mazao - Mbezi Luis. Aidha, Mfuko unaendelea kutoa mikopo kwa *SACCOS* za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuziwezesha kuwakopesha wanachama wake kwa riba nafuu. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero imeishapata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 10.0 ambazo ziliahidiwa kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu ikiwa ni kuendelea kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa mwaka 2006 ya kuupatia shilingi bilioni 107.3 kwa awamu kumi ili kuuwezesha kumudu mabadiliko ya kuubadili kuw Mfuko wa Pensheni.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Jukumu la Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982, ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ili kusaidia kuleta maendeleo. Hadi Machi, 2009 mikopo ya jumla ya shilingi milioni 741.6 imetolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nne na kufanya mikopo yote iliyotolewa kufikia jumla ya shilingi bilioni 3.7 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 45 ikilinganishwa na maombi yaliyowasilishwa ya jumla ya shilingi bilioni 11.8. kwa upande wa Michango ya Akiba, jumla ya shilingi milioni 192.2 zimechangwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 24 kati ya shilingi milioni 450 zilizokadiriwa na kufanya michango yote ya Akiba kufikia jumla ya shilingi bilioni 2.4 ikilinganishwa na kiasi kinachopaswa kuchangwa cha jumla ya shilingi bilioni 5.5. kwa upande wa Mikopo na Riba, jumla ya shilingi milioni 147.7 zimerejeshwa na kulipwa kati ya shilingi milioni 495 zilizotrajiwa kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingi zina nia ya kukopa, lakini kwa upande mwingine kasi ndogo ya kurejesha mikopo na uwasilishaji wa michngo, kunapunguza uwezo wa Bodi kukopesha zaidi. Hata hivyo, Bodi imeanzisha utaratibu wa kuingia mikataba ya kurejesha madeni na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazodaiwa. Hadi Machi, 2009, Bodi inazidai Mamlaka za Serikali za Mitaa 122 jumla ya shilingi bilioni 5.6 kwa viwango tofauti kutokanana michango ya akiba.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Bodi hiyo ni kukopesha Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuzisaidia Serikali za Mitaa. Hadi sasa kuna Halmashauri ambazo zimekopeshwa. Nitoe wito kwa Halmashauri kurudisha kwa haraka fedha hizo ili Halmashauri nyingine ziweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam *(Dar es Salaam Rapid Transit).* Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Ibara ya 45(h) inaelekeza kwamba katika kuboresha hali ya usafiri, hatua zichukuliwe kutekeleza Mradi wa Mabasi ya Usafiri wa Haraka Jijini Dar es Salaam. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilianzisha Wakala wa Usafiri wa Haraka mwezi Mei, 2007. Jukumu kubwa la wakala, ni kuratibu uedeshaji wa Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka *(DART)* katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano. Katika kutekeleza jukumu hilo kwa mwaka 2008/2009, Serikali imekamilisha taratibu za kupatikana kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani milioni 122.1 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kupitia Awamu ya Pili ya mradi wa *Central Transport Corridor (CTCP2);* Kukamilika kwa makubaliano kati ya *DART* na *TANROADS* ya kusimamia ujenzi wa miundombinu itakayotumiwa na Mabasi Yaendayo Haraka; Ulipaji wa fidia wa mali zitakazoathiriwa na miundombinu iliyotarajiwa kujengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupatikana kwa fedha za ujenzi wa miundombinu kutoka Benki yan Dunia, Julai, 2008 zabuni ya ujenzi wa miundombinu ya *DART* ilitangazwa tarehe 25 Julai, 2008. Baada ya uchambuzi zabuni hiyo haikufanikiwa *(Non Responsive).* Tathmini ilifanyika na kugundua sababu zilizofanya zabuni hiyo kukosa waombaji kuwa ni kuhusisha kazi za ujenzi wa barabara na majengo kwa pamoja.

Kutokana na hili ilibidi kutafuta Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu upya kwa kutenganisha ujenzi wa barabara na majengo. Usanifu huu umekamilika na zabuni ya ujenzi wa miundombinu itatangazwa mwezi Julai, 2009 na kazi ya ujenzi inategemewa kuanza mwezi Januari 2010. Shughuli nyingine zilizofanyika ni kuanzisha na kuzindua mradi mdogo wa elimu kwa jamii kuhusu mfumo bora wa mabasi na mahitaji ya nishati safi. Mradi huu unaofadhiliwa na Programu ya Umoja wa Mataifa ya Hifadhi ya Mazingira (UNEP), unalenga kujenga uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa mfumo mpya wa mabasi na kuwaandaa wananchi kuutumia wakiwa wanajua manufaa yake kiuchumi, kiafya na kimazingira. Tunasema kwamba mradi huu unaanza rasmi mwaka huu na ujenzi unategemewa kuanza mwezi Januari mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba nizishukuru Kamati za Bunge za Sheria, Katiba na Utawala na Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa michango na maelekezo yao kuhusu utendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati hizo zimetoa changamoto nyingi ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imeahidi kuzifanyia kazi kwa lengo la kuboresha utendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia naomba nitambue na kushukuru juhudi zinazofanywa na Asasi za Kiraia (CSOs) ambazo zimekuwa mstari wa mbele kufuatilia masuala ya maendeleo ya wananchi. Asasi hizi zimetumia nyenzo na rasilimali zake kufanya ufuatiliaji wa matumizi mazuri ya fedha za wananchi, wametekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na hata kutoa elimu ya demokrasia na Utawala Bora katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi. Ushirikiano wa aina hii baina ya Asasi za Kiraia na Serikali, ni muhimu na utaendelea kudumishwa. Vile vile, napenda kutambua mchango mkubwa wa wananchi wanaoutoa katika kutekeleza shughuli zao za maendeleo kwa kuchangia katika miradi ya maendeleo na ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo yao na katika ufuatiliaji na kuhoji matumizi ya rasilimali zinazopelekwa na Serikali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, niwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Kwa kuwa umetugawia hotuba yako, basi tutaendelea kuitafakari. Sasa namwita Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kuhitimisha hotuba yake.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Katika kuhitimisha hotuba, basi naomba kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote kwa ushauri wao ambao umewawezesha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, kutekeleza majukumu yao ya Kitaifa kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Phillemon Luhanjo pamoja na Vyombo vyote vya Dola kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuiwezesha kukamilisha maandalizi yote ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2009/2010 pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya kila Wizara, Mikoa, Wakala na Taasisi za

Serikali Zinazojitegemea. Nawashukuru Watanzania wote na Washirika wetu wa Maendeleo kwa michango yao ambayo imewezesha kufanikisha Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Phillip Sanka Marmo, Mbunge wa Mbulu, Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa msaada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Shukrani za pekee kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa jitihada walizoonyesha katika kipindi hiki. Nawashukuru vile vile Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu, Bwana Peniel Michael Lyimo na Bibi Maimuna Kibenga Tarishi na Naibu Katibu Mkuu, Bwana Fanuel Eusebius Mbonde kwa ushauri wao wa Kitaalam ambao wamenipa mimi na Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi katika kipindi hiki. Nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2009/2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Nchi yetu imepata misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wetu mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa Nchi rafiki, Nchi fadhili, Taasisi za Fedha Duniani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mifuko Mbalimbali ya Fedha Duniani, Madhehebu ya Dini na Mashirika Yasiyo ya Serikali. Misaada na mikopo hiyo imechangia sana katika kutekeleza miradi ya mbalimbali ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo waliyotupatia na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za kuleta maendeleo ya Taifa letu.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 28, sasa nawomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atoe hoja ili uweze kumalizia hotuba yako hata kama itakuwa imepita saa saba. Sasa basi namwomba atoe hoja ya kutengua Kanuni hiyo ili tuweze kuongeza muda, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha mchakato wa hotuba ya Waziri Mkuu inayoendelea sasa, naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya 28(3) iweze kutenguliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki hoja ya kutengua Kanuni ya 28(3))*

**SPIKA:** Karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili uhitimishe bila presha yoyote, kupanda wala kushuka. *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa mwaka 2009/2010, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 143,268,010,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 67,979,095,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 75,288,915,000 ni kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa mwaka 2009/2010 Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya Shilingi 197,886,256,000. Kati ya hizo, Shilingi 124,368,171,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 73,518,085,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Shilingi 168,135,049,000. Kati ya hizo Shilingi 123,013,358,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 45,121,691,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Aidha, Halmashauri zote zinaombewa jumla ya Shilingi 2,044,567,344,000 kati ya hizo Shilingi 1,565,973,955,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 478,593,389,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano inaombewa jumla ya Shilingi 68,257,038,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge ambapo Shilingi 62,109,293,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 6,147,745,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya kwa muhtasari, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2009/2010 ya jumla ya Shilingi 68,257,038,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge, na jumla ya Shilingi 2,553,856,659,000 kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo za Ndani na Nje kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu:-

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu Sh.143,268,010,000

- Matumizi ya Kawaida Sh.67,979,095,000

- Matumizi ya Maendeleo Sh.75,288,915,000

Mheshimiwa Spika, mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa:-

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Sh.197,886,256,000

- Matumizi ya Kawaida Sh.12,368,171,000.

- Matumizi ya Maendeleo Sh.73,518,085,000

(ii) Ofisi za Wakuu wa Mikoa Sh.168,135,049,000

- Matumizi ya Kawaida Sh.123,013,358,000

- Matumizi ya Maendeleo Sh.45,121,691,000

(iii) Ruzuku kwa Halmashauri Sh.2,044,576,344,000

- Matumizi ya Kawaida Sh.1,565,973,955,000

- Matumizi ya Maendeleo Sh.478,593,389,000.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge, Sh.68,257,038,000.

- Matumizi ya Kawaida Sh.62,109,293,000

- Matumizi ya Maendeleo Sh.6,147,745,000. Jumla Kuu ni Sh.2,622,113,697,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii yapo Majedwali ambayo yanafafanua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha makadirio ya Ofisi yako kwa upana na nadhani tumeelewa vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kwamba sasa itabidi kusitisha shughuli ili saa 11.00 ndio tumsikie Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ila kabla hatujatoka, nawajibika nitaje majina ya Waheshimiwa Wabunge ambao wataanza kuchangia ili waweze kujiandaa kwa kuwepo ukumbini. Nitawataja watano wa mwanzo ambao ni Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi na Mheshimiwa Abdulkarim Shah. Naomba hao wote wawepo ukumbini saa 11.00 jioni ili tuanze nao.

Kwa sasa, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.06 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Samuel Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli pale mchana. Niliwaarifu kwamba kama kawaida ya kanuni zetu, sasa itakuwa ni kupokea maoni ya Kamati, baadaye maoni ya Kambi ya Upinzani halafu ndio tutaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Ninawaomba Waheshiwa Wabunge msiniletee tena maombi ya kuchangia kwa sababu hata hawa mia moja na moja waliiomba si wote watakaopata nafasi kwa siku hizi yaani leo, kesho na kesho kutwa na kidogo sana siku ya Alhamis, Mheshimiwa Waziri Mkuu anapohitimisha, kwa uzoefu tulio nao, Wabunge takribani sitini tu ndio wataweza kuchangia. Kwa hiyo, kuongeza juu ya mia moja na moja, ni kupoteza muda tu. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, tupate maoni ya Kamati.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Namba 99 (7), Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, Fungu 25 - Waziri Mkuu, Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 – Mfuko wa Bunge, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania.

Aidha, nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, kwa Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Mafungu 70 – 89 na 95 kwa ajili ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, ofisi ya waziri mkuu sera uratibu na bunge Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi; Baada ya kuiletea Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha wa 2009/2010, tarehe 4 Juni, 2009 Kamati ilikutana katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam na kupokea maelezo ya Muhutasari wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Aidha Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo na Mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Fungu 25 – Waziri Mkuu na Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2008/2009, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ilitekeleza shughuli mbali mbali za kuliletea taifa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Baadhi ya shughuli ambazo zilifanyika ni pamoja na kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu

kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo mikoani, ambako pamoja na mambo mengine aliweza kukutana na wananchi ambao walimweleza kero zao nyingi za msingi na matatizo yao mbalimbali. Vile vile aliweza kutoa maelekezo kwa watendaji na kutoa msisitizo kwa viongozi kuwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara maalum katika mikoa ya kanda ya ziwa na mingineyo ili kutoa msukumo kwa viongozi kuweza kukabiliana kwa nguvu zao zote tatizo la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino), juhudi ambazo kila mmoja wetu anakiri kuwa zimeleta matunda na sasa hivi Watanzania wote wenye ulemavu wa ngozi wanaishi na kuendelea na kazi za ujenzi wa taifa bila hofu na wasiwasi mkubwa. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi zake hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha baadhi ya kazi zilizofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 ni pamoja na kuzijengea uwezo kamati mbali mbali za maafa za mikoa, ili ziweze kujiweka tayari kukabiliana na maafa na majanga mengine yanapojitokeza. Kwa kipindi hicho cha Mwaka wa fedha, Ofisi hii iliweza kukabiliana na maafa makubwa ya ajali ya mlipuko wa mabomu katika Kambi ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania (JWTZ) iliyopo Mbagala, Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu iliendelea na kuratibu Shughuli za Bunge ambazo hutakiwa kutekelezwa na Serikali yakiwemo Maagizo na Maazimio mbali mbali pamoja na ziara za Kamati za Bunge kwenye taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilielezwa kuhusu mikakati iliyopangwa na hatua zinazochukuliwa kutekeleza sera ya serikali ya kuhamishia Makao Makuu yake Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Fungu 42 – Mfuko wa Bunge.Katika Mwaka uliopita ilielezwa kuwa Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya Sh. 57,442,490,900/= zilizowezesha kufanyika kwa mikutano minne ya Bunge ambayo ilichambua kikamilifu masuala ya kitaifa na kusimamia utendaji wa Serikali. Aidha ilielezwa kwamba Kamati za Bunge zilikutana kama ilivyopangwa na kufanya ziara maeneo mbali mbali kwa nia ya kufuatilia utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuhusu juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Ofisi ya Bunge katika kuliwezesha Bunge letu kuwa la kasi na viwango *“Standard and Speed”*, ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kama yalivyoainishwa katika ibara ya 63 (2) ikisomwa kwa pamoja na ibara za 89 na 96 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Fungu 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitengewa jumla ya shilingi 12,794,241,100/= ili kutekeleza kazi mbalimbali. Kamati ilielezwa kuwa kati ya kazi muhimu zilizofanyika ni pamoja na;- kuandaa rasimu ya kuunganisha Sheria ya Uchaguzi, kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Mikoa sita (6) ya Tanzania, kuweka vigezo vya kugawa mipaka ya majimbo, kuandaa rasimu ya Sheria ya Tume ya Uchaguzi, kutoa taarifa kwa wapiga kura na wadau wengine kwa wakati, kutoa elimu kwa wapiga kura pamoja na kusimamia chaguzi za nafasi za Ubunge na Udiwani.

Mheshimiwa Spika, aidha, ilielezwa kuwa kulikuwa na mwamko mdogo wa wananchi waliojiandikisha kupiga kura kujitokeza siku ya upigaji kura wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Katika mwaka 2008/2009, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iliidhinishiwa Sh.19,901,907,000/=, ambazo shs.17,252,999,996/= ni ruzuku kwa vyama vya Siasa na 2,648,907,000/= ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Katika kipindi hicho kazi muhimu zilizofanywa na Ofisi hii ni pamoja na kukagua shughuli za vyama vya siasa Kisheria katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Mjini/Magharibi, Kusini Pemba, Pwani, Lindi, Tanga na Mbeya. Aidha Ofisi ilishiriki katika timu ya SADC kuangalia uchaguzi wa Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Spika, Vile vile Ofisi iliifanyia kazi Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2008 ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Januari 2009. Aidha kwa kipindi hicho Vyama vitatu (3) vya siasa vilipatiwa usajili wa muda ambavyo ni *Peoples Democratic Movement* (PDM), *Democratic National Congress* (DNC) na *alliance for Tanzania Farmers Party* (ATFP).

Mheshimiwa Spika, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Tume ya kudhibiti Dawa za kulevya iliidhinishiwa sh. 1,136,100,000/=. Kamati iliarifiwa kuwa baadhi ya kazi ambazo zilitekelezwa na Tume hiyo ni pamoja na kukamilisha utafiti wa kupambana na rushwa katika kudhibiti madawa ya kulevya, kuwezesha uteketezaji wa mashamba ya bangi katika mkoa wa Tanga, kuendelea kuchangia uendeshaji wa kikosi kazi cha kupambana na biashara ya dawa za kulevya, kutoa vifaa vya uelimishaji sanjari na kushiriki katika matukio ya kitaifa ya uelimishaji wa madhara ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Katika mwaka 2008/2009, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania iliidhinishiwa Jumla ya Shs.3,754,282,000/= kwa ajili ya Mishahara na Matumizi mengineyo. Kazi zilizofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na kuandaa mkakati wa pili wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI (2002-2012), Mkakati wa Kinga Dhidi ya maambukizi mapya ya VVU, kutathimini utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI kwa kuhusisha wadau kutoka katika Sekta na ngazi mbalimbali nchini pamoja na kutengeneza

kuimarisha na kuendeleza *"National Data Base"* ili Tume iweze kukusanya na kuhifadhi Takwimu za kitabibu na zisizo za Kitabibu.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Mbali na kupokea taarifa ya utekekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu wa Bunge kwa mwaka uliopita, Kamati ilipokea maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka. 2009/2010, yakiwemo matarajio ya mapato na mpango wa maendeleo. Aidha Kamati ilifahamishwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huo. Mwisho Kamati iliombwa kuidhinisha kupitisha Jumla ya shilingi 211,525,048,500/= kati ya fedha hizo shs.130,088,388,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shs.81,436,660,500/= ni kwa ajili ya mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana kabisa kutolewa fedha hizo kwa Ofisi hiyo huku ikiweka msisitizo na ushauri wa kuyatilia maanani mambo yote yaliyoshauriwa katika Idara na Vitengo vyake mbalimbali wakati wa kuchambua makisio haya.

Ushauri na Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Fungu 25 – Waziri Mkuu na Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika mafungu haya Kamati ilitoa ushauri wa kuongezwa kwa wigo wa Bajeti ya Waziri Mkuu, ili aweze kufanya ziara nyingi zaidi mikoani ambazo zinaonekana kuwa na manufaa makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu suala la Uratibu wa maafa kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kujipanga vizuri kukabiliana na maafa ikitilia maanani kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa baadhi ya mikoa kukumbwa na balaa la njaa nchini kwa mwaka huu, kutokana na kukosekana mvua ya kutosha katika mikoa mingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri serikali kuweka azma ya dhati ya Kuhamia Makao Makuu Dodoma kwa kuzitaka wizara zihamie rasmi Dodoma. Aidha Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu – *CDA*, kulichukua suala la upimaji na ugawaji wa viwanja kwa umakini mkubwa ili kuepuka matatizo yaliyoanza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Fungu 42 – Mfuko wa Bunge. Kamati imeridhika na uendeshaji wa Bunge na kwa hivyo inaishauri serikali kuendeleza juhudi za kulimarisha Bunge hili kama ilivyo kwenye Mpango Mkakati uliozinduliwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kamati inaishauri Serikali kuwa bado elimu ya uraia inahitajika kutolewa kwa kiwango kikubwa ili lengo la wananchi kutumia haki zao za Kikatiba ikiwemo ya upigaji wa kura liweze kufikiwa. Aidha Kamati vile vile ilishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kukaa pamoja na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar *(ZEC)* kuondoa kasoro ndogo ndogo zilizowahi kujitokeza huko nyuma kwa ajili ya chaguzi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge. Aidha Kamati inaishauri serikali kuipatia Tume ya Uchaguzi ya Taifa jengo la kisasa kwa ajili ya kazi zake za kila siku.

Mheshimiwa Spika, Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa. Kamati inaishauri Serikali kuwa, ili vyama vya siasa viweze kuwa na ushindani mzuri katika chaguzi mbalimbali ifikirie namna ya kuvipatia ruzuku vyama vyote vitakavyoshiriki uchaguzi. Aidha Kamati ilishauri Ofisi hii kuendelea kuvisimamia na kuvishauri vyama vya siasa kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria za nchi na Katiba za Vyama vyao, ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza hasa kwa wakati huu wa kuelekea uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na janga hili ambalo kama taifa halikuwa makini, madhara yake yatakuwa makubwa sana katika muda mfupa ujao. Aidha tunaishauri Serikali kuwa na vifaa vya kisasa na mbinu mpya kukabilina na tatizo hili kwani inaonyesha kuwa wahusika wa biashara hii ni watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha na mtandao mpana duniani

Mheshimiwa Spika, Fungu 92 –Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Pamoja na kazi kubwa na ya kupongezwa inayofanywa na Tume hii bado kuna kazi kubwa ya kuratibu mapambano dhidi ya UKIMWI nchini. Aidha elimu bado inahitajika kutolewa katika Mikoa na taasisi mbalimbali ambazo bado zinaonyesha zina kiwango kikubwa cha maambukizi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu ya utekelezaji wa Sheria inayohusu mambo ya UKIMWI iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inaishauri Serikali kusimamia suala la utoaji wa dawa za kurefusha maisha ambalo baadhi ya sehemu limejitokeza kuwa ni la kibiashara badala ya kutoa huduma. Aidha kwa mara nyingine tena Kamati inaishauri serikali kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo la muda mrefu la upatikanaji wa kiwanja ili jengo jipya liweze kujengwa.

## OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA

## SERIKALI ZA MITAA – TAMISEMI

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi. Kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanyika tarehe 4 – 5 Juni 2009 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam. Kama ilivyo ada, tarehe 04 Juni, 2009 Kamati ilipokea maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani. Mb, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, Mb, Naibu Waziri. Aidha, baada ya maelezo hayo, Kamati ilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu yaliyopangwa kwa mikoa kwa mwaka wa Fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mikoa kwa mwaka 2009/2010 kwa Mafungu 70 - 89 na Fungu 95 yaliyowasilishwa na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Majukumu. Katika Mwaka wa Fedha 2008/2009, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitengewa jumla ya Sh. 1,555,839,136,100/= ambazo kati ya fedha hizo Shs. 1,093,087,022,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.462,752,114,100/= kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Ofisi hii kwa Mwaka uliopita pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza. Lakini kabla sijataja maeneo machache ya shughuli zilizotekelezwa, napenda nitumie fursa hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, kwa kufanikisha majukumu yaliyopangwa licha ya ufinyu wa Bajeti ambao umejitokeza katika mafungu waliyoidhinishiwa ya 56, 70-89 na 95.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyojitokeza. Itakumbukwa kuwa kati ya maeneo ambayo yamekuwa yakisimamiwa na Bunge lako tukufu na kutolewa ushauri wa kina kupitia Kamati ya Bunge ya Hesabu za Seikali za Mitaa na Kamati hii, ni utunzaji wa Hesabu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kazi nzuri zinazofanywa na Kamati za Bunge, na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Taasisi nyingine zinazosimamia mamlaka za Serikali za Mitaa, tumearifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliendelea kuboresha utunzaji wa hesabu zao na hivyo hakuna Mamlaka zilizopata hati chafu. Hata hivyo Kamati inasisitiza kuwa matumizi ya fedha yalingane na thamani ya kazi. (Value *for money)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inachukua nafasi hii kuzipongeza Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa kuonesha umakini huo na tunaomba ziendelee kuboresha utekelezaji wa shughuli zingine wanazotekeleza.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo Kamati yangu iliarifiwa kuwa lilitekelezwa kwa mafanikio makubwa mwaka uliopita wa 2008/2009 ni uboreshaji wa Muundo wa Sekretarieti za Mikoa na kuendelea kutoa ushauri wa Kitaalam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, ilielezwa kuwa kulikuwa na ufanisi mkubwa katika Utekelezaji wa Programu za kukuza uchumi na kupunguza umasikini na kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Wabunge, Hospitali za Mikoa, nyumba na Ofisi za Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Vile vile Kamati yangu ilifarijika sana baada ya kupewa taarifa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zilitekeleza kwa mafanikio makubwa mfumo wa kutoa ruzuku ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGDG), Mpango wa Maendeleo ya shule za Msingi, programu za maendeleo ya Kilimo, Ukarabati wa barabara vijijini na uboreshaji wa huduma za Afya. Kamati inapongeza sana mafanikio haya, hasa suala la “Programu za Maendeleo ya Kilimo” ambalo kila mmoja wetu anaelewa umuhimu wake kwa kipindi hiki kinachotukabili. Aidha, Kamati yangu imearifiwa juu ya mafanikio ya maandalizi mazuri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo makubaliano kati ya Serikali na Wadau juu ya jinsi ya kuendesha Uchaguzi huru na wa haki yamefikiwa. Aidha, kamati iliomba Wizara kuendelea kusimamia maandalizi hayo na ikiwezekana Serikali kutoa taarifa ya maandalizi hayo kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizojitokeza. Kamati iliarifiwa baadhi ya Changamoto kadhaa zilizojitokeza kwa Mwaka uliopita 2008/2009 ambazo kati yake Kamati ilishauri zifanyiwe kazi kwa haraka katika Kipindi kijacho. Aidha Changamoto mbili hizo ni “kutowiana kwa majukumu na rasilimali zinazopeleka katika mamlaka za Serikali za Mitaa” na “kutopatikana kwa Wakandarasi wenye uwezo wa kutekeleza miradi mbalimbali kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa”.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Mikoani. Katika kipindi cha mwaka uliopita 2008/2009 Mikoa iliidhinishiwa Sh.32,917,762,000/- kwa kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo shs 29,947,762,000/= ni fedha za ndani na shs. 2,970,000,000/= ni fedha za nje. Shughuli mbalimbali za maendeleo zilizofanyika katika Mikoa kwa Kipindi hicho ni pamoja na;

(i) Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya;

(ii) Ujenzi na ukarabati wa baadhi ya Hospitali za Mikoa;

(iii) Kuendelea na Ujenzi wa Ofisi Mpya ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

(iv) Ujenzi wa Ofisi za Wakuu na nyumba za watumishi wa Wilaya za Rorya, Bahi, Misenyi na Pangani;

(v) Kuendelea na ukarabati wa Hospitali mpya za Mikoa ya Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara, Ruvuma na Mwanza; na

(vi) Ukarabati wa nyumba za kuishi za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya maendeleo ya Mikoa mingi ilipatiwa fedha za ndani kwa wakati kwa kiwango cha asilimia tisini na moja (91%) hadi Machi, 2009. Tatizo kubwa lililojitokeza ni kuipatia miradi hiyo fedha za nje ambazo hadi Machi 2009 ilikuwa imepatiwa asilimia Kumi na tatu (13%.) tu.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali kuipatia miradi hii fedha zinazoidhinishwa za nje na ndani kwa wakati mwafaka, ili kuepuka athari za kupanda kwa gharama za vifaa kunakosababishwa na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Mbali na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009, pia Kamati ilifahamishwa juu ya kazi mbalimbali zilizopangwa kufanyika kwa Mwaka 2009/2010, na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa na Halmashauri . Mwisho Kamati iliombwa ipitishe jumla ya Sh.2,415,288,442,000/=. Kati ya fedha hizo Sh.1,813,355,277,000/= ni Matumizi ya Kawaida ikiwemo Mishahara na Sh.601,933,165,000/= ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na 2009/2010. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo saba (7) maoni hayo yalihusu mambo yafuatayo:-

(i) Semina kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu maboresho ya Serikali za Mitaa;

(ii) Kuongeza Bajeti ya Maendeleo Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI;

(iii) Kuwasilisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wilaya na Mikoa kwa wakati;

(iv) Udhibiti wa Watumishi wasiowajibika katika Halmashauri;

(v) Ujenzi wa Ofisi na Nyumba mpya za Serikali badala ya Ukarabati;

(vi) Taarifa za Vitabu vya Bajeti vya Mikoa kuonyesha maelezo ya kina ya Shughuli zilizopangwa; na

(vii) Matengenezo ya barabara za Mikoa;

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya maoni na ushauri wa Kamati kwa ujumla yamo katika Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 yaliyowasilishwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti lililopita.

Mheshimiwa Spika, maoni na Ushauri wa Kamati Kwa Bajeti ya 2009/2010.Kwa mwaka 2009/2010, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Ukarabati wa majengo na ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Ofisi zao uendelezwe. Vile vile Ujenzi wa Jengo la Mkuu wa Mkoa wa Kagera upewe kipaumbele kwa Bajeti ijayo ya 2010/2011;

(ii) Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* Uongezwe kutoka asilimia 30% ya sasa hadi angalau asilimia arubaini 40% ili fedha hizo ziweze kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara za Vijijini;

(iii) Suala la shule za Sekondari kukabidhiwa kwa Halmashauri za Wilaya liangaliwe na litekelezwe kwa umakini ili kuepusha matatizo ya uendeshaji. Sambamba na hilo Kamati inaishauri serikali itenge fedha za kutosha ili kuepusha matatizo hayo;

(iv) Halmashauri za Wilaya ziendelee kutafuta na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya gharama za uendeshaji;

(v) Mikoa ihakikishe kuwa vikao vya RCC vinaendeshwa kwa wakati kwa mujibu wa Sheria ili kusaidia kuondoa matatizo mengi yanayozikabili Ofisi za Wakuu wa Mikoa kwa ujumla. Aidha Wizara ifikirie wazo la kuwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya RCC;

(vi) Agizo la Serikali la kulifanyia ukaguzi soko la Kariakoo litekelezwe kwa haraka ili kuweza kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya muda mrefu yanayolikabili soko hilo;

(vii) Serikali iyatafutie ufumbuzi matatizo ya muda mrefu ya Shirika la Elimu Kibaha, likiwemo lile la Chuo cha waganga kilichopo hapo. Aidha Shirika hilo litengewe fedha za kutosha katika bajeti ijayo ya mwaka 2010/2011 kutokana na umuhimu wake kwa Taifa; na

(viii) Serikali ihakikishe kuwa inasimamia na kukamilisha ujenzi wa Daraja la Godegode lililopo Mpwapwa kwa kipindi cha mwaka huu wa Fedha 2009/2010 ili liweze kutumika na kuondoa kero kwa wananchi wanaolitumia daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Pili, napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushirikiano mkubwa alioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tatu, natumia fursa hii, kuwashukuru Mheshimiwa Philip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Celina O. Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo na Maafisa wake, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa kwa Kamati na kuiwezesha kuwasilisha maoni yaliyoboresha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makisio haya ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka ujao wa fedha wa 2009/2010. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali za Sekta za Utumishi wa Umma, Mikoa na Halmashauri, ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa, Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Juma Omar, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa; bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Ramadhan

Abdallah na Ndugu Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha kuwa, maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), jumla ya Sh. 221,525,048,500 na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, jumla ya Sh. 2,415,288,422,000, kama yalivyowasilishwa na watoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, ni zamu sasa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini baada ya kusoma hotuba yake, naruhusiwa kuzingatia mambo haya kabla:-

Natoa tahadhari kuhusu baadhi ya mambo ambayo yanakiuka kabisa Kanuni zetu na kwa maana hiyo, nitamsihi katika mambo haya ama asiyasome au sijui atafanyaje sasa, maana yake anakiuka Kanuni na huyu ni Mbunge mzoefu. Nitatoa mifano, ukurasa wa 15, sentensi ya mwisho anasema; "Udhaifu wa Serikali yenyewe kuanzia kwa Mkuu wa Nchi." Hii ni kinyume na Kanuni ya 64(1)(e) nitainukuu: "Mbunge hatazungumzia mwenendo wa Rais, inatajwa hapa; Mkuu wa Nchi ndiyo Rais, kwa hiyo, kumtaja Mkuu wa Nchi na kusema nchi yetu imekuwa kichwa cha mwendawazimu na kisicho na mwenyewe, maamuzi ya kiutawala hayafanyiki, inaafiki Kanuni mbili; 64(e) ambayo hairuhusu kuzungumzia mwenendo wa Rais isipokuwa kwa hoja mahususi, kama kuna hoja iletwe. Pia inaathiri Kanuni ya 64(1)(g), hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. Mimi nimeamua hiyo ni lugha ya kuudhi sana, kusema hakuna maamuzi yoyote na hali hii ni Serikali haipendezi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye ukurasa wa 16, naomba ayaone hayo ili ayaache tu kwa sababu nadhani kama Serikali watasimama kusema yapo kinyume cha Kanuni, uamuzi wangu utakuwa mwepesi. Ukurasa wa 16, yanazungumziwa Mashirika ya *TCRA* na *TCAA*, nimekabidhi Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG)*, kwa Kamati ya Mashirika ya Umma ili wayafanyie kazi mambo haya; kuyaleta sasa hivi ni kukiuka Kanuni ya 53(8) inayosema: "Mbunge yeyote hataruhusiwa kuwahisha shughuli za Mkutano huo unaoendelea, isipokuwa kufuata masharti ya Kanuni hizi au kuwahisha shughuli ambayo itazingatiwa katika Mkutano unaooendelea." Nimeomba Kamati ya Mashirika ya Umma, izingatie Taarifa ya Kamati ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuhusu mambo mbalimbali ambayo yameorodheshwa kwenye Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu. Hayo yanahusu pia ukurasa wa 17; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na pia yanahusu Kiwira ukurasa wa 26.

Waheshimiwa Wabunge, Kiwira katika orodha ya shughuli za Serikali, imepangwa kuzungumzwa Jumatatu tarehe 27 Julai, 2009; kwa hiyo, kuzungumzia Kiwira sasa, nayo inapingana na Kanuni ya 53(8), kwa maana Mbunge anataka

kuwahisha shughuli ambayo tayari imekwishapangwa kuzingatiwa katika Mkutano huu huu. Licha pia ya jitihada ya kujaribu kumzungumzia Rais Mstaafu, hayo yote nadhani asubiri tu. Tafsiri yake ya kisheria ni kwamba, kinga ya Rais Mstaafu siyo *absolute;* hayo ni mawazo yake hatujayapata kutoka kwenye Mahakama yoyote. Kwa hiyo, mtu hawezi kuleta mawazo yake akasema anavyoona yeye ndiyo iongoze shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dokta Slaa, kwa tahadhari hizo, nakuita sasa usome maoni yako ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakupongeza kwa namna mnavyojali kazi na heshima ya Bunge na kuzingatia Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya Kanuni Namba 68, tupate mwongozo wako kwanza, kwa kuzingatia maelezo uliyoyasoma hapa, Mheshimiwa Mbunge, anataka kutumia Chama cha Upinzani kukiuka Kanuni za Bunge na Kanuni zilizokiukwa ni Namba 64(e), 64(j) na 53. Tunaomba mwongozo wako, kwa maoni yangu, nafikiri taarifa yote ingefukuzwa kwa sababu imekwishakuwa *tabled* Mezani. Kwa hiyo, hata tukisema asisome, amekwishai-*table* Mezani na imesambazwa. Kwa hiyo, ombi letu ni kutaka uamuzi wako kwamba, taarifa yote ifukuzwe. *(Makofi)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tukifanya hivyo tutakuwa tumekosea, kwa sababu baadhi ya sehemu amejadili hotuba na isitoshe katika utaratibu mzima wa kujadili hotuba yoyote ya makadirio ya fedha, lazima maoni ya Upinzani yawepo; haikamiliki bila ya maoni ya Upinzani; vinginevyo, itabidi tuahirishe Bunge ili tukazingatie upya suala hili ambalo siyo la kawaida.

Mimi nadhani nimekwishatoa mwongozo wangu kwamba, asome taarifa bila kukiuka Kanuni za Bunge, yapo maeneo ya kawaida anaweza kuendelea nayo hayo mengine hayawezi kusomwa. Ile ku-*table* tu Mezani, haitoi uhalali kwa *Hansard* kufuatilia. Kwa hiyo, yale yote yanayokiuka Kanuni, hayataingia kwenye *Hansard* na kwa hiyo si Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa njia hiyo, nadhani tutakuwa tumelinda uhuru wa Wabunge humu ndani, lakini pia tumetii Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dokta Slaa endelea.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa Mwongozo ulioutoa. Niombe tu kwa masikitiko kwamba, taarifa nyingine ambazo kwa bahati mbaya ulikuwa umeandika sisi hatukuwa tunajua. Kwa hiyo, tunapoandaa hatujui kama kuna kitu kimeshatolewa; na kwa kuwa haikuwa kwenye *0rder Paper,* hatukujua kama kuna barua zimeshapelekwa kule, lakini mwongozo wako sitaukataa ila pale utakapoona nimezungumza kwa kupitiwa, kwa kuwa hatukuwa tumeandaa hivyo, basi nitaomba unikumbushe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha, 2009/2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 99(3)(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru sana wananchi na wapiga kura wangu wa Wilaya ya Karatu, ambao daima wameendelea kuniunga mkono wakati wote, kwa njia mbalimbali na hasa kwa mshikamano wao wa kuijenga Wilaya yetu, kiasi leo tunajivunia maendeleo makubwa yanayoonekana baada ya miaka kumi ya Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kuongozwa na CHADEMA. Nawashukuru sana na hasa kwa kuionesha Tanzania nzima kuwa, kumbe maendeleo yanawezekana hata bila ya CCM. Nachukua fursa hii kuwahakikishia kuwa, nitaendelea kuwatumikia kwa akili, moyo na uwezo wangu wote katika kufanya yale yote tuliyocheleweshewa kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Watanzania wote, kutoka kona zote za nchi, wenye mapenzi mema ambao kwa maelfu, wameendelea kutuunga mkono na kujifunza kutoka Karatu katika jitihada zao mbalimbali za kujiletea maendeleo. Kwa wapenzi wetu wote, Mwenyezi Mungu, awarudishie mara mia kwa upendo wenu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa nimekosa fadhila iwapo sitatoa shukrani kwa Chama changu cha CHADEMA, ambacho ndiyo kimeniwezesha kufika hapa Bungeni. Vilevile natoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani, wakiongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa msaada walionipa wakati wote wa maandalizi ya Maoni haya ya Kambi ya Upinzani. Aidha, napenda kuwapongeza sana Wananchi wa Busanda, ambao walitupigia kura nyingi katika uchaguzi mdogo wa Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mheshimiwa Celina Kombani Mbunge, Mawaziri wa Nchi, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu, kwa kuandaa Bajeti hii wakisaidiana na Wataalamu wao wote.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa shukrani iwapo sitakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, awajalie hekima na busara na kuwapatia nguvu na afya mnazohitaji katika kuliendesha vizuri Bunge letu, hasa katika kipindi hiki kigumu katika historia ya nchi na Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya nne tangu Serikali ya Awamu ya Nne iliposhika uongozi wa nchi yetu; na ya pili tangu Mheshimiwa Pinda kuwa Waziri Mkuu. Kambi ya Upinzani, pamoja na mapendekezo yake kuhusu Bajeti na namna ya kuondoa utegemezi katika Bajeti ya Serikali, kwa kupendekeza vyanzo vipya iwapo Serikali

ingelivizingatia, inatoa maoni yake kuhusu hotuba hii kwa kufanya tathmini ya Malengo na Mwelekeo wa kazi za Serikali katika vipindi mbalimbali vya nyuma, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kipindi walichoshika madaraka.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii ndiyo kipimo na kigezo kikubwa, kujua kama Serikali inatekeleza malengo yake kama yalivyopangwa au laa. Kigezo muhimu cha kujua kama mtu anaendelea ni kupima alikotoka na aliko leo, na hasa kwa kutathmini mihadi mbalimbali ya Serikali na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele katika bajeti yetu; Bajeti yetu bado ni tegemezi, siyo kwa mipango ya maendeleo tu, bali pia kwa uendeshaji wa Serikali yenyewe (*Recurrent Expenditure*). Utegemezi huo mwaka huu ni zaidi ya asilimia 33.45 ya matumizi yote ya Serikali. Hii ni hali ya hatari sana. Baada ya kuona kila mwaka Bajeti yetu ni tegemezi, Kambi ya Upinzani, imefanya utafiti kuona kama kweli matumizi yetu yanakwenda kwa misingi ya vipaumbele au tunatumia tu fedha. Ugunduzi wetu ni kama ifuatavyo:-

(i) Wakati tunakopa fedha ndani na nje na kuwategemea wahisani wetu wa Kibajeti, Kambi ya Upinzani imegundua kuwa, mwaka huu Serikali imeanzisha kasma mpya inayoitwa *personal allowances-in kind*, yaani ya aina; ni mara ya kwanza neno *in kind* linatumika. Tumechunguza maana yake nini kwani kwa kawaida Serikali haina malipo yoyote *in kind*, yaani ya aina, bali hulipa fedha taslimu kwa kuwa ndiyo aina ya malipo pekee yanayoweza kudhibitiwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, uchunguzi wetu umegundua kuwa, kasma ndogo ya 210500 inatumika kulipia chakula na viburudisho.

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kupitia kila Wizara na kila Idara ,kujua fedha hizi ni kiasi gani kwa ujumla wake na uwiano wake na Wizara au Idara nyingine za Serikali. Kama hesabu zangu ni sahihi, kiasi cha jumla kwa kasma hii inatisha kwani ni shilingi 19,963,429,490.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika - Kuhusu Utaratibu. Kanuni ya 64, lakini nataka nitumie Kanuni ya 68, kuhusu hili ambalo Mheshimiwa Mbunge analitaja chini ya kasma 210500, ambayo ipo katika kila kasma na yeye anaitaja kana kwamba ni chakula. Mimi kama Mratibu wa Shughuli za Serikali, nimewasiliana na Kamishna wa Bajeti, kifungu hiki siyo cha chakula. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge athibitishe kama kifungu hiki kinatumika kwa chakula.

**SPIKA**: Labda Mheshimiwa Waziri utusaidie tulimalize; ni cha nini sasa ili tujue? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana ni kwamba, huku mbele ameendelea na kuituhumu Serikali kuhusu vifungu mbalimbali ambavyo tafsiri yake ni tofauti na hali

halisi katika matumizi ya Serikali. Kifungu hiki hakitumiki kwa chakula na haya ndiyo maelezo ya Kamishna wa Bajeti.

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri wa Nchi TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kufafanua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hiyo *personal allowance in kind*, katika vitabu vyetu ina maana kwamba ni fenicha, friji na vitu kama hivyo na siyo chakula, chakula kina fungu maalum. Kwa hiyo, labda angeangalia vizuri zaidi akapata ufafanuzi wa kina zaidi na hizo ziko kwenye stahili za viongozi; kwa mfano, mimi lazima ninunuliwe friji na fenicha. Kwa hiyo, nikinunuliwa fedha zimewekwa kwenye fungu hilo. Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na kadhalika, wana haki ya kupata vitu kama hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA**: Nadhani Mheshimiwa Dokta Slaa inajijibu yenyewe, kwa sababu binadamu hatuli viti, hatuli mawe, hatuli friji; huo ndiyo ufafanuzi. Kwa hiyo, nadhani hesabu yako ungeiondoa, haihusiki kabisa.

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, Bungeni tunafanya kazi kwa nyaraka, mimi nimetumia kitabu cha randama tena ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyowasilishwa ofisini kwako na Mheshimiwa Marmo juzi. Sasa watuletee kitabu.

Kanuni ya 63(4), inataka anayetuhumu asijibu kwa maneno na kifungu hicho nilichotumia kinafanana kabisa katika randama walizowasilisha, kwenye kitabu kikubwa haionekani na hutaweza kuigundua kwa sababu wameweka jumla. Mimi nimepitia kila kasma, baada ya kupata kwenye randama zao, sasa wawasilishe hapa randama zao halafu tuone kama sivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 63(4). *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Dokta Slaa, Kanuni ya 63(4) inasema hivi; Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii; atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge. Sasa wewe unayeng’ang’ania kwamba, hii lazima ni chakula uko katika *disadvantage*, kwa sababu wanamnukuu Kamishna wa Bajeti. Kwa akili ya kawaida, mimi kama kiongozi wa shughuli humu ndani; ni lazima nimwamini Kamishna wa Bajeti, anayenukuliwa kuliko wewe.

Kwa hiyo, bora uyaondoe kwa sasa na tutayashughulikia kwa namna nyingine; itakapogundulika Serikali imedanganya basi ipo namna ya kushughulika nayo, lakini kwa sasa siwezi kukubali hayo yaingie kwenye *Hansard*, yanaleta takwimu nzito, kunywa chai shilingi bilioni 19 na vitu kama hivyo ambavyo sivyo, naomba uyaondoe.

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwa manufaa ya Taifa, nitaacha hicho kifungu lakini hivi vifungu vyote vimejumuishwa kutokana na randama zao; sasa mimi nafikiri kama itakuwa hivyo, baadaye nitafikiria uamuzi mwingine.

**SPIKA:** Jamani amekwishaondoa hivyo.

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ikizingatiwa kwamba, chakula sasa narekebisha hilo tuseme siyo chakula, hata ingelikuwa ni fenicha; nimepiga pia vifungu vya fenicha na kuona kuwa, kila mwaka fenicha inanunuliwa; sasa hilo nalo linahitaji maelezo, lakini niliache kwanza.

Mheshimiwa Spika, nilinganishe tu jumla ya fedha ambazo zimetajwa katika kifungu hicho ni shilingi 12,052,171,000, lakini ninataja hili kwa sababu nalinganisha na Mahakama Kuu zote nchi nzima, ambayo ina shilingi 17,884,425,000 tu; Mahakama za Wilaya na za Mwanzo nchi nzima zimepewa shilingi 10,289,826,000; Ikulu imepewa 7,329,345,000 tu; Ofisi ya Waziri Mkuu shilingi 5,461,028,000; Msajili wa Vyama vya Siasa anayehudumia vyama vyote vya siasa shilingi 19,955,620,000; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepewa shilingi 17,400,689,000; na *Court of Appeal* imepewa shilingi 9,680,143,000 tu.

Mheshimiwa Spika, tunachoangalia hapa ni kuangalia kama *priorities* zetu za bajeti zinaenda sawa, ndiyo msingi wa hoja yangu na Bajeti ni uchambuzi; sasa ninaambiwa nisichambue basi nitakubali kwa sababu ni maelekezo yako.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa kasma ya malipo ya *allowance* ya binafsi *(personal allowances-in kind*), Kasma ya Takrima *(Hospitality)* nayo ina jumla kuu ya shilingi 10.923,026,875. Nimepita kila kasma na nimejumlisha, anayekataa kama Kasma hiyo ya *Hospitality* kwenye vitabu si sahihi, basi nafikiri ni vizuri alete mahesabu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU, NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika - Kuhusu Utaratibu. Siyo vyema kumkatisha Mheshimiwa Mbunge namna hii, lakini pia tukumbuke hapa hatupo kwenye Mkutano wa Hadhara wa Vyama vya Siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kasma hizi ni nyingi sana, kwa Halmashauri za Wilaya ziko zaidi ya 1500, acha Idara zote za Serikali; iwapo Mheshimiwa Mbunge ataendelea kutaja hizi takwimu kwa kupotosha Bunge lako na kuupotosha umma, hivyo matumizi mabaya ya Bunge ataje kifungu hiki 2206000 ambayo inaitwa *clothing, bedding and footwear services*, apite kila Wilaya atuambie tunataka kununua nini, kwa sababu pia tunanunua; kwani kosa liko wapi kumnunulia mgambo viatu au shati?

Sasa hapa siyo kwenye mkutano wa siasa, kwa hiyo, matumizi haya ni halali na mimi ningeomba sana Mheshimiwa Spika, Bunge lako lisitumike kama jukwaa la kisiasa. Haya ni matumizi halali ya Serikali na Mbunge kama ana uhakika fedha hizi zinatumika vibaya, aende kasma zote ambapo tunatoa vitanda, godoro, blanketi, viatu na tupate hesabu hizi zote; la sivyo hapa ni kwamba, tunalipotosha Bunge, tunawapotosha wananchi na hapa siyo mahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** vivyo hivyo kasma inayofuata ambayo nayo ameitaja 221400; kwa kila kasma ambayo ni *hospitality and supply services*, atutajie pale ambapo anadhani fedha zinatumika vibaya, kwa sababu kila Serikali ni lazima ifanye kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yetu, kinachofanyika hapa ni mkutano wa hadhara, ambao una-*appeal* kwa *sympathy* ya Wananchi wote wa Tanzania. lakini kumbe hapa tunaongelea mambo ya ukweli ambayo yapo katika kila Wizara ya nchi yetu. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kumsikiliza huyu bwana kwa utaratibu huu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, rai ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nilidhani anazungumzia usahihi wa tarakimu, lakini hakufanya hivyo. Sasa hoja ninayoiona anayoijenga Msemaji wa Kambi ya Upinzani ni kwamba, haya hayana kipaumbele. Sasa mimi siwezi kumzuia kuhusu anavyolinganisha vipaumbele, kama yeye kwa maoni yake, Serikali itafuta haki zote za watumishi wasipewe friji, wasipewe kila kitu; hayo ni maoni yake, mimi nadhani tumwache. Hapo tu atakapofika kwenye vifungu vile ambavyo nimevisema, atakuwa anaathiri Kanuni, lakini kwa sasa yeye ana haki zote hizi ambazo zipo kwenye *Standing Order* za Serikali zisiwepo. Yeye angekuwa upande wa Serikali, basi kungekuwa hakuna chai, hayo ni maoni yake, wananchi wana akili wanasikiliza, wataweza kuamua nini kifanyike. *(Makofi)*

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Lengo langu ni hilo, kuonesha vipaumbele vyetu kama ni sahihi au laah, ndiyo maana nafanya uchambuzi, na kwa bahati mbaya vipengele nimetoa kwenye randama, pamoja na vitabu, sasa kama nimekosea kwenye kasma nitaomba nisahihishwe tu.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa, sababu moja kubwa ya wafungwa kusongamana mahabusu ni kesi kutoendeshwa kutokana na kutokuwepo fedha za kutosha katika Idara ya Mahakama. Haiingii akilini mwa mtu yeyote kuwa, Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 10, kiasi cha Takrima, kupewa kifungu zaidi ya Mahakama zote za nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 10 zinatosha kununua angalau magari aina ya Suzuki 364 na huu ni uchambuzi wa bajeti, kwa bei ya shilingi 30 milioni kila moja, kuwawezesha Mahakimu wetu hao kutimiza majukumu yao na kuwafikia wananchi wengi ambao wanapoteza haki zao kwa vile wanashindwa kusafiri mwendo mrefu kuzifikia Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine, Serikali yetu inayosema inawajali wananchi wake, imetumia fedha nyingi zaidi katika Takrima kuliko kutumia fedha kidogo zilizoko angalau kuwafikishia haki wale wananchi wanaohitaji haki zao za msingi. Tungeweza kutengeneza fedha kidogo zaidi, tukaweka kwa wale watu muhimu na yale maeneo muhimu yakabaki na chai lakini siyo kila mahali na chai inamfikia nani ofisini; inawafikia watu wa kada fulani tu siyo watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, mbele ya macho ya kimataifa, Tanzania inaonekana nchi yenye dhamira safi ya kulinda maadili ya viongozi wake na tunaendelea vile vile kuwatetea watu wetu. Ukilinganisha hilo na kifungu cha Sekretarieti ya Maadili, ambayo inalinda haki za Watanzania wote, imepewa shilingi bilioni tisa tu. Kwa maana ya kwamba, nikilinganisha na kifungu kile bado na wao wamepewa chini, sasa tunajiuliza kama tunaweka kipaumbele kwenye hii chai na Takrima au chochote tutakachoita, lakini chombo muhimu kama Sekretarieti ya Maadili tunashindwa kukihudumia; nafikiri ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ripoti ya Sekretarieti wameonesha kazi walizofanya maeneo waliyotembelea na hivyo hivyo kwa Tume ya Haki za Binadamu, sasa tunajiuliza; je, kwa nini hawa watu wanashindwa kufanya kazi yao? Wanashindwa kwa sababu hatukuwatengea fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, ni hivyo hivyo kwa *Law Reform*, kazi zao ziko nyingi, kuna sheria zimepitwa na wakati, kwa mfano, sheria yetu ya kumlea mtoto aliyepatikana nje ya ndoa; mpaka leo ni shilingi mia moja. Sheria hiyo ni ya tangu miaka ya 1960 hatujairekebisha. Tume hii imepewa shilingi bilioni 1.3, nalinganisha bado na ile taarifa ambayo tumeipata kwa upande ule mwingine.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi, ambayo pamoja na kazi zake ni kufanya ukaguzi wa maeneo ya Kazi husan viwanda, mazingira ya kufanyia kazi hususan nyumba wanazoishi wafanyakazi wetu kwenye maeneo mbalimbali, hali yao si nzuri na hii ni kwa sababu hela waliyopewa Wizara hii ni shilingi bilioni tisa. Haziwawezeshi kufanya ukaguzi kwenye maeneo yote wanakofanya kazi wafanyakazi wetu. Ipo Sheria ya *Inspectorate* katika Wizara hii, lakini kwa kuwa wana shilingi bilioni tisa, yote imeelekea kwenye zile kazi nyingine; ile kazi ya kukagua imekuwa sio muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokuwa tunasema, takwimu zinaonesha kitu kimoja tu; nacho ni kukosekana kwa umakini katika kupanga vipaumbele; kusimamia maandalizi ya bajeti au kwa makusudi kabisa kuwa na matumizi yanayotulenga sisi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri inaelekea wazi kuwa, kwa bahati mbaya, inawezekana wenzetu hawayakuyajumlisha kama mimi nilivyoyajumlisha. Ukiyatazama kwenye kasma moja moja, hutastuka, hutaona kama ni nyingi, lakini kaa chini jumlisha zote, ndio tunaona kuna uzito mkubwa sana. Kasma niliyosema ya mavazi, mimi pia ninaelewa kuna Wizara inashughulika na jeshi; tunajua mavazi, tunajua matandiko, tunajua vitanda pale vina kazi; lakini tunapokuta kwenye kila Wizara tunajiuliza; hawa ni

akina nani Wizarani!  Ingekuwa kwenye Halmashauri naelewa kuna mgambo; huko Wizarani tuna nani?

Tuna watumishi wachache walioko, tuna walinzi, lakini kwa kila kasma inaonekana ni fedha nyingi. Sasa kama watu watasema sio nyingi, basi hili ni suala lao, lakini mimi naona ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ndio msimamizi na Bunge letu ndio msimamizi na mtekelezaji. Bunge letu ndiye msimamizi wa mipango yote ya Serikali.  Ninayasema haya kwa kutumia mamlaka tuliyopewa, sisi kama Kambi ya Upinzani; lakini vilevile sisi kama Bunge, tunatakiwa kusimamia matumizi ya Serikali. Huwezi kuyasimamia kama hukuyachambua, ndio maana ninapozungumza kuchambua; ni lazima tuwe na taarifa, tuziweke hadharani, ndio tuweze kuiona Serikali inafanyaje kazi.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea Serikali itatujibu, lakini naona inaenda mbali zaidi.  Tungeweza kutumia fedha hizi kidogo tulizonazo, kwa mfano, tukanunua pikipiki, kwa ajili ya Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, ambayo imetawanyika katika vijiji vyote. Mara nyingine ni zaidi kuliko hata Wizara ya Afya, kwa sababu zahanati kwa sasa haziko kila mahali. Watendaji wetu hawa, tumewaacha.  Ungenunua kwa fedha hizi pikipiki, shilingi bilioni sita tu zingetosha kuwanunulia Kata zetu zote 2500. Wakapata fedha za kufanya kazi, wakaweza kutembea, wakaweza kufanya kazi zile za kimaendeleo, ambao wao tunawaona kama ni *engene* ya maendeleo. Kwa kuwa hatukuwapa hizo fedha, hawa watu wanakaa vijijini na sisi wengine ambao tunakaa vijijini tunajua, wanakaa na tunawalipa.

Kimsingi, tunaweza kusema tunawalipa bila tija yoyote tunayopata. Tungeelekeza vipaumbele vyetu, Wizara hii tungeisaidia.

Mheshimiwa Spika, ndio maana nimefika mahali nasema, kimsingi kwa bajeti hii, kwa fedha walizopewa; sioni tena tija hata ya kuwa na Wizara.  Nafikiri watu wa Maendeleo ya Jamii, wataona kwamba ni kweli fedha ni kidogo sana.  Wanashindwa kufanya kazi. Sasa tukisema hili, sio kwa sababu tunataka kuwasema vibaya.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda wangu ulichukuliwa na sijui sasa muda wangu ni kiasi gani, nguvu yangu katika maeneo ambayo ulisema kwamba nisiyaseme, sasa yale maeneo yote, naona nimeyaruka.  Kimsingi, Taarifa ya CAG ikitolewa ni *public document* na kama hakuna *Order Paper*, tulitakiwa kuijadili. Mimi nakubali kwa sababu ni mwongozo wa Spika na sitaki kubishana na wewe.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa haya mengine hukuyasema, kwa mfano, tuna malalamiko makubwa kwenye mashirika yetu; na Serikali pamoja na Bunge ndio tunasimamia haya mashirika vilevile. Kwa mfano, Shirika la Hifadhi la TANAPA, ambalo katika usimamizi, Taarifa ya CAG, inaonesha kwamba, wametumia fedha nyingi. Kiasi cha fedha kilichotumika; kwa mfano, shilingi bilioni nne zimetumika kinyume na Sheria. CAG anasema sio Dr. Slaa.

**MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO:** Mwongozo wa Spika. Kifungu cha 68(10).

**SPIKA:** Ndio Mheshimiwa Diallo.

**MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO**: Mheshimiwa Spika, msemaji anayeendelea kuzungumza, anazungumzia kitu ambacho umekitolea maamuzi. Uwamuzi wa Spika, kuhusu suala lolote la utaratibu, utakuwa ni wa mwisho. Sasa ulieleza kwamba, Taarifa ya CAG imepelekwa kwenye Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Nadhani ile ndio ilikuwa *ruling*, sasa yeye anaanza kurudia. Naomba mwongozo. *(Makofi*)

**SPIKA:** Ni kweli Waheshimiwa; TANAPA ipo katika mtiririko huo huo; ni sehemu ya zile taarifa ambazo zimepelekwa kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma na tunasubiri taarifa yao. Kwa hiyo, halina haja ya kujadiliwa hivi sasa. Kwa mujibu wa Kanuni ya 37(8). *(Makofi)*

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini ni mara ya kwanza tunajadili, halafu tunaacha kujadili, ku-*quote* kule. Tutaona wakati wa mjadala mzima, tuone kama haki itatendeka kiwango gani. Naruka sehemu zote hizo, lakini ukweli ni kwamba, sisi pia hatukuwa tumeona, hatukujua kama kuna barua, kwa hiyo, tuliandaa tukijua ni utaratibu wa kawaida.

Kwa hiyo, naomba radhi kama itakuwepo humo, lakini ninachozungumzia ni kwamba, usimamizi wa Sheria katika vyombo vyetu, katika maeneo yetu mbalimbali na katika Serikali na tumeona katika Serikali Kuu pia CAG ameisema, tunafanya manunuzi ambayo hayakufuata Sheria. Ndicho tulichokuwa tunakizungumza katika eneo hili, pamoja na kwamba, hata taratibu za kibodi nazo zilikuwa hazifuatiliwi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, rasilimali zetu na fedha zetu, kwa hali hii, itakuwa ni vigumu kuzijadili sisi kama Bunge, kwa sababu kwa Taarifa za CAG, ndio mwongozo wetu. Kwa sababu umetoa mwongozo, sitaki kuliingilia naliacha ili tuweze kuliona.

Naomba nizungumzie kidogo kuhusu suala la rushwa, ikizingatiwa kuwa kwa muda wa miaka miwili sasa, Taifa letu ndani ya Bunge hili Tukufu, kwenye mikutano ya hadhara, kwenye vyombo vya habari; na Mbunge anaruhusiwa kuzungumzia kitu kilichoko kwenye vyombo vya habari na taarifa mbalimbali za ubadhirifu, ufisadi, wizi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sitazungumzia masuala yaliyoko mahakamani, lakini ninataka Serikali ituambie katika haya ambayo hayako mahakamani; ni utaratibu gani; hatuingilii undani wa mahakama, tunataka kujua taratibu gani zinafuata. Ningependa

Waziri Mkuu, atujibu katika majibu yake baadae haya yote ambayo tumeya-*raise*, lakini Serikali nadhani itakuwa na majibu.

Mheshimiwa Spika, bajeti inatumika na Serikali kupanga matumizi ya fedha kidogo zilizoko maeneo na sekta muhimu zinazohitaji kipaumbele na wananchi wote kwa ujumla. Hivyo; ni kweli kuwa, bajeti ni silaha na chombo muhimu sana katika kutoa dira ya utendaji kazi katika Taifa. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani ina maoni kuwa, kupanga ni kitu kimoja na kutumia ipasavyo kilichoidhinishwa ni kitu kingine. Hii tunaisema hivi, kutokana na mtiririko mzima kwamba, Sheria zimekiukwa, tunategemea zitachukuliwa hatua kwa wale watakaotakiwa. Tutakapokuja wakati huo, tuta-*demand* kujua ni hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika wote hao.

Mheshimiwa Spika, labda niende kwenye eneo lingine; tunafahamu kwamba, vyombo vya habari vilisaidia sana katika kueleza jinsi ufisadi ulivyokuwa umeenea katika nchi yetu. Napenda kutumia nafasi hii, kuvipongeza vyombo vyote vya habari, jinsi vilivyosimama kidete na kueleza na kwa sasa hatua imeanza kuchukuliwa. Nadhani demokrasia inapaswa kupimwa kwa vigezo vya namna hiyo. Pamoja na hiyo, tungependa kusema vitisho vya aina yoyote kwa vyombo vya habari, vinauwa demokrasia ya kweli na vinarudisha nyuma, utaratibu wote ule wa kusaidia demokrasia katika nchi.

Mheshimwa Spika, suala zima la umaskini katika nchi ni lazima tulizungumzie na lazima lipatiwe ufafanuzi wa kina na Waziri Mkuu. Leo asubuhi, Mheshimiwa Waziri, alijaribu kujibu, lakini hatukuridhika na majibu yale. Serikali ituambie kuna utaratibu gani na mkakati gani wa makusudi wa kusaidia Watanzania wetu waweze kuondokana na umaskini? Hapa ninatoa mfano; tukubali kuwa, katika tafsiri iliyoko kwenye vitabu vya Serikali; juzi Waziri alisema kuna taarifa mbili tofauti, kama taarifa zinagongana kwenye vitabu viwili vya Serikali, sio kazi yetu sisi Wabunge, wala sio kazi yetu Wapinzani kuamua ni kipi sahihi. Kwa sisi tutatumia kile ambacho tumetoa kwenye Taarifa ya Serikali. Umaskini unaonesha kwamba unapungua; kiwango kinapimwa kwa kutumia shilingi 641 katika Jiji la Dar es Salaam, 532 katika miji mingine na 465. Hata kwa namna yoyote ile, mtu ungempa shilingi 641, hawezi kunywa chai asubuhi, hawezi kula chakula cha mchana, hawezi kula mlo wa jioni, akapeleka mtoto shule, akanunua nguo, akaenda hospitali. Ndicho tunachokieleza kwamba, sisi ni lazima tukubali kwamba, tunahitaji mjadala mpana zaidi wa kuangalia umaskini wetu badala ya kusema unapungua, kwa kiwango kile ambacho Waziri alisema; mtu anayehesabiwa sio maskini ni yule ambaye anapata zaidi ya dola moja kwa siku.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali ije na majibu sahihi ya kuwatoa Watanzania kwenye lindi hili gumu la makali ya maisha ya Watanzania. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aje na majibu hayo. Wananchi wengi wameacha kunywa chai, kwa taarifa ambazo wanatuletea, kwa kuwa sasa sukari ni shilingi 1200 maeneo mengi ya Tanzania. Mikate iliyokuwa kimbilio la walala hoi hasa mijini, imekuwa haishikiki tena, kwa vile bei inakimbilia shilingi 1500, nyama inazidi kuwa hadithi, kwa sababu kilo moja sasa ni shilingi 4500 katika maeneo mengi. Mchele ambao ni chakula cha Watanzania wengi ni shilingi 1500. Sasa tunajiuliza; kwa kipato hiki

ambacho tumeambiwa ni chini ya dola moja, wananchi hawa wangapi wanaweza kula nyama, wanaweza kununua mchele na mikate?

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima katika hili ije na majibu, ambayo yatakuwa ya wazi na hayatakuwa na utata. Watu wengi kama nilivyoeleza, walikuwa wanaongelea masuala ya Mheshimiwa Rais Mstaafu, umesema nisiyazungumze, lakini nilikuwa ninasema nyaraka zote tulizozitoa zinajionesha. Kwa hiyo, Serikali itakapokuja, itoe maelezo kwa nini nyaraka hizi ambazo ni za Serikali nazo zinatia utata? Iweje tuwe na utata katika maelezo; nyaraka za Serikali zinaonesha yale tuliyokuwa tunayasema?

Mhesimiwa Spika, ninaruka maeneo yote yale ambayo ulikuwa umeyasema, lakini sina uhakika kama *Deep Green* ipo katika maelekezo yako, sikuiona na Waziri hakujibu asubuhi? Tungependa sisi kujibu *Deep Green* hii ambayo tuna kigugumizi nayo ni nini; na kwa nini Waziri Mkuu kwa mfano alikuwa mkali sana kwenye suala la DECI ambayo ni halali awe mkali kwa sababu Sheria ilivunjwa? Kwenye hili na taratibu sasa zimevunjwa. Deep Green na TANGOLD zote zime-*operate* katika nchi miaka minne kabla hazijasajiliwa. Hivyo ndivyo walivyofanya hawa wa DECI. Ukali ule wa Waziri Mkuu, usiishie kwa DECI, uende pia kwenye haya makampuni ambayo nayo yamekiuka Sheria hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninaruka mengi kwa sababu ya maelekezo yako ya hapa, lakini swali la KAGODA nalo haukulitolea maelezo, sina uhakika kama nalo lipo? KAGODA ninavyojua halipo Mahakamani na kwa kuwa haliko mahakamani naomba nilizungumzie.

Kwa kuwa Serikali imepata kigugumizi kuhusu ufisadi uliofanyika kupitia Kampuni ya KAGODA, Kambi ya Upinzani imelazimika kueleza kwa kirefu tena kilichojiri kupitia KAGODA. Taarifa mbalimbali zilizoko katika kampuni hii na sura ya ufisadi inayoonekana wazi; Kampuni ya KAGODA imesajiliwa ikapata Hati Namba 54040, tarehe 29 Septemba, 2009. Wote walioandikwa katika Hati hiyo wanaoitwa *promoters*, taarifa zote tunazopata kwenye vyombo vya habari ni utata kama *plot* hiyo haipo na kwamba hao watu hawapo. Sasa tunataka Serikali ituambie ni nani hawa; na kama hawajulikani, Wizara ya Ardhi iliwahi kutoa Plot Namba kwenye magazeti, hawajakanusha ilisema kwamba hiyo Plot Namba iliyosemwa haipo; sasa kama utata huo upo, Serikali iliyosajili kampuni na Plot Namba, inatueleza nini Watanzania? Kwa maana hiyo, ardhi yetu inaweza kuuzwa siku nyingine kwa kutumia *documents* ambazo wala sio halali. Kwa hiyo, tunapenda tupate taarifa ya jambo hilo na kwa kuwa haliko ndani, basi nadhani halina utata wowote.

Mheshimiwa Spika, leo ni takriban miaka minane, tangu Kambi ya Upinzani ilipopinga uamuzi wa kinachoitwa ununuzi wa rada ndani ya Bunge hili hili na tukazomewa tulipotoka nje. Kwa hiyo, ninalisema nikiwa kifua mbele, kwa sababu tulichopinga wakati ule, leo kimekuja kuonekana kama ni tatizo katika nchi. Nina hakika, baadhi ya haya ambayo leo wenzangu wanayakataa, yatakuja kuwa hivyo hivyo. Sasa miaka minane baadae, Kambi ya Upinzani inaona fahari kubwa. Tulichokisema sio tu kimeelekea kuthibitika, lakini imekuwa ni hadithi dunia nzima na imehusishwa na

kitendo kikubwa cha ufisadi, rushwa au wizi wa mali ya umma. Ufisadi huo umejadiliwa ndani ya Bunge la Uingereza, mara kadhaa na uchunguzi kuanzishwa na shirika la kwao la SFO.

Sasa sitaki kuingia kwa undani, lakini *documents* zinajionesha, tunachohitaji kujua sisi kama Watanzania ni kitu gani? Fedha zilizoibiwa ni za kwetu, kama ziliibiwa; kama kuna ufisadi ulitokea katika hela zetu. Wakati Uingereza wanachunguza SFO, sisi tunachukua nini? Mfano, Marekani wametajwa tu kwenye gazeti, kesho yake wakaanzisha upelelezi, sisi kwetu tumekaa na Bunge letu wala hatuliarifu. Hii si ishara nzuri ya Utawala Bora wala Utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, suala la *commodity import support*, kule mwanzo nilipolitaja na watu wengi hawakuelewa, nililitaja Novemba 2007 wakati nahojiana na Gazeti la *The East African* nikiwa Mangola Kijijini kabisa. Nilichokisema sio hiki kinachofanywa sasa na Serikali. Kinachofanyika ambacho kimetangazwa kwenye magazeti ni kuwadai wale waliokopa. Mimi nilichokuwa nazungumzia ni aina ya ufisadi uliokuwepo kupitia *commodity import support.*

Mheshimiwa Spika, taarifa tulizonazo, makampuni 980 yalianzishwa kupata hiyo fedha, lakini kati ya hizo, kampuni moja tu ambayo tuna rekodi yake *proper*, ina zaidi ya makampuni hewa 35. Sasa tunajiuliza; tusipojadili haya mambo na Serikali ikatupa taarifa, tunasimamia nini katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, hali ya siasa nchini; kila kukicha, kuna taarifa ya mgomo kwenye shirika na kadhalika. Nadhani hii yote tunajua. Sasa tukizungumza amani na utulivu; ni kuhakikisha hali hii ya amani na utulivu kweli inakuwepo. Migomo haitakuwepo Vyuoni wala kwa wafanyakazi na wala wafanyakazi wetu hawanyanyasiki kwa namna yoyote ile na haki zao wanazipata. Taarifa ya Tume ya Haki za Binaadamu, iliyozunguka katika zaidi ya Mikoa kumi na imekwenda kwenye Wilaya zaidi ya 82, imeonesha haki hizo zimevurugwa, zimekanyagwa na zimenyanyasika. Taarifa ya Tume ya Binaadamu sio ya Dr. Slaa wala sio ya Kambi ya Upinzani; ni ya Serikali. Tunataka kuihoji Serikali imechukua hatua gani katika Taarifa hiyo, ambayo sasa wanayo zaidi ya mwaka mmoja wakati Watanzania wetu wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, haiishi hapo, manyanyaso hayo yamejitokeza kwenye sura nyingi za Kisheria. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nitaomba anipe ufafanuzi wa kina katika hili baadae. Kijiji cha Matuhi, Wilaya ya Kiketo, tarehe 11 Juni, 2009 katika Mkutano Mkuu wa Kijiji, Wananchi walimjadili Mwenyekiti wao ambaye walikuwa wanamtuhumu kwa wizi wa shilingi milioni saba au ubadhirifu wa shilingi milioni saba, kwa sababu bado ni tuhuma. Taarifa hiyo ikasomwa na wakaamua kumsimamisha kwa kutumia kifungu cha 141 cha Sheria ya Serikali za Mitaa Namba 7 ya Mwaka 1982. Mkutano ukateuwa Kamati ya Muda, *DC* akaenda kule akaridhia yale maamuzi; akamtuma Mkaguzi wa Wilaya pamoja na *DAS* wakathibitisha wizi wakasoma taarifa kwa wanakijiji wakaridhia. Cha kushangaza, tarehe 18 Juni, Mkuu wa Mkoa, alifika na kufanya mkutano wa ndani, akiwa na maaskari na katika mkutano wa hadhara na akatoa amri ya kuirudisha serikali iliyoondolewa na Mkutano Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 141 kiko *clear*, akiondolewa kiongozi mmoja mmoja au wote kwa kutumia kifungu cha 141, hakuna rufaa popote hata ikienda Mahakani itaingia kwa taratibu nyingine, lakini hakuna mamlaka nyingine ya kawaida. Sheria hii imetungwa na Bunge. Tunazibadili sheria na mifano huko nyuma ilikuwepo, iliyokwisha kutokea. Mfano huu haukuishia hapo; katika Kijiji cha Dareda, Wilaya ya Babati Vijijini, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, alikwenda kwenye mkutano wa hadhara, mwananchi mmoja anayeitwa Jermana, alimtuhumu Kaimu Afisa Misitu wa Wilaya kwa kula na kuchukua rushwa. Katika mkutano huo, Mkuu wa Mkoa alitoa amri ya mdomo ya kumfukuzisha kazi mtumishi huyo; sina ushahidi, inasemekana alisema kwamba, hamtaki katika Mkoa wake. Toka 2007 mpaka leo, mtumishi huyo amesimama. Huu hauwezi kuwa mfano wa demokrasia hata kidogo. Namshukuru sana Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, nilimpa *documents* zote za kesi hii, amechukua hatua na amenirudishia, anasema kwamba ni kweli kuna dalili ya kumnyanyasa huyu raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yako mangapi? Tunayoyapata ni machache tu, yako mangapi ambayo hayajatufikia? Kwa hiyo, ningependa katika hili pia Serikali itusaidie, tunapokuwa na sheria tuzizingatie. Sheria haikutungwa kwa wadogo tu, iwabane na wakubwa na viongozi vilevile. Kule Wilayani Karatu nako njiapanda, tulicheleweshewa shamba ambalo Mheshimiwa Rais alilirudisha, sasa ni mwaka karibu wa nane, Mkuu wa Wilaya mara anaunda Tume, lakini Taarifa ya Tume haipatikani.

Sasa mwisho wa yote, mwananchi ambaye alikuwa anajenga hiyo, aliyekuwa amekusudia Rais ampe *plot* ajenge nyumba wakati bei ya simenti iko shilingi 3000 au 4000, bei ya bati iko hivyo hivyo, leo bei ya bati ni shilingi 18,000, sisi serikali ndio tunaosababisha umaskini wa watu wetu. Tunataka katika haya mambo ya namna hii, Serikali ituambie kuna nini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ya pili au ya kwanza?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hilo. Kwa kuwa muda wangu sikuujua, kwa hiyo, nime-*lose track.*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi vilevile kule *PADEP*, tuna *double standard* katika nchi yetu. Kule Kijiji cha Kanded, Mwenyekiti wa Kijiji, alikodisha shamba ambalo lilikusudiwa kuwa la vijana 240 likakodishwa mkulima mmoja. Shamba hili limefadhiliwa na Mradi wa *PADEP*, kwa taratibu tunazojua, hata Halmashauri ya Wilaya haina mamlaka ya kufanya *re-allocation* bila kibali cha Hazina. Serikali ya Kijiji inafanya *re-allocation*, inabadilisha matumizi, inakodisha shamba kwa mtu binafsi; Mkuu wa Wilaya analinda! Mkuu wa Mkoa tulimpa taarifa, hakuna hatua ambayo

inachukuliwa. Tunaweza kuona mambo ya aina hiyo, yanavyoweza kuleta mkanganyiko katika nchi yetu.

Hii ni mifano michache tu ya maeneo ambayo ninayafahamu au nimeletewa taarifa zake za kina. Ni dhahiri kuwa, viongozi wetu ambao tulitegemea watakuwa wahimili, ndio wanakuwa vinara wa kuzuwia na au kusaidia kupindisha sheria kwa malengo wanayofahamu. Tunaomba Serikali Kuu, isimamie matumikio ya aina hii yasiendelee kuwaumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika chaguzi ndogo mbalimbali, tumeona idadi ya wapiga kura inashuka na kiwango kinachoshuka tumekionesha ukurasa wa 70. Sababu moja ambayo imeelezwa ni shahada kununuliwa na tumeorodhesha idadi, namba za shahada na watu walionunua. Walipelekwa polisi, lakini hawakuchukuliwa hatua. Tumeweka hiyo na nina ushahidi wa kina katika hilo. Kama hiyo haitoshi, vilevile watu wetu wanapigwa; lakini tukitoa ripoti hakuna hatua inayochukuliwa wakati watu wetu wakikamatwa kesho yake wanaachiwa pale pale. Kwa hiyo, tungependa kujua na kama unahitaji ushahidi wa RB na aya R zinazohusika katika suala hilo tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi, suala la uimarishaji wa Serikali za Mitaa. Kwanza, nizungumzie suala la 50% kwa 50%. Nakumbuka kwamba, Mheshimiwa Rais, tarehe 21 alipokuja ndani ya Bunge alisema, kutakuwa na mjadala wa Kitaifa. Kambi ya Upinzani tunataka kuuliza; ule mjadala wa Kitaifa umefikia hatua gani ili tuweze kujiandaa. Najua kila chama kinajiandaa kwa utaratibu wake, lakini tulihitaji utaratibu wa Kitaifa tupate 50 kwa 50. Serikali za Mitaa tunaomba Sheria Namba 7, Namba 8 mpaka 11 zirekebishwe ili ziendane na muda, kwa sababu tunapata matatizo katika utendaji kazi kutokana na sheria hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nitazungumzia kidogo uchaguzi mdogo wa Novemba unaokuja; ni kweli kwamba, taratibu zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri leo asubuhi, sisi hatukuwa tunazijua, tumezipata lakini hotuba yetu tumeiandaa kabla. Tulipokuwa tunaandaa hotuba hiyo, tulikuwa tunafikiria kwamba ni muhimu watu wote wapate semina za kutosha. Mgogoro tulioupata mwaka 2005 ni wasimamizi wasaidizi waliosimamia chaguzi hawakufuata taratibu. Mfano halisi ni Kijiji cha Mashine ya Maji kule Temeke Dar es Salaam.

Mheshimiwa Waziri, kama atahitaji nitamweleza kwa kirefu kilitokea nini; kwa sababu walipeleka mpaka *FFU* wananchi wakasema tulishapiga haturudii tena. Sasa haya ni mambo ambayo yanaweza kuleta vurugu na ni imani yangu kwamba, yatasahihishwa na yatafanyiwa kazi. Tulitegemea katika uchaguzi huu, daftari la wapiga kura litatumika, tumeambiwa kuna daftari lingine; tunajiuliza kwa nini tumekwenda kwenye daftari lingine wakati tungeweza kutumia lilelile ambalo tumeligharimia kwa hela nyingi zaidi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nalazimika kutoa ufafanuzi tena kwa sababu bado tutakuwa na Wasemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye kasma nyingine. Ndugu zangu wa

Kambi ya Upinzani, hapa tunasimamia haki tu, ipo lugha ya Kibunge na Kanuni zake. Unaweza kuwa na hisia kali sana juu ya mambo fulani, lakini namna yanavyowasilishwa ndani ya Bunge ni lazima kuzingatia Kanuni za Bunge. Mfano mmoja ni Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, huyu ni Mbunge sasa ni mwaka wa 14 hapa Bungeni na anazijua sana Kanuni na ni msomi mzuri kwa kweli. Utaona kwa makusudi tu, ameamua kuchukua ajenda fulani ili aweze kuipatia jukwaa na kutoa mawazo yake. Sasa hayo sio madhumuni ya Bunge na ndio maana tuna kitabu kizima kabisa hiki cha Kanuni. Lugha ya kuudhi hairuhusiwi, huwezi kumjadili Rais hata kama humpendi na kuna msururu wa watu wengi tu ambao huwezi kuwajadili.

Natoa tahadhari hii kwa sababu ya ule mtiririko wa hoja ya Kambi ya Upinzani, kuhusu hoja iliyopo ambayo ni Bajeti. Hiki ni kikao cha kupitisha makadirio na matumizi. Ningeomba mnaofuata mlenge hapo, mtazungumza kwa raha mtamaliza. Ukiwa na hoja mahususi kuhusu *TANAPA*, Kanuni zipo. Ukiwa na hoja mahususi kuhusu jambo lingine lolote, Kanuni zipo. Yale mambo ya Mashirika ya Umma, namsubiri Mwenyekiti wa *POAC*, ambaye naye anatoka kambi ya Upinzani, atakapoyaleta tutayajadili na ndio maana ile ya kuyawahisha. Unaanza kuyazungumza leo wakati yako kwenye Kamati! Nadhani tumeelewana Waheshimiwa.

Sasa wachangiaji wangu ni kwa mtiririko ufuatao: Ataanza Mheshimiwa Mudhihir, atafuatia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatia Mheshimiwa Felix Mrema, aliyekuwapo kwenye orodha, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ameomba azungumze kesho kwa sababu ana dharura. Kwa hiyo, yeye ninamwacha na atafuatia Mheshimiwa Estherina Kilasi. Namwita sasa Mheshimiwa Mudhihir.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, niruhusu nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Hoja ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mimi sina matatizo na hoja ya Bajeti tuliyoipitisha juzi, sina matatizo na Hotuba ya Waziri Mkuu, maana maeneo mawili yaliyokuwa yananisumbua ndiyo nitakayoyazungumzia. Hili la kwanza, bahati nzuri ibara ya 19 ya hoja ya Waziri Mkuu imezungumzia juu ya ulegelege wa baadhi ya viongozi, ambao wanakosa ubunifu, uaminifu, uadilifu na kutenda kazi kwa mazowea. Tatizo halipo tu kwa viongozi, tatizo lipo vilevile kwa baadhi ya Mawaziri ambao wanatanguliza ubinafsi mbele. Mwaka 2003, Wizara ya Madini kupitia *GST* walifanya *survey* ya *limestone resources*, jasi la kutengeneza saruji, katika mwambao wa Mkoa wa Lindi na ripoti ninayo hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa kimaabara, umeonesha kwamba, kutoka Mchinga kuelekea Kaskazini, Vijiji vya Maloo na Nnang’ole, kuna kiasi cha jasi tani milioni 16.2 na kutoka Mchinga kuja Kusini mpaka Likong’o kuna mabaki pale au kuna kiasi cha jasi tani milioni 24.3.

Kwa bahati njema, uchunguzi wa maabara umeonesha kuwa jasi hiyo ina wastani wa *calcium oxide* 50.56%, ambayo ni malighafi tosha ya kutengeneza saruji. Hali hii

kutokana na ukweli kwamba, jasi limeadimika duniani, imevutia wawekezaji wengi sana. Mwaka jana wakafika wawekezaji pale Mchinga, wakawalipa fidia Wananchi wa Mchinga. Wameacha kulima na wengine wameng'oa matofali yao. Halafu kwa sababu kuna Waziri tu akisikia jina la Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, nyongo humtumbukia, anapata kichefuchefu, haifai ndimu mbichi wala mbilimbi; amekuja akasema kiwanda hiki kihame Mchinga kiende Machole. Kinachoumiza zaidi ni kwamba, amesema kitu kibaya sana kumsingizia Rais katika mambo ya ovyo ovyo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dokta Ben Carson…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, mimi ninamheshimu sana Mheshimiwa Mudhihir na leo tunaanza kujadili hotuba nyingine nzito, baada ya ile ya Waziri Mkuu; ni ile Kanuni ya 64(1)(a).

Mheshimiwa Spika, alianza Mheshimiwa Selelii, akiwalaani Mawaziri wote na wengine wametumia lugha chafu tu. Wengine tungekuwa tayari kujiuzulu kama kweli tunajipendelea na kama kweli sisi ni wabadhirifu. Kwa hiyo, tunavyozidi kuendelea, Wabunge wawe majasiri wataje majina, hii *mass generalization* inatuumiza sana. Kwa hiyo, kwa kutumia Kanuni ya 4, mimi naomba wawataje kwa majina ili wale ambao kama dhamira yao inadai wajiuzulu kuliko *mass generalization* na kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a), hii sio lugha nzuri na kwa Kanuni zote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri pale awali ni mambo yamepita, sasa inaonekana yanaendelea. Kwa hiyo, ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge, pamoja na rafiki yangu Mudhihir, wawe majasiri, wamtaje jina Waziri ambaye anajipendelea, ambaye hana uadilifu, kuliko kutuunganisha wote kwa pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ahsante. Kwa mujibu wa taratibu za kuendesha Bunge, itakuwa ni vigumu mimi niagize kila anayetoa tuhuma amtaje na muhusika. Pengine ninachoweza kusema ni kwa maana tu ya ustaarabu katika kuendesha mambo, baadaye mtu wa namna hiyo ni vizuri aende kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndio ataje jina ili Serikali iweze kulifanyia kazi hilo jambo.

Nasema hivyo kwa sababu tukikaa hapa pia tukawa tunatumia uhuru wa kuongea Bungeni, kuwataja watu kwa majina, mimi sina imani kwamba tutalinda amani ndani ya Bunge hili. Kwa sababu kile kinachoonekana pengine upendeleo ni utekelezaji tu wa ilani.

Sasa kila mtu akisimama akasema ni fulani ananyoosha na kidole, tunaweza kufika pabaya. Mimi nadhani mtu akisema kuna Waziri mmoja hatendi haki, labda amalizie na nitatoa taarifa rasmi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hiyo itatosha kabisa.

Mheshimiwa Mudhihir, nadhani ukienda katika mstari huo, nisingependa utaje jina hapa hadharani kwa sababu watu wote wanatuangalia. Pengine si vizuri sana na pengine ukishataja jina ni vigumu sana kuja kuomba radhi, kwa sababu unaweza kuwa umekosea. Kwa hiyo ni vizuri ukanong'one Serikalini ili lichunguzwe na tuweze kujua baadaye kama ni kweli au sivyo.

Huu ni mwongozo kwa wote jamani, tushike hivyo. Mheshimiwa Mudhihir. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa mwongozo huo na kwa desturi, baridi huwa na mzizimo kwa kondoo mwenye manyoya haba. Inatisha sana unapoona kondoo amejaa manyoya, halafu bado na yeye anazizimwa na baridi kwa kiasi kile kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini muda wangu utakuwa umehifadhiwa. Dokta Ben Carson, katika kitabu chake, *"Think Big"*, amesema hivi: "Mtu yeyote mwenye akili za kawaida, anapotaka kufanya uamuzi anatakiwa kujiuliza maswali mawili na ninaomba kuyanukuu; *What do I gain if I do? What do I sacrifice if I don't?"* Kwa Kiswahili, tafsiri isiyokuwa rasmi ni kwamba: "Hivi mimi ninapata manufaa gani, ninapata tija gani nikichukua uamuzi huu? Ninakosa nini nisipochukua uamuzi huu? Mimi ninaomba kutoa ushauri wa bure tu, faida zinazotokana na kiwanda hiki kikibakizwa palepale Mchinga, tunaondosha gharama za uzalishaji zisizokuwa na sababu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa huyu anasema kiwanda kikiwekwa pale, basi miamba itakapokuwa inapasuliwa, majengo ya kiwanda yatapata nyufa. Sisi tunaona kuna kiwanda pale Wazo, kipo palepale yanapopatikana malighafi, ukienda kule Songwe Mbeya Cement, kiwanda kipo palepale, ukienda Pongwe kule Tanga, kiwanda kipo palepale. Unatoa kiwanda kutoka Mchinga Mlima wa Mamba, kwenye Kitongoji cha Gezaulole mpaka Lindi kilometa 35; hivyo barabara ile ambayo imejengwa kwa mapesa mengi ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi, malori ya ukubwa wa tani 40 wastani wa 100 kwa siku yanatoa kifusi pale kupeleka Machole; barabara hii baada ya miaka miwili itakuwa hali gani? Hivi na hili nalo linahitaji digrii ya chuo kikuu kulitambua? Hili nalo ni aina ya kulaani mtu?

Ipo sera yetu ya *urbanization;* kuwazuwia vijana wasikimbie vijijini kwenda mijini. Sisi tumejiunga na *UN Habitat,* sasa tunataka tuwaondoe vijana Mchinga, waje Lindi Machole, wale wa Dar es Salaam mnawaita Wamachinga, sasa sijui wakija Lindi mtawaita akina nani? Hivi na hili nalo huwezi kuliona? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sio hiyo tu; faida nyingine ya kubakiza kiwanda pale ni kwamba, ustawi wa Wana-Mchinga utapatikana, kwani huyu bwana ana ugomvi gani na watu wa Mchinga? Kuna mapato kwa Halmashauri, kuna mrabaha, kuna biashara

zitazuka pale, lakini anasema vilevile Mchinga hakuna umeme; umeme unaletwa na ukiletwa umeme vijijini, basi ndio unasaidia kupunguza gharama ile ya kuleta umeme kwa sababu kutakuwa na kiwanda. Vilevile tunaepusha mgogoro wa kisiasa usiokuwa na sababu. Yale mnayoyaona yanatokea kule Port Hacort, Nigeria, ni matokeo ya maamuzi ya ubinafsi ya namna hii. Hasara anayoweza kupata ni moja tu; kuvumilia kusikia jina langu linapotajwa Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, ndio hasara peke yake. Sasa hasara hii moja na faida zote zile, si ni bora aende kwenye uwingi kule? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mchungaji Eckhart Tolle, katika kitabu chake, *"The Power of Now"* ukurasa wa 13, naomba kumnukuu, anasema hivi: *"The mind is a superb instrument if used rightly. Used wrongly, however, it becomes very destructive to put it more accurately, it is not so much that you use your mind wrongly. You usually don't use it, it uses you. This is the decease you believe that you are your mind, this is the delusion, the instrument has taken you over."* Tafsiri isiyokuwa rasmi, akili huwa na manufaa ikitumiwa vyema, ikitumiwa vibaya huleta uharibifu; na sio kwamba unaitumia vibaya bali huitumii kabisa, akili inakutumia wewe; huu ni ugonjwa. Unaamini kuwa uko barabara na akili zako hali sio hiyo, akili imekuteka nyara.

Mheshimiwa Spika, viongozi ni lazima tujifunze kuzungumza na roho zetu, hata kama mwenzako humpendi, kwa sababu Waswahili wanasema wazimu hauna kwao. Huyo huyo Eckhart Tolle anasema kwenye ukurasa wa 14: *"You have probably come across, made people in the street incessantly talking or muttering to themselves. Well, that is not much different from what you and all other normal people do, except that you don't do it out loud."* Kwa tafsiri isiyo rasmi inasema: "Bila ya shaka umewahi kuwaona wendawazimu mitaani wakizungumza pweke; hali hiyo haina tofauti na wewe na watu wengine wa kawaida, isipokuwa wewe huzungumzi kwa sauti. Kwa hiyo, kama huwezi kuzungumza na akili yako vizuri kwa sababu tu ya inda na chuki, unaweza ukajikuta unafanya mambo ya ovyo kabisa kuliko ya yule ambaye anazungumza kwa sauti. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki hakiondoki Mchinga kikaenda kwenye Jimbo lake, kinakwenda kwenye Jimbo la Lindi Mjini, wala hana manufaa nacho, basi tu kutaka kunikera mimi. Anakuwa kama nyoka wa mdimu vile; anakaa kwenye mdimu wakati hali ndimu wala hajisingi kwa yale majani, lakini ukija wewe kuja kuchuma ndimu nyoka anakugonga kichwani. Hii ni tabia ngumu sana. Mimi hapa ningependa kuwanukuu wasanii wa Simba Wanyika waliposema: *"Wewe una wako nyumbani, mimi nina wangu nyumbani, chuki ya nini kati yangu mimi na wewe?"*

Sasa kauli ya Watu wa Mchinga walionituma wanasema hivi, hatuna nongwa na kiwanda kile kuhamishwa pale, maana si kila mtu na mali yake bwana, lakini kikishahamishwa, asisogee mtu kuja kuchukua jiwe pale au jasi kupeleka huko. Nasema hivi nikijua hatari iliyo mbele yangu, huyu bwana mkubwa tayari anatarajiwa au anajitarajia kuwa Rais wa 2015, hata wakati huo akiwa Rais, mimi ninasema haitawezekana kutoka jiwe pale. Kiwanda pale, ndio jiwe pale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ndio ufisadi. Twende darasani maana yake hivi karibuni kumetoka neno la ufisadi, linatumika sana na watu na ninaona kama wanalitumia vibaya.

Msomi mmoja amezungumza kwenye *Television* moja kwamba, neno hili ni jipya limeibuliwa na Dokta Slaa pale Mwembe Yanga. Ukweli ni kwamba, neno la ufisadi ni la siku nyingi sana katika Lugha ya Kiswahili. Ukienda kwenye Kamusi iliyotungwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Tanzania, Toleo la Mwaka 1981, ufisadi maana yake nanukuu: *"Ni mtu mbaya, mtongozaji, mharibifu, mpotevu, mwasherati, fitina, mgomvi."* Hii ndio tafsiri ya Ufisadi. Neno hili ufisadi tumelitohoa kutoka Lugha ya Kiarabu na Waarabu wamelitumia maeneo mengi, hata kwenye *Quran, Suratul-l-Baqara*, neno la ufisadi linatumika pale Mwenyezi Mungu anapowaambia watu, *"Wala msifanye ufisadi katika ardhi,"* aya ya 11. Neno hili sio tu kwenye *Quran*, linatumika vilevile hata kwenye misemo ya Kiarabu na yote hiyo tafsiri yake inafanana na *TUKI*. Pale Waarabu wanaposema, majogoo wakiwa wengi huufisidi usiku; maana huyu anawika saa sita, yule saa nane, hata alfajiri huijui imekujaje; hii ndio tafsiri ya ufisadi. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pengine kama ninao muda kidogo, maana yake nilikatizwa katizwa katikati hapa; nimeipitia hii hotuba ya ndugu yangu hapa, inauma sana pale anaposema kwa miaka 10 tu *CHADEMA* ilipotawala pale Karatu, mambo yamekuwa makubwa kuliko miaka 40 iliyopita. Mimi nafikiri tungekwenda kumwona Profesa Covey anasema nini; anasema: *"If we allow ourselves to dwell on negatives on hurts, on mistreatments, we will be negative thinkers."* Ukurasa wa 153. Hapa kila mmoja wetu akikaa kijijini kwake alipozaliwa au mtaani kwake alipokulia, toka alipopata akili mpaka leo, akisema hali ni ile ile hakuna mabadiliko, huyu mtu habadiliki tena hata angekuja shetani mbele yake; ni lazima tukubaliane kwamba, kuna mambo mengi yameshafanyika ya kutosha. Hivi ni kweli kwamba, ile barabara iliyojengwa kupitia Karatu kwenda Ngorongoro imejengwa na CHADEMA? Hata kidogo, haiingii akilini, lakini kusema hakuna kilichofanyika na kama alivyosema mwenzangu kwamba, kumbe yanayosemwa kwenye magazeti tunaweza tukaogelea nayo! *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, inauma sana unaposoma kwenye magazeti Mzee wetu Mkapa, analaumiwa laumiwa tu. Mzee huyu hakufanya kitu, vitu hivi vinaumiza sana. Kwa ufupi sana, mimi nilivyojaribu kuviorodhesha tu kwa haraka haraka jamani nchi hii Mkapa ameichukua ikiwa haikopesheki. Mfumko wa bei ulikuwa ni zaidi ya 40%, makusanyo ya ndani yalikuwa ni bilioni 25 akayapandisha mpaka bilioni 130. Nchi hii Mkapa aliweza kuifikisha mpaka kwenye *HIPC* tukafuzu mtihani wa *HIPC*. Mpango wa MMEM na MMES, leo tuna shule kila kata ni Mkapa huyu. *Mtwara Corridor,* mtandao wa barabara kuunganisha mikoa yetu, Uwanja wa Taifa. Hata hapa tulipo humu ndani ni matokeo yake yeye. Sasa ikiwa wewe kazi yako ni kuangalia machafu tu; yaani unashindwa hata na nyuki; nyuki anakusanya majani makavu yenye ukafu, majani mabichi, anakusanya utomvu, lakini *product* ya mwisho ni asali tamu ajabu. Wewe ukiwa kama inzi, hata ukitua kwenye chakula ujue maradhi tayari yameingia, wewe una matatizo. *(Makofi/ Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nishukuru kwa kupata nafasi ya kuwa mchangiaji wa pili. Naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi ninaomba kidogo niende kwenye mambo ambayo hayatawachekesha, kwa sababu kaka yangu amewachekesha.

Mheshimiwa Spika, jambo la uwongo likiongelewa mara 1000, linaweza likawa la ukweli. Mimi naomba nizungumzie Utawala Bora. Wewe mwenyewe ulinipeleka Marekani wiki sita, nikasoma Utawala Bora, nikiwa na Mama Anna Makinda na Mheshimiwa Mnyaa. Nilisoma Chuo Kikuu cha Washington kwa wiki sita, asubuhi na jioni juu ya Utawala Bora. Hakuna Wizara Muhimu kama Utawala Bora. Kila Wizara inahitaji Utawala Bora ndani yake na ili ujue Wizara hii ni muhimu, ndio maana Waziri wa Utawala Bora ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Hawa wenzetu hili jambo la ufisadi, maana yake naongelea ufisadi sasa, wanalichukua kama ni lao na ndio picha wanayoipeleka nchi nzima; sivyo. Naomba niseme ni kwa nini sivyo. Tuanze kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; wa kwanza amefungua milango kwamba, sasa kila kitu kiwe wazi na mambo yaangaliwe. Angeweza kufunga, hilo ni la kwanza. La pili, wanaposema jambo hili ni sisi tunaosema Wabunge wa CCM ni wanafiki, mna kidhibiti? Wakizungumza, nina kanda yao, si kweli. Wakati ilipokuja Kamati ya Mheshimiwa Dr. Harisson Mwakyembe hapa, wao wako 44; sisi tuko 274, tungesema hapana isingepita. Wabunge wa CCM hawakumbatii ufisadi wala Serikali ya CCM haikumbatii ufisadi. Yule mmoja mmoja ambaye ni fisadi, tunamnyofoa tena sisi wenyewe. Kwa hiyo, hili jambo nalisemea kwa mkazo kwa sababu wamelipenyeza kila mahali nchi nzima, si kweli. Nilitaka nianze hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa wanaweza wakawafanya Watanzania wakawaamini, nakusihi wakati unamalizia utoe ripoti ya jitihada zilizofanywa na Serikali kuhusu ufisadi na jitihada zinazofanywa na Wabunge wa CCM humu ndani. Maana sisi hatuwezi kwenda Mwembe Yanga, sisi ni watawala na ukisoma hiki kitabu kilichotolewa na *World Bank* kinasema: "*The Role of a Parliament In Curbing Corruption.*" *Corruption* inapiganiwa humu humu ndani, sio Mwembe Yanga; kwa hiyo, namsihi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe jitihada zinazofanywa na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi katika kupambana na ufisadi. Atoe hatua ambazo Rais, anazichukua katika hili suala la ufisadi na mwishoni sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe mikakati endelevu ya Serikali yake imejipanga kiasi gani, kupambana na hili suala la ufisadi, lakini aende kwa kasi sasa kwa sababu ninaona kama wenzetu wanataka kufanya mambo visivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaenda jambo la pili, hilo nimemaliza. Nchi yetu ina mihimili mitatu; kuna Mahakama, kuna Bunge lako hili na kuna Serikali Kuu, lakini katika Serikali Kuu, kuna kichwa cha Serikali Kuu. Kuna haja na umuhimu ninaouona

wa wakati Waziri Mkuu, anapofunga sasa tuwe kama nchi zilizoendelea. Nchi zilizoendelea Msemaji wa *White House,* anafahamika ni nani mpaka mtoto mdogo anamjua. Sasa basi ni vyema Waziri Mkuu, kwa sababu wananchi sasa wameingia kwenye kuchanganyikiwa, Waziri Mkuu pia aelekeze Msemaji wa Bunge ajulikane ni nani? Msemaji wa Serikali Kuu ni nani? Msemaji wa Mahakama ni nani? Lazima tujue Msemaji wa Ikulu ni nani? Hapa mahali panaleta mgongano, karibu kila mtu sasa anasema na Ikulu ni mahali pakubwa. Hatuwezi kuacha tu kila mtu akasema, ajulikane na nchi ijue kama ambavyo wenzetu Wamarekani wanajua, Msemaji wa *White House* ni nani na sisi ijulikane. Akisema Msemaji wa Ikulu, tunajua kasema Rais. Hilo nimelimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kubwa sasa. Mimi napenda kutumia Katiba ya Nchi, mmh! Eenhe! Katiba inaeleza wazi tena haikuficha; ili Kiti cha Mbunge au Jimbo liwe wazi ni vitu gani vinavyosababisha. Naomba mkasome kwenye Katiba ni vitu gani vinavyosababisha Jimbo liwe wazi. Mimi leo nimekuja tu kwa sababu imebidi nije niseme, nina mitihani. Mimi majuzi walikuja wananchi wangu wamepagawa wanatoka Jimboni, gazeti hili, eeh! Jamani kuna kazi!

*(Hapa Gazeti husika lilitolewa kwa ushahidi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, gazeti hili, naomba kunukuu kichwa cha habari: *"Majimbo ya Wabunge watano wa CCM yatangazwa yapo wazi."* Naomba kuli-*table.*

**SPIKA:** Linaitwaje hilo gazeti?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, hili gazeti linaitwa, *Nipe Habari Nguvu Ya Jamii.*

Mheshimiwa Spika, kichwa cha habari kinasema hivi: *"Majimbo ya Wabunge watano wa CCM yatangazwa yapo wazi ni ya wana mgambo wa ufisadi."* Naomba kuli-*table* hili gazeti na nitaomba lipelekwe kwa Waziri Mkuu. Ndugu zangu, haya magazeti uchwara yatatupeleka pabaya. Magazeti ya namna hii tukiendelea kuyaachia, yatatupeleka kwenye vurugu, nafikiri watu hawajui maana ya Ubunge wa Jimbo. Mimi Jimbo langu nimelihangaikia, leo unatangaza Jimbo langu Anne Kilango liko wazi! Iko hapa, wananchi wangu wamekuja na magazeti, halafu hawa watu walivyo *smart*, wameyaelekeza haya magazeti kwenye hayo Majimbo matano, yanauzwa huko huko. Wananchi wanayo, hawaelewi; Mheshimiwa Jimbo letu liko wazi? Nikawaambia nipeni.

Mheshimiwa Spika, katika hili sitaelewana na mtu, patakuwa padogo tena hapa. Katika hili sitakubali, hili ni kubwa. Majimbo matano ya *CCM* yako wazi, mimi ninavyojua Katiba na Sheria ya nchi, anayetangaza Majimbo kuwa wazi ni Tume ya Uchaguzi, ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Jaji Makame. Ukishatoa magazeti kama haya na unatoa wananchi wasome, wananchi wanasoma hayo Majimbo matano yaliyoko wazi, hakuna dhambi kubwa kama hii. Eti majimbo haya matano yako wazi kwa sababu

ni ya wanamgambo wa ufisadi. Kesho asubuhi, hili gazeti litasema Kiti cha Urais kiko wazi, wakiachiwa hao; kwa sababu kama sisi Majimbo yetu matano yako wazi, kwa kuwa sisi ni wanamgambo wa ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi naona Umoja wa Vijana wa Tanzania wote wanaandama, UWT wote wanaandama, wanamuunga mkono Rais, kwa sababu anapambana na ufisadi; ataponea wapi? Sisi ni wanamgambo, yeye sasa ni Amiri Jeshi wa hawa wanamgambo, kwa hiyo, na yeye pia kiti chake kitatangazwa wazi, hapana. Hili gazeti nitaomba Serikali, hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati unafunga, tujue limechukuliwa hatua gani nzito na ya uhakika, ambayo itafanya watu wasirudie utani huu. Huwezi kuamka tu ukafanya kama unavyotaka. Nchi hii ina Utawala Bora, sio nchi ya *free lance*, yaani kila mtu anaweza akasema anavyotaka. Jambo hili limenikera, jambo hili limeniudhi na nikupe picha; mimi nasoma vitabu sana, ukienda ukiangalia matatizo yaliyotokea Rwanda, yalianzishwa na magazeti uchwara. Ukienda Kenya, vurugu za Kenya magazeti uchwara yalichangia; haya magazeti uchwara haya, yatatufikisha mahali penye vurugu. Watanzania tutakuja kujutia nchi yetu ambayo ni nzuri kuliko nchi nyingi sana huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ambavyo hili jambo limenikera, ninaiomba Serikali katika hili ichukue hatua nzito na hawa watu wenye tabia ya kuandika mambo ya kihuni waache. Hii ni nchi yenye Utawala Bora. Kama wewe ni fisadi; kwa nini tusikuseme? Ninawaomba wananchi mnisikilize; hatutanyamaza kuwakosoa mafisadi hata siku moja, kwa sababu tunataka nchi yetu iwe sawa na nchi za wenzetu ambazo zina Utawala Bora. Sasa hapa mlikuwa mnaona tunatangazwa na wenzetu hawa wa upande huu kwamba, wao ndio wanaopambana na ufisadi, huku sisi wabunge wa CCM tayari, Majimbo yetu yanatangazwa kwa sababu tunapambana na ufisadi. Mnaona sasa *contradiction* hiyo? Katika hili ninaomba niwe wazi kabisa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati unapofunga tujue hili gazeti limechukuliwa hatua gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa Gazeti husika lilipelekwa kwa Mheshimiwa Spika)*

**SPIKA:** Wahudumu, pokeeni hilo kwanza nilione kabla sijampelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaendelea na ninamwita sasa Mheshimiwa Felix Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, wakati huo Mheshimiwa Abdulkarim Shah, naomba ajiandae.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri Mkuu. Nami pia najiunga na wenzangu katika kumpongeza na kumshukuru Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, kwa hotuba zao nzuri za bajeti. Nisipoteze wakati, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa hotuba yake ile ya Tarehe 10 Juni, juu ya msukosuko wa masoko ya kifedha ulimwenguni na jinsi ulivyoleta mporomoko wa uchumi sio ulimwenguni tu,

hata kufikia katika nchi yetu. Naishukuru Serikali, Rais, pamoja na Serikali yake, kwa kuandaa mpango huu wa kunusuru uchumi wa Tanzania na athari za msukosuko wa fedha, unaotokana na uchumi huu wa dunia jinsi ulivyoifikia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama kuna Jimbo au Mkoa ulioathirika sana na msukosuko huu wa kiuchumi ni Jimbo langu la Arusha na Mkoa wetu wa Arusha. Hii imeelezwa vizuri kabisa na Mheshimiwa Rais na napenda nirejee tu kuwa katika Jimbo letu la Arusha, Mkoa wa Arusha, Sekta ya Utalii, imeathirika sana. Sekta hii ndiyo inayoongoza kwa kuathirika ikifuatiwa na Sekta ya Madini kule Mererani. Mambo yamesimama vijana wetu wale wana Apolo hawana ajira, wamerejea Mjini Arusha tunabanana kule Mjini Arusha na hebu fikirieni hawa vijana wakirejea mjini bila ajira, tuna matatizo gani pale Arusha, hali ni ngumu kweli kweli. Sekta ya Mboga Mboga pia imeharibika; ajira zimeathirika na wawekezaji katika sekta hizi wameathirika. Nitaishia hapa, nisiishie kwa kusema, sisi tumefarijika sana kuona Serikali imetambua matatizo haya na imekuja na huu mpango wa kunusuru na angalau kutuletea mwarobaini ambao tunaamini utapunguza matatizo yanayotukabili na utatusaidia katika kurefusha maisha katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa shukrani hizo kutoka Arusha na kutoka kwangu mimi binafsi; ni mategemeo yetu kwamba, kazi hii ya utekelezaji wa mpango huu, itafanyika kwa ufanisi na haraka inayotakiwa ili ajira zisiendelee kuathirika zaidi na uchumi usiendelee kuporomoka zaidi. Nijaribu kutoa angalizo; wenzangu wamejaribu kugusia na mimi nitarudia; nilisema mwaka jana kwamba, lipo tatizo la maamuzi katika Serikali yetu. Nimesema kuna tatizo la *paralysis by analysis* na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulikiri kwamba, tatizo hili lipo na tukakushauri ulitafutie dawa. Napenda kukueleza kwamba, kweli umeanza kazi ya kulitafutia dawa tatizo hili, lakini kwa wakati huu tunapokwenda kwenye msukosuko huu, inahitajika nguvu ya ziada ya kuhakikisha kwamba, maamuzi yanafanyika kwa wakati na yale ambayo yanatakiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni mategemeo kwamba, utazingatia hilo na utasukuma Serikali yako katika kuhakikisha kwamba, haya maamuzi yanayotakiwa kufanyika ya utekelezaji wa huu mpango, yanatolewa kwa wakati na kwa kiwango tunachokitegemea ili kitunusuru sisi katika matatizo haya yanayotukabili. Nitoe mfano tu; katika kueleza baadhi ya matatizo tunayoyaona yaliyoko Serikalini, tumetazama jinsi mlivyokuwa mkisimamia Sekta ya Umeme. Mimi binafsi nilifadhaishwa kidogo na jinsi mlivyokuja Bungeni mara mbili, kufuata Kamati mbili tofauti, kutafuta *support* kutoka kwetu; sasa nikajiuliza kwa nini mnashindwa ninyi wenyewe kuamua yale yaliyokuwa yanawakabili? Kuyaamua maamuzi tu yaliyotakiwa kuhakikisha kwamba, megawatt 100 zimepatikana ziingizwe katika Grid yetu ya Taifa. Sasa woga huu ni wa nini? Mheshimiwa Waziri Mkuu, liangalie hilo litafutie dawa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme katika nchi yetu ni kubwa kuliko megawatt 100. Tanzania ni nchi ambayo wenye kupata huduma hii ya umeme ni asilimia 14 tu na hao 14 wanapata huduma hii ya umeme kwa matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, tatizo letu ni kuja na mikakati ya kuhakikisha kwamba, asilimia 86 ambayo haipati huduma hii ya umeme, inapata huduma ya umeme. Hili ndiyo tatizo linalotusumbua, hakikisheni

mnalihusisha Bunge letu hili katika kuja na mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya kutatua tatizo hili la kufikisha umeme kwa asilimia 86 ya nchi yetu, ambayo haipati umeme. Hii ndiyo changamoto yetu. *(Makofi)*

Sasa tunapoteza miaka zaidi ya mitano, bado mtazamo wetu ni wa megawatt 100 au megawatt 200, lazima tutoke huko; kinachonisumbua mimi ni kwamba, pamoja na mtaji mzuri tulionao Rais wetu anang'aa vizuri sana kimataifa.

Nchi yetu kidemokrasia inang'aa vizuri sana, tutumie nafasi hii vizuri kusukuma mradi ule wa Stigglers' Gorge, ambao ungetuwezesha sisi kuzalisha megawatt 2000 na tuondokane na tatizo la umeme katika taifa letu. Sio kuondokana na tatizo la umeme tu, lakini pia tungeweza kugeuza Rufiji Basin itumike katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Kwa hatua hiyo, moja kwa msukumo wa mradi huo mmoja tu, haya mapinduzi yetu tunayoyasema ya kilimo cha kijani, yataweza kufanikishwa kwa mradi kama wa Stigglers' Gorge. Sasa kwa nini hatuonekani kusukuma au tunasumbua na vitu kama hivyo vikubwa vya kitaifa ambayo vitatu-*engage* sisi sote katika kutafuta tunafanikishaje? Jambo la namna hii, linapoteza wakati; mwaka hadi mwaka *megawatt* 100, tutoke huko.

Arusha tunayo mengi yanayohitaji msukumo; Sekta ya Madini tulisema inahitaji msukumo, Mererani nimesema kumeathirika, pale Arusha tunaowaona wachimbaji wadogo wadogo na matunda yao wanatuletea katika Mji wetu wa Arusha. Hao wakubwa ni wa kwenu huko, hao wadogo ndiyo tunaona uwekezaji wao Arusha unatufaidisha namna gani. Sasa ni mategemeo yetu, katika ule mpango wa kunusuru uchumi, mtaweka mkazo, mtawapa kipaumbele hawa wachimbaji wadogo wadogo wa madini pale Mererani, hasa ile taasisi yao ya TAMIDA, ambayo inahitaji isaidiwe na ipewe msukumo.

Mheshimiwa Spika, wanaohitaji msamaha wa kodi ni hawa wadogo sio wakubwa; wadogo ndiyo wapewe auheni. Naona waamuzi mnakuwa wepesi mno kuwaonea huruma wakubwa, lakini hawa wadogo mnakuwa wazito mno kuonekana mnawasaidia! Sasa tubadilishe mwelekeo wetu, tuonekane tunatia nguvu pale panapostahili kupokea.

Mheshimiwa Spika, kilimo kiwe cha kisasa. Tunasema sasa hivi ni Kilimo Kwanza na mpango kazi umekwishaandaliwa. Mimi nashukuru kwamba, haya yote yanafanyika, yasiendelee kuwa maneno kama jinsi ambavyo tumezoea kuyasema. Sasa hivi tuwe tofauti, kweli iwe ni Kilimo Kwanza na tuonekane tunakwenda kwenye kilimo cha kisasa. Kinachonisumbua mimi ni kwamba, tunajichanganya kidogo, tunasema tuna mapinduzi ya kilimo lakini katika kuzalisha na kujitosheleza kwa chakula, huwezi ukajitosheleza kwenye chakula kama bado wewe mtazamo wako ni kilimo cha kujikimu; lazima tutoke kwenye kilimo cha kujikimu, twende kwenye kilimo cha kibiashara na katika kilimo cha kibiashara tutaweza kujikimu na tutaendeleza uchumi wetu kwa kuingia katika kilimo cha kibiashara na kufanya biashara ya kilimo sio vinginevyo. Tukibaki tu kwenye mtazamo wa kujitosheleza kwenye chakula, tutakuwa tunabakia tu

tumeganda kwenye kilimo cha kujikimu kitaifa na hivyo tutakuwa tumepoteza mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia jinsi ya kupeleka matrekta 55 mwaka huu na ununuzi wa matrekta 55. Mwaka jana amenunua 60 na matrekta madogo walinunua 29 na mwaka huu 1628. Sasa najiuliza; je, kweli haya matrekta yanatosheleza kuleta mapinduzi ya kilimo ya kijani katika Sekta ya Kilimo? Hata kidogo, tukiwa bado tunategemea, bajeti yetu kwa ajili ya ununuzi wa zana za kisasa hatutafika. Lazima taasisi za fedha zitumike vizuri ili ziweze kufanya kazi yao ya kuleta mapinduzi katika Sekta hii ya Kilimo. Tufanyaje, mmesema kuwa taasisi ya fedha haikuathirika; ni kweli haikuathirika kwa sababu haifanyi shughuli za kibenki katika nchi yetu. Wao wamekaa Dar es Salaam, wanashughulika na *Treasury Bills* na *Treasury Bonds* na wanatengeneza fedha kilaini; wataathirika namna gani katika mtikisiko huu wa kiuchumi?

Wanatakiwa wafanye shughuli za kibenki kama nchi nyingine hizo kubwa zilivyokuwa zinafanya shughuli za kibenki. Marekani pamoja na ulafi wao wote ule, sekta ya kifedha imeathirika kwa sababu waliwekeza kwenye sekta ya ujenzi wa nyumba *(mortgage finance);* waliwekeza katika *finance leasing*, wakawekeza katika *credit finance* na kwa ajili ya *consumer credit*. Ndiyo shughuli za kifedha za kibenki, sasa benki zetu hazishughuliki na shughuli hizo, zinakaa Dar es Salaam zinatengeneza pesa kilaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto yetu hasa ni benki zetu hizi tunazifanyaje ili ziweze kushughulika na *mortgage finance*, ziweze kushughulika na *financial leasing* ili matrekta yapatikane kwa mkopo kutoka kwenye taasisi za fedha, sio kwenye bajeti. Hatuna pesa kwenye bajeti ya kuweza ku- *satisfy demand* iliyo katika nchi ya trekta au zana za kilimo, ndiyo changamoto iliyoko. Waziri wa Fedha anayo mamlaka, Gavana anayo mamlaka, tumewawezesha wazitumie sheria hizo kuzisukuma taasisi za fedha zifanye wajibu wao. Nchi nyingine zinafanya hivyo na sisi tusiwe wa mwisho kufanya hivyo, *it can be done*, wasukumwe.

Mheshimiwa Spika, pale Arusha tuna tatizo lingine; *General Tyre*, tunangojea maamuzi miaka mitano sasa inakwisha bado maamuzi hayajapatikana. Tunashukuru mshahara tumeletewa, lakini hautoshi, watu wanangojea kiwanda kifufuliwe, tafadhali sana simamia *General Tyre* ifufuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tuna ICTR, inafikia ukomo wa kazi yake, watu 800 wataondoka, wale wageni, 500 wananchi pale wanawategemea na huo uchumi wote wa Arusha unaotegemea ICTR utaathirika. Tuichangamkie hiyo, Rais wa ICTR kaniambia tukiichangamkia hiyo, kuna kazi ambayo bado haijakamilika ya ICTR. Tuzungumze na Umoja wa Mataifa, tuhakikishe kazi hiyo inamalizika pale Arusha na isipelekwe mahali pengine popote, lakini hiyo lazima sisi tuonekane tumechangamka. Naomba Waziri Mkuu, uishabikie hiyo, hakikisha kwamba ile kazi iliyobaki ya ICTR haihamishwi kupelekwa nje, imalizwe pale pale Arusha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmojawapo wa wachangiaji wa Hotuba ya Waziri Mkuu leo. Naomba nianze kwa kusema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo sitakuwa na kilio zaidi ya kusema mambo ambayo ni mazuri, kwa dalili ambazo naziona nimefanyiwa katika Wilaya yangu ya Mbarali. Kwa hiyo, naomba niipongeze Serikali. Nafarijika kwamba, viongozi wakubwa wawili; Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu, wametembelea Wilaya yangu hadi vijijini. Kwa hiyo ni hatua moja ambayo na mimi nimenufaika sana, kwa kutembelewa na viongozi hawa. Kwa hiyo, nahitaji kuwashukuru na kuwapongeza kwa kuamua kuja Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na vilio viwili vikubwa sana vya barabara ambayo iliingizwa kwenye Ilani ya Uchaguzi, kwa miaka kumi sasa, lakini Mheshimiwa Kawambwa ameniosha sana jana, baada ya kupata ujumbe sasa inaanza kutengenezwa na ninapoongea nime-*confirm*, tayari watu wameanza kazi. Nashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

La pili ni moja ya mambo mazito, ambayo Mheshimiwa Rais, wakati anaanza uongozi wake aliyasema. Nafikiri mawili, matatu, yameangukia Wilaya ya Mbarali, nikiondoa la mifugo na la upanuzi wa hifadhi. Kilio chetu kilikuwa maeneo yale ambayo tulikuwa tunayategemea kwa kilimo, yalikuwa yamechukuliwa na hifadhi kwa asilimia kubwa na hasa kabla ya kupitisha sheria ambayo ilitofautiana sana na maamuzi yetu na wilaya, mkoa na uongozi mzima. Naishukuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa kuungana na mimi na Waziri mwenye dhamana hiyo, kuhakikisha kwamba, tunafikia muafaka. Nawashukuru sana na nawapongeza sana. *(Makofi)*

Kilichobaki ni awamu ambayo nafikiri kama Waziri peke yake wa Maliasili na Utalii hataweza kuimudu ni fidia ambayo ni kilio kikubwa sana kwa Wana-Mbarali. Wale wote waliohamishwa vijiji saba, maana yake ni kupoteza Kata moja. Ninaamini hela nyingi sana zimetumika, karibu bilioni sita na kitu katika kutoa fidia. Unapokuja kwa mtu mmoja mmoja, hali si nzuri ni mbaya sana, si rahisi ukampa mtu elfu hamsini, laki moja, laki mbili, ukategemea aende akaanze maisha na hakuhama kwa kupenda, amehamishwa kwa lazima. Kwa hiyo, namwomba Waziri Mkuu, hili ambalo Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii tumezungumza naye, ninaamini wakishirikiana na Hazina na wewe ukaweka mkono wako, basi uhakikishe kwamba, hiki kilio cha Wana-Mbarali waliohama kwa hiari, linatekelezwa na tuondoe kabisa kilio hicho, wafurahie kutunza ile Hifadhi ya Ihefu, ambayo inakwenda vizuri sana. Kwa hiyo, nakuomba hilo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nilitaka nizungumze kuhusu ugawaji wa maeneo. Nimekuwa nikisiliza maswali hapa ya Wabunge na mimi mwenyewe; kuhusu ugawaji wa Tarafa, Kata na Majimbo. Tumekuwa tukiambiwa tusubiri 2010 wakati wa uchaguzi, kwa imani kwamba, wale wote ambao tumeshapitisha kwenye RCC, kwa maana

Halmashauri imepitisha, tumepeleka RCC tumekubaliana, tukaleta maombi yetu TAMISEMI na kwenye ofisi husika. Tulifikiri ni wakati muafaka wa kujibiwa sasa hata kwa maandishi ili tujue kwamba sasa ombi limepokelewa na tunafikiri linafanyiwa kazi, mtu huelewa ni kitu gani kinaendelea mpaka hiyo 2010. Ninavyofahamu, Tarafa hazingoji 2010, sisi Mbarali tumeleta, Wilaya kubwa ambayo ina ukubwa wa *square kilometres* 16, tuna Tarafa mbili. Tumeleta maombi yetu muda mrefu, sasa ni mwaka wa pili, lakini hatujui muafaka wake ni nini na sijui tunasubiri nini?

Mheshimiwa Waziri, ningeomba sana hilo uweke mkono, uone na sisi tunapata Tarafa kabla hata ya mwaka huo wa 2010. Najua Waziri mwenye dhamana yupo, lakini na wewe ni kama Msimamizi Mkuu, kwa kweli nitaomba hilo ulisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina tatizo kubwa sana, sijajua msemaji wa mwisho katika Wizara ni nani, hasa Waziri anapotoa maagizo kwenye Wizara, nina matatizo kwenye Wizara tatu, ambazo mwenyewe angalau nafanya nazo kazi na nimekuwa nikifuatilia kwa karibu. Nafikiri kuna matatizo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Hizi Wizara tunapata Mawaziri wazuri sana na wamekuwa wakibadilishwa, lakini nafikiri kuna watu wamekaa muda mrefu sana huko kwenye kilimo; kama ni wakurugenzi ni wa muda mrefu hawataki kubadilika kwenda na wakati.

Kwa hiyo, ukienda unaongea na mtu wa ofisini anasema ndiyo, Waziri anatoa agizo lake humu ndani ya Bunge, lakini utekelezaji wake unaenda taratibu. Sasa tunashindwa kuelewa ni nani tumsikilize; Mtaalamu, Mtendaji wa Wizara au tunamsikiliza Waziri.

Ningeomba Waziri Mkuu, hili liangaliwe maana utaendelea kubadilisha Mawaziri katika Wizara hii; tunajua wamepita Mawaziri wengi sana, wenye uwezo wa kufanya kazi, lakini kuna kitu kinawavuta. Ukienda Elimu, nafikiri Mawaziri wamekuwa wakituambia hapa walimu hawana madai, walimu hawana matatizo, lakini unapokuja kwenye hali halisi, unashangaa kukuta walimu bado wanalalamika hawajalipwa mafao yao, hawajalipwa pesa zao za uhamisho. Wao kama wazee, nafikiri wanapewa taarifa; sasa kuna nini? Tungepita kila idara tuone kiini chake, mimi sisemi kwamba, watu wabadilishwe lakini kuna wakati tuone kila mtu anawajibika katika hizo Wizara.

Kwenye maji na umwagiliaji, natoa mfano tu Mheshimiwa Rais, alipotembelea Mbarali aligiza kwamba, scheme zote za umwagiliaji; kuna scheme mbili; Madibira na Igurusi. Nataka nipate taarifa na nione *design* yake au *feasibility study* imefanyika na nipewe taarifa na akaniagiza Mbunge usipoona jambo limetimia, nione wewe mwenyewe. Ukikutana na wale wataalamu ni hivi, lakini na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji alitembelea kule, akaona hali halisi na ametembelea Mashamba ya Mbarali, lakini mtu tu kwa mapenzi yake, anazidi kuhamisha vifaa anapeleka sehemu nyingine. Anahamisha pale ambapo vipo, kwa mfano, Shamba la Madibira, kuna lile la umwagiliaji lenye ekta 3000; kahamisha matrekta, magari na vifaa mbalimbali anasema, napeleka sehemu nyingine, havijarudi mpaka sasa. Sasa tunapata wasiwasi; siku moja nimekwenda Wizara ya Elimu, nikamwomba Mkurugenzi wa Elimu naomba nije nikuone. Akaondoka halafu akasema nilienda kuzika, lakini fikiria; Mbunge umesafiri

*all the way* unafika pale unaambiwa mtu amekwenda kuzika na alijua anakwenda kuzika kwa nini asikupigie hata simu? Kwa hiyo, nafikiri kuna matatizo katika Wizara hizi ambazo ni muhimu sana kwetu.

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka nizungumzie kilimo kwa ujumla, kama alivyoliweka Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimpongeze; kila mahali alipotembelea amesisitiza sana kuzungumzia suala la kilimo. Wilaya yangu ni sehemu ya kilimo na alipofika kule, alikuta sehemu kubwa inahitaji kilimo cha umwagiliaji. Sasa niseme tu ili kilimo kiboreshwe, ninaamini pembejeo ni muhimu, mbolea kwa maana ya mbolea, matrekta, lakini mwisho wake soko la mazao haya ambayo tunalima ili kumfanya Mkulima aendelee kulima na apate kipato na miundombinu vilevile inayosaidia kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikianzia kwenye upande wa pembejeo, amezungumzia hapa matrekta, lakini mkombozi mkubwa wa mkulima wa kawaida ni *power tillers* na yeye emeona. Cha kusikitisha, sasa hatuelewi, wananchi wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba, wanatafuta pesa za kununua *power tillers,* chombo pekee kwa wale wenye ushirika ni sehemu ya SCCULT.

Sasa kwangu wametoa *deposit* ya hela nyingi sana pale SCCULT, wamekuwa wakisubiri trekta hizo hazijapatikana mpaka leo, Waziri Mkuu na wewe ni shahidi. Sasa sijajua tatizo ni pesa au ni trekta zinakotoka; kwa ushauri wangu zile pesa za JK au za mikopo; kwa nini zisingipelekwa huko SCCULT ili waagize hizo *power tillers* ziweze kusaidia. Ninaamini umefanya majaribio kwenye wilaya yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, uliona zile *power tillers.* Uliitisha Wakuu wa Mikoa wote na umeona jinsi ambavyo zinaweza kusaidia wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba hili ni jambo muhimu sana, tuwape hawa SCCULT pesa za kutosha waagize *power tillers* na hawa ambao wameshatoa angalau *deposit,* waweze kupewa *power tillers* waweze kuondokana na umaskini.

La tatu ni upande wa masoko; mimi nafikiri na wenzangu ambao wanatumia mpenyo wa stakabadhi za mazao ghalani na wewe umeona ni soko kubwa na zuri sana kwa mkulima wa kawaida. Anapovuna na kuwekwa kwenye ghala akisubiri bei ipande, wakati huo anapata pesa za kukopa kwa ajili ya kumwezesha. Sasa tatizo liko kwenye maghala. Tulipokuwa tunapitisha sheria hii, tulisema kutakuwa na uwezeshaji wa maghala, yatatengenezwa ya kisasa, lakini sasa ukipita kwenye maghala mengi si ya kisasa na uendeshaji wake sio ule ambao tuliudhamiria wakati tunapitisha sheria.

La nne, kama nilivyomsikiliza vizuri Mheshimiwa Rais, alipokuwa anazungumza kwamba wale wafanyabiashara ambao walinunua mazao kwa wakulima na bei haikupanda watapewa fidia. Sasa nilikuwa najiuliza swali moja; kwa mfano, wakulima wameweka mazao ghalani wanasubiri bei ipande wauze, lakini kwa sasa bei haikupanda; je; na wao watakuwepo katika kupewa fidia? Kwa sababu umeweka bei haikupanda, mtikisiko wa uchumi umetokea, kwa hiyo, ina maana hawatapata fidia. Sasa nalo hili liangaliwe ili mkulima aweze kupata faida kwa hilo.

Mwaka jana kumeanzishwa mpango wa *voucher system*, ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliuzindua Kilombero na Wilaya yangu ikawa ni mojawapo. Sasa kwa hali niliyojifunza, walionufaika katika mpango huu sio wakulima wa kawaida; kumekuwa na ubadhirifu mkubwa sana katika utoaji wa *voucher* hizi, sisi tumefanya majaribio.

Sijajua kuna kitu gani pale ndani; aidha, unawanufaisha viongozi wa vijiji, wenyeviti na Wakala, kwa sababu Wakala asipokuwa mwaminifu, akakaa na Afisa Mtendaji wa Kijiji, wakasaini kile kitabu wakaenda kuchukua pesa. Kwa hiyo, yule mkulima ambaye tulimdhamiria apate mbolea hawezi kupata, labda sasa Wizara ya Kilimo ikae tena iangalie kuna tatizo gani. Baada ya sisi kuona kwamba, wakulima hawakunufaika ni watu wachache wamenufaika, tuliweza kuunda Kamati ya Madiwani, imepita kuchunguza kila kijiji ambapo vitabu vilipelekwa. Tunategemea matokeo yakija, tutakuwa na ushauri mzuri sana kwa Serikali ili usaidie kwa wilaya nyingine ambazo mtatumia mpango huu wa *voucher system*, lakini umekuwa ni mpango mzuri sana.

Mbolea hii ya Minjingu, inaonekana bado haijaeleweka kwa wananchi, imebaki kwenye maghala na inaonekana mazao mengi hayaleti tija kwenye mazao mengi. Sasa nafikiri kuna tatizo fulani, tunahitaji elimu sana kwa ajili ya mbolea ya Minjingu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwenye kilimo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, umetembelea mashamba mengi na tulikuwa tuna mashamba makubwa sana, mengine yamebinafsishwa na mengine hayajabinafishwa. Ukienda kwa mfano kule Mbozi, kuna mashamba makubwa ya mahindi, ambayo hayafanyiwi kazi na wananchi wanahitaji kuyatumia yale mashamba. Sasa tunafikiri wenzetu wataalamu, whether ni kilimo au kadiri utakavyoona inafaa, basi wapite wafanye tathmini ya mashamba yote haya, kama tumeamua kuweka kipaumbele kwenye kilimo. Hata kwa wale ambao wamebinafsishwa, ni muafaka kupita kuangalia kama kile ambacho tulidhamiria wazalishe wanakizalisha. Je, wameongeza uzalishaji zaidi ya ule ambao ulikuwa unafanywa huko nyuma? Ninafikiri tutakuwa tumeondokana na tatizo la njaa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwisho, suala la wastaafu ambao walikuwa chini ya Mpango wa PPF, wamekuwa na kilio chao cha muda mrefu sana. Suala hili lilinishinda kujibu, wanasema tusubiri miaka 55 au 60 ya kustaafu na tulishapunguzwa kazi na tumeshakuwa na umoja wetu. Kutokana na hali ya maisha, sasa hivi nimejikuta afya hainiruhusu hata kufika hiyo miaka 55 au 60, ninaweza nikafa, nina magonjwa ya kisasa, labda anaumwa UKIMWI; hivi nikae tu kusubiri miaka 60; hakuna utaratibu mwingine unaoweza kufanyika ili mimi nilipwe mafao yangu mapema? Ni jambo ambalo unaweza kuona ni la kawaida sana, lakini mtu anapokwambia linakugusa.

Mtu anasema amepunguzwa kazi, hawezi kusubiri miaka 60, anajua kabisa miaka yake ya kuishi ni miwili, mitatu. Tunafikiri sasa ni wakati mzuri wa hii sheria basi iangaliwe upya. Unapokuta watu laki tatu wameunda umoja wao, wanazungumzia suala hili, tuseme ni kitu muhimu sana kwa wananchi hawa kuwasaidia.

Upande wa elimu kama nilivyozungumzia, matatizo bado tunayo. Naamini Waziri mwenye dhamana ya elimu yupo, tumedhamiria kabisa kuboresha elimu, lakini majengo bado yamebaki hayajamalizika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Waziri Mkuu, ambayo iko mbele yetu. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote walioko pamoja naye, wanaomsaidia kazi na Watendaji Wakuu, kwa yote yale waliyotueleza katika kitabu hiki.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kuendeleza shukrani zangu kwa Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia. Naomba niwapongeze Wakurugenzi Watendaji, pamoja na Wataalamu wake wote, bila kuwasahau Waheshimiwa Madiwani, ambao ndiyo wanasimamia vizuri shughuli zote zinazofanywa katika Halmashauri ya Mafia. Yapo matatizo madogo madogo, binafsi nimeyashuhudia, lakini ni mambo ya kurekebisha na ninaamini tutafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nililokuwa nataka kusema la kwanza, nizungumzie upande wa kuboresha wilaya zetu. Nazungumzia hili kwa kuwa Wizara hii ni mtambuka. Wizara mtambuka inaingia idara zote, inapeleka wataalamu wake au kupitia jina la Wizara zile wale wataalamu wanamsadia.

Mheshimiwa Spika, Mafia ni Wilaya ambayo sasa hivi inakuja juu sana kimaendeleo na hii yote ni jitihada za Serikali. Sisi tunasema, lakini baada ya kusema jitihada za Serikali kwa maana *channel* yake na siwezi kuacha kutoa shukrani; nilipoanzia mimi mwaka 2000, baadhi ya yale tuliyoyasema na Serikali ya Awamu ya Tatu, walipoanza ku-*take over* yale tuliyoyaongea na baadaye Serikali ya Awamu ya Nne wakaweza kuyaendeleza na kuyaboresha zaidi.

Naomba niwashukuru wale wote waliokuwa katika Serikali ya Awamu ya Tatu; Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, nakushukuru sana kwa kuanza ujenzi wa Gati la Mafia, pamoja na aliyekuwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba; mzee wangu nakushukuru sana. Hatuwezi kuacha thamani ya yale ambayo mmetufanyia, kwa sababu bila ya ninyi ingekuwa kipindi hiki ndiyo tunaanza. Mlianza ninyi na sasa Serikali ya Awamu ya Nne inafanya kazi yake vizuri na hali ya Mafia sasa hivi tunakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, sasa hivi naamini kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Estherina Kilasi kwamba, yuko katika kutoa shukrani kwa yale yaliyofanywa; na mimi naomba niseme kwa niaba ya Wananchi wa Mafia kwamba, tunaomba tuishukuru Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwani Gati la Mafia linajengwa na kwa taarifa niliyoipata katikati ya mwezi wa saba, Mkandarasi atakuwa amefika *site*.

Tunakushukuru kwa sababu hicho ndiyo kilikuwa kilio kikubwa sana cha Wananchi wa Wilaya ya Mafia. Tunaamini kwa kuwa limesemwa litafanyika. Serikali hii ni mahiri na yenye uadilifu, kama yapo au wapo watu wachache ambao ndiyo wanaichafua Serikali hii, mimi nasema tunakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, Mafia katika kuendeleza kama tulivyosema unajengwa uwanja wa ndege, barabara zitatengenezwa, Gati litajengwa, lakini na gesi sasa hivi inachimbwa. Ninaamini wakati wowote ule, tutapata matunda mazuri, gesi inachimbwa na itapatikana na visima zaidi ya viwili au vitatu vitachimbwa pale Mafia.

Sasa kwa kufanya hivyo na wakati wa utanuzi au maboresho ya mji wetu, nilikuwa naiomba sana TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, muiangalie Mafia. Unapomhamisha mtu na kusema tunataka kutengeneza barabara tutakulipa fidia, utamlipa mtu atakwenda kununua shamba, akinunua shamba atakwenda atafanya maarifa apate riziki ya lile eneo na akishapata atakuwa amelihodhi kisheria. Baadaye atajenga upya nyumba yake itaangalia Magharibi, mwingine atajenga eneo lile lile jirani yake itaangalia Mashariki. Kwa hiyo, tutaitengeneza Mafia, tutaitengeneza *squarter* ya kudumu duniani.

Ninachoiomba Serikali, iiweke Mafia kama eneo ambalo tunataka liwe mfano na linaweza likawa mfano bora katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki. Mafia naomba niseme, tunaweza tukaitengeneza ikawa Mini-Singapore; ni eneo zuri ambalo linaweza likaboresha yale yote yaliyokuwa yakifanyika nje hata biashara. Inawezekana baadaye tukafanya *free port* kama Serikali ikiona inafaa ili wafanyabiashara wenye magari yao na wenye biashara zao, wawe wanaleta Mafia. Badala ya mtu kupanda ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Dubai au Japan, atakuja Mafia kwa Dola mia moja ili aweze kununua gari lake na kuweza kulileta Bara. Tutapata mapato na ajira zitapatikana. Vilevile tutaitengeneza nchi yetu na hali ya nchi itazidi kuboreka kwa kupitia Mfuko wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nililokuwa nataka kulizungumzia, ambalo ni kero ni kwamba, Mafia ni Kisiwa; juzi nilizungumza suala la usalama wa baharini. Sasa hivi kuna ujangiri au ujambazi, ambao unafanyika katika Pwani yetu ya kutokea Muyuni kuja Mafia mpaka maeneo ya Kilwa na Pwani hii ya Rufiji.

Sasa hivi watu wanakuja na boti, wanakwenda wanawavamia wasafiri wetu wanaosafirisha mazao yao au bidhaa zao na kuwateka. Sasa juzi wakati nauliza swali la msingi, Mheshimiwa Hasnain Dewji aliuliza swali lakini bahati mbaya hakuliuliza mahali husika; alisema tunaomba Wizara husika ya Ulinzi au Mambo ya Ndani, iweke Kituo Maalum cha Rescue cha kuweza kuwasaidia wale wanaopata athari baharini. Pale Mafia ni karibu na Kilwa, pia ni karibu na Mkuranga. Kwa hiyo, tunaweza kuwasaidia kwani watu wengi wanakufa. Hivi juzi tu amefariki binamu yangu mmoja baharini na amepatikana siku ya pili, lakini amepatikana akiwa ameshafariki, kwa sababu ya kukosa huduma ya uokoaji. Kwa hiyo, kungekuwa na kituo na taarifa zingefika mapema, kama kungekuwa na vyombo pale Mafia basi tungeweza kuokoa maisha ya yule kijana, kama ingekuwa ahadi yake basi ingekuwa tena halina nguvu.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala lingine linalohusu magazeti. Suala la magazeti kama lilivyozungumzwa na Mheshimiwa Anne Malecela, yanatuumiza. Yamemuumiza Mheshimiwa Anne Malecela akiwa mmojawapo kati ya Majimbo matano yaliyo wazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ya Kilimo, Maendeleo ya Mifugo, Uvuvi na Maji, ilidhalilishwa na yote yalitokana na uandishi mbovu wa waandishi wa magazeti haya mpaka tulifikia Mheshimiwa Waziri na ninaweza kusema tu Mheshimiwa John Magufuli; alinukuliwa akisema kwamba, hatishwi na Kamati ya Kilimo inayoongozwa na Mheshimiwa Gideon Cheyo, kisa wanasema eti tutapinga kuipitisha Bajeti ya Wizara ya Mifugo. Tumeongea wapi maneno hayo?

Tulipokuja kukaa na Mheshimiwa Waziri, alikataa alisema hakusema. Sasa tunalipeleka wapi? Baada ya siku mbili au tatu, likaandika tena kwamba, Mheshimiwa Rais, baada ya kusoma yale magazeti inaelekea pengine na wenyewe wakawa wamemnukuu vibaya akasema, Magufuli nakukabidhi rungu, choma nyavu usitishwe na wanasiasa uchwara, kwa maana ya Kamati nzima ni wanasiasa uchwara sasa. Haya yote yametokana na uandishi mbovu wa magazeti.

Mheshimiwa Spika, hili ukilinyamazia na ukisema tuwaonee huruma, tunaadhirika sisi na Bunge lako tutakuwa vichekesho tu mbele ya jamii. Naomba kwa hili, uwe mkali na uweze kulichukulia hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magazeti haya sasa hivi yanatukera; sisi Watanzania tuko wa rangi mbalimbali, lakini akitokea mtu anafanya jambo fulani utasikia Mtanzania mwenye asili ya Kiasia, Mwarabu, Mmanga Mmoja au Mdosi; haya yanatokea wapi? Mnataka tufanye kazi gani ili tuonekane kwamba sisi ni Watanzania safi? Haya yote ni uchochezi wa magazeti na baadhi ya Viongozi wengine wanafikia kusema kwamba, hao Wahindi hawafai, kama mmoja semeni mwekezaji kisha fukuza, lakini usitaje Mhindi.

Juzi nimeshuhudia mwenyewe pale Ilala; Mhindi mmoja aligongwa na jamaa wa pikipiki pale sokoni Ilala. Sasa wakati yule mtu anatoka kuangalia vipi alivyoumia, basi lilitoka kundi la watu pale sokoni wakasema Mhindi huyo, Mhindi huyo! Sasa wakamkamata yule Mhindi kwa kumzuia ili yule mwenye pikipiki akimbie na alikimbia mpaka mimi nilipofika nikawaambia ninyi mnataka kumdhuru. Nikatoa kitambulisho changu, *Redbull,* nilipotoa tu a wale watu wakasema mtu wa usalama, hawakuelewa ikabidi wakimbie, ndiyo nikamchukua yule jamaa nikamwambia ingia kwenye gari yako hapa watakubamiza ondoka akaondoka zake. Hata alipokuja *traffic* alisema bwana basi sitaki chochote, kwa kuwa sikuumia basi na hivi ni vya kupita.

Kwa hiyo, naomba sana tunapoahidi kwamba, tunamuenzi Baba wa Taifa; hivi tunamuenzi kwa njia gani? Haya magazeti yanatutakia nini? Mimi leo rangi yangu ndiyo hii; nifanyeje? Hivi mchango wangu hauthaminiki katika nchi hii mpaka watamke? Kwa hiyo, naomba unyanyapaa huu ukemewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiona gazeti, kiongozi au mtu yeyote anazungumzia tabaka la aina fulani, huyo alaaniwe na wala msitie shaka.

Iliposemwa kwamba, Baraza la Mawaziri lilaaniwe, mimi nasema aliongea kwa uchungu, lakini pia na ninyi mko mbele ya Mwenyezi Mungu, anawalinda tu. Nawaombea dua, laana za maneno mbaya kwa bahati mbaya yakija basi zisikufikieni na muweze kufanya kazi vizuri. *Inshallah* kwa nguvu za *Allah*, mtafanya kazi vizuri, tuweze kufanikisha maendeleo ya nchi yetu na tuko imara kuhakikisha kwamba, haya yote tunayafanikisha na tunasaidiana.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo yako ya mwisho, umezungumzia masuala ya michezo na Ofisi za Wabunge. Naomba sana utaratibu huu wa viwanja vya michezo, hebu tuleteeni Wilaya zile mlizosema zina matatizo. Unaweza ukamfariji kijana au mwananchi kwa michezo, maana baada ya kutoka pale akishindwa atakwenda kuvuta bangi, atakwenda kufanya hili, mwisho wake wanakuwa wahuni au wakabaji.

Tunaomba basi TAMISEMI, safari hii, pamoja na Wizara husika ya Michezo, waandae Programu Maalum, kama mwaka huu ilishapita basi mwakani; kama inavyofanya mambo mengine, iweze kuandaa pesa kwa kuanzia kwa kushirikiana na Wananchi na Halmashauri, tuanze kujenga viwanja vya michezo katika kila Wilaya. Hivi ni vitu ambavyo vitatusaidia na kuweza kuitangaza nchi yetu na kuweza kupata pia vipaji vya watoto ambao ni wanamichezo wa kuweza kuja kuitangaza nchi hii katika ulimwengu huu tuliokuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sina la zaidi, naomba nirejee tena kuishukuru Serikali na ninawaambia Wananchi wa Mafia kwamba tupo, Serikali yenu ipo, mimi nipo na mtambo wa maji mnauona huo. Mimi nashirikiana na Serikali, tunachimba visima vizuri. Mwisho, ninaomba Serikali itutambue sisi tunaotoka Mafia. *(Makofi)*

Waziri wa Maji, naomba nikwambie nimechimba visima zaidi ya 20 katika Wilaya yangu, tena virefu na ghali. Sasa pale nitakapowaombeni misaada kwa kushindwa, naomba sana mliangalie.

La mwisho, kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kumwomba Waziri wa Maji aje Mafia yeye au Naibu wake. Ikishindikana basi anipe Wataalamu twende katika Kijiji cha Kisiwa cha Juani, akaangalie binadamu anavyokunywa maji ambayo wakati mwingine hata wewe mwenyewe utashtuka. Hali ya kisiwa kile ni mbaya sana, kwa hiyo, naomba hili suala aweze kutuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, zimesalia dakika tano kwa muda wetu wa kawaida wa kuahirisha Bunge. Kwa hiyo ni dhahiri huyu atakuwa mzungumzaji wetu wa mwisho kwa leo.

Orodha hii ya wachangiaji ina kasoro, ingawa imefuata jinsi ambavyo mmeomba, lakini Kanuni na taratibu zetu katika Bunge, zinatukumbusha kwamba, uchangiaji ni lazima uchukue sura inayozingatia pande za Muungano, Jinsia, Upinzani na Chama

Tawala, wazoefu na wale waliochaguliwa juzi. Kwa hiyo, kwa utaratibu huo, nimemwagiza Katibu aikarabati hii ili nipate sura hiyo.

Kwa hiyo, wale mliokuwa mmeniandikia hapa pengine mtapata bahati, lakini kama nilivyosema, idadi ni kubwa mno, wengine itabidi mzungumze wakati wa sekta.

Waheshimiwa Wabunge, si kweli kwamba katika orodha hii wapo walioongea wakati wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha hakuna; hawa wote ni wale ambao hawakuongea katika Hoja ya Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, kwa maana ya maandalizi ya kesho, ningeomba niwataje wanne tu wa mwanzo wengine wasubiri kidogo.

Tutaanza na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, atafutiwa na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, atafuatia Mheshimiwa Vita Kawawa na baadaye Mheshimiwa Grace Kiwelu. Huo ndiyo mtiririko wa hao wanne wa kwanza na waliobaki, Katibu ufanye ukarabati ili tupate uwakilishi au mchanganyiko mzuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naliahirisha Bunge hadi kesho Siku ya Jumanne, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 23 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)